# MIKAKATI YA KUFUNDISHIA STADI YA KUSOMA KWA KUTUMIA VITABU VYA HADITHI, KATIKA SHULE ZA MSINGI ZA KAUNTI YA KAKAMEGA NCHINI KENYA

**Lichuma Sussy Khakasa**

**Tasnifu iliyowasilishwa kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Taaluma ya Elimu ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro**

**NOVEMBA, 2018**

## UNGAMO NA IDHINISHO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa popote na yeyote kwa minajili ya shahada yoyote au jambo jingine lolote lile. Hairuhusiwi kutolesha tasnifu nzima au sehemu yake bila kibali cha mtafiti au Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Sahihi…………………………..............................................Tarehe……………………………

**Lichuma Sussy Khakasa**

**EDK/G/03/2015**

Tasnifu hii imeidhinishwa kwa kibali chetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Sahihi…………………………..............................................Tarehe……………………………

**1. Dkt. Susan C. Choge.**

Mhadhiri Mwandamizi,
Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi,
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia
cha Masinde Muliro.

Sahihi…………………………..............................................Tarehe……………………………

**2. Dkt. Fred Wanjala Simiyu**.

Mhadhiri Mwandamizi,
Idara ya Kiswahili na Lugha Zingine,
Za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii.

## HAKI MILIKI

Tasnifu hii ni hakimiliki kwa mujibu wa mkataba wa BERNE, kifungu cha sheria cha haki miliki cha mwaka wa 1999, kulingana na sheria na hataza za kitaifa na kimataifa. Hakuna kibali kutolesha au kuchapisha tasnifu hii au sehemu yake kwa namna yoyote bila idhini ya mwandishi au Mkuu wa Kitivo cha Taaluma ya juu kwa niaba ya chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

# TABARUKU

Kwa wazazi wangu marehemu Bw. Mwombe Charles na Marehemu Bi. Dinah Mwombe walinizaa na kunilea kwa mapenzi ya dhati hadi nikafikia umri huu wa kujitegemea kielimu. Mume wangu Nelson Muyundo Lichuma na wanangu wapendwa Clinton Mutali, Christopher Wamalwa, Collins Sibuchi Lichuma na Cohen Wafula Lichuma.

# SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati zimwendee Maulana kwa kunijalia siha njema, amani na maarifa ya kuandika tasnifu hii kwa jinsi hii. Asante Rabuka kwa kuwapa wanangu afya njema, kunipa nguvu na hekima ya kukabiliana na mambo magumu wakati wote wa masomo yangu.

Ninashukuru sana wote waliokuwa na msaada kwangu nilipokuwa nikisoma na wakati wa utafiti. Shukrani ziwaendee waelekezaji wangu Dkt. Choge Susan, Bw. Luganda Manasseh na Dkt. Wanjala Simiyu ambao walijitolea mhanga kuisoma kazi yangu, kunielekeza na kunishauri bila kuchoka.Vile vile ninatoa shukrani zangu kwa wahadhiri wote wa idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro ambao walinifaa wakati nilitaka usaidizi kutoka kwao hasa Dkt. Khalili Elizabeth, Bw. Opunde Shadrack, Bw. Marani John, Bw. Wanyama Eric na Bi. Rukia Salim.

Shukrani zangu za pekee zimwendee Marehemu mume wangu Nelson Lichuma kwa kunipa nafasi ya kujiendeleza kimasomo hasa kiwango cha shahada ya kwanza. Alinihimiza na kunipa mshawasha wa kuendelea na masomo. Mungu aiweke roho yake mahali alikomuandalia kule mbinguni. Siwezi kuwasahau wazazi wangu Marehemu Bw. Charles Mwombe na Dinah Navalayo ambao walinizaa, wakanilea, wakanielekeza na kuniwekea msingi bora katika masomo yangu. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaangazia kule mbinguni.

Sina budi kuwashukuru wanangu wapendwa ambao walijotolea kwa udi na uvumba kunisaidia nilipowahitaji.  Hawa ni Clinton Mutali, Christopher Wamalwa, Collins Lichuma na Cohen Lichuma. Aidha siwezi kumsahau kakangu mpendwa Simon Mwombe na dadangu Hellen Mwanzo kwa kuifadhili elimu yangu. Ahsanteni kwa michango yenu ya kunichipuza kuwa msomi.

Vilevile nawapa mkono wa tahania wazamili wenzangu, Okello Truphena na Oloo Mary Aluoch kwa kushirikiana kwa mambo mengi ya kitaaluma. Pia nawashukuru marafiki zangu walionitia shime kila wakati nilipohitaji msaada mpaka nikafikia kiwango hiki.Bila shaka ni sharti nimshukuru Mwalimu Mkuu na walimu wenzangu kwa kunitia moyo wa kuendea na masomo. Ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape maisha mazuri, na marefu yenye ufanisi.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika shule za Msingi za Manispaa ya Kakamega. Kusoma ni mojawapo ya stadi nne za lugha ambazo ni muhimu na za msingi katika maisha ya mwanafunzi ili aweze kuwasiliana na kufaulu katika masomo yake. Kuna wanafunzi wa darasa la nne ambao hawajajua kusoma na ambalo ni tatizo la kielimu. Hali hii ilimchochea mtafiti kufanya utafiti katika shule za msingi, Manispaa ya Kakamega katika kaunti ndogo ya Kakamega ya kati ya Kaunti ya Kakamega nchini Kenya. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubainisha vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi vinavyotumiwa na walimu wanapofundisha stadi ya kusoma, kuchunguza maandalizi ya walimu ya ratiba ya kazi, andalio la somo darasani na matumizi ya vitabu vya hadithi, kutambua mikakati ambayo walimu hutumia kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi na hatimaye, kupambanua majukumu ya mwanafunzi katika ukuzaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Utafiti huu ulifanyika katika shule za manispaa ya Kakamega, katika Kaunti ya Kakamega. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Utabia ya Skinner (Davis School District Curriculum and Instruction 2016, Laurete Education 2015, Rodgers 1976 na Skinner 1957) kuhusu ujifunzaji wa lugha kama mchakato wa uigaji na mazoea. Nadharia hii inafafanua kuwa ukuzaji na uimarishaji wa tabia hutokana na mazoezi anuwai ya kukariri na kurudiarudia. Nadharia hii ilitumiwa kuchunguza ukuzaji na uimarikaji wa tabia kutokana na motisha na mazoezi mengi ya kusoma vitabu vya hadithi. Muundo wa kimaelezo wa kisoroveya ulitumika kwa kuwa ulifaa utafiti huu. Mbinu za utabakishaji, maksudi na nasibu zilitumika kuteua shule za msingi 12, nane za umma nane na nne za kibinafsi.Walimu 65 wa Kiswahili pamoja na wanafunzi wao wa Kiswahili wa darasa la nne walihusishwa katika utafiti. Vifaa vya kukusanya data vilikuwa hojaji na mwongozo wa uchunzaji. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na kuwasilishwa kupitia kwa asilimia, majedwali, chati duara na maelezo yaliyotoka kwa watafitiwa. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa vitabu vya hadithi vina nafasi muhimu sana katika uimarishaji wa stadi ya kusoma. Utafiti uligundua kwamba ingawa matumizi ya vitabu vya hadithi ni njia nyepesi na muhimu sana ya kufunzia stadi ya kusoma baadhi ya walimu hawazingatii matumizi yavyo na wale wanaozingatia hufanya hivyo bila kuzingatia utaratibu kamili. Hivyo basi, utafiti umependekeza mikakati kabambe na ya dharura ifanyike ili vitabu vya hadithi viweze kutumika ipasavyo. Usomaji wa vitabu vya hadithi ufanywe kuwa jambo la lazima na hata kutahiniwa katika shule za msingi ili kutayarisha wanafunzi wa shule za msingi katika mtihani wa kitaifa. Mitihani hutegemea kusoma na kuandika hivyo basi mwanafunzi anayepata umahiri katika stadi ya kusoma ana nafasi nzuri ya kupita mtihani wake wa darasa la nane na kwa somo la fasihi afikapo shule za Upili na Vyuo Vikuu. Wizara ya Elimu na washikadau wengine wanastahili kushiriki katika jambo hili. Kusoma kwa upana husaidia kuimarisha stadi ya kusoma, matamshi bora, uakifishaji na miundo ya sentensi zinazotungwa na wanafunzi.

# ABSTRACT

The purpose of this study was to investigate the instructional strategies used in teaching reading skills using story books in primary schools. Reading skills are essential and a foundation for communication in life and a success to a learner in Education. It is appaling that some students can't read. A learner who is not able to read fluently encounters problems in communication and learning at school due to poor interpretation or low speed of reading. This study therefore sought to investigate the strategies used in teaching reading skills by using Kiswahili story books in class 4 within Kakamega municipality in Kakamega Central Sub-county of Kakamega County in Kenya. The strategies used by teachers included choosing the story books, teacher preparation, the use of the story books and the participation of the learners towards reading story books. The study was guided by the Behaviourism Theory which was proposed by Skinner. (Davis School District Curriculum and Instruction 2016, Laurete Education 2015, Rodgers 1976 and Skinner 1957). This theory explains the development of behaviour after repeated practice of activities. The theory explains that effective learning occurs when there is a lot of practice done through drilling and repeated activities as well as motivation. The study was guided by a descriptive survey. Stratified, purposeful and simple random sampling techniques were used in selecting 12 primary schools which included 8 public schools and 4 private schools which were used in this research. 65 teachers of Kiswahili and class 4 learners were included in the study. Questionnaires and classroom observation were utilized in data collection. Data was analysed in line with the objectives of the study and presented in simple percentages, tables, pie charts and explanations of the respondents derived from the answers of the respondents. The research findings showed that story books had an important role in enhancing the reading skills, despite some teachers hardly use them. Those attempting to use them do it without following any clear preparation. It is randomly done. The research recommends that proper strategies be put in place to enable teachers to use story books to enhance reading skills in an organized manner.Thereading of Kiswahili story books be made compulsory and examinable at primary level in preparation for the teaching of fasihi in secondary and university level of Education.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINISHO** ........ **ii**

**HAKI MILIKI** ........ **iii**

**TABARUKU** ........ **iv**

**SHUKRANI** ........ **v**

**IKISIRI** ........ **vi**

**ABSTRACT** ........ **vii**

**YALIYOMO** ........ **viii**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ **xiii**

**VIELELEZO** ........ **xiv**

**MAELEZO YA VIFUPISHO** ........ **xv**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ........ **1**

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti ........ 1

1.2 Suala la Utafiti ........ 4

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 5

1.4 Maswali ya Utafiti ........ 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 6

1.6 Tahadhania za Utafiti ........ 7

1.7 Nadharia ya Utafiti ........ 7

1.8 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 13

1.8.1 Upeo wa Utafiti ........ 13

1.8.2 Mipaka ya Utafiti ........ 14

1.9 Hitimisho ........ 14

1.10 Maelezo ya Istilahi ........ 15

**SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI ........ 17**

2.1 Utangulizi ........ 17

2.2 Stadi ya kusoma ........ 17

2.3 Vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi ........ 18

2.3.1 Uteuzi wa Vitabu vya Hadithi ........ 19

2.4 Nafasi ya Vitabu vya Hadithi katika Ufunzaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kusoma ........ 19

2.5. Jinsi ya kufunza Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Kitabu vya Hadithi ........ 22

2.6 Maandalizi ya Mwalimu katika Kufundisha Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi ........ 24

2.7 Mikakati ya kufundishia Stadi ya Kusoma ........ 27

2.7.1 Mazingira ya Kusoma ya Nje ya Shule ........ 29

2.7.2. Mazingira ya Shule za Msingi ........ 29

2.8 Majukumu ya Mwanafunzi katika Kukuza Stadi ya Kusoma ........ 30

2.9 Tafiti za hivi karibuni ........ 31

2.10 Hitimisho ........ 35

**SURA YA TATU: MUUNDO NA MBINU ZA UTAFITI ........ 36**

3.1 Utangulizi ........ 36

3.2 Muundo wa Utafiti ........ 36

3.3 Eneo la Utafiti ........ 37

3.4 Idadi Lengwa ........ 38

3.5 Uteuzi wa Sampuli ........ 38

3.5.1 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli ........ 39

3.5.2 Sampuli Teule ........ 40

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 41

3.6.1 Njia za Ukusanyaji wa Data ........ 41

3.6.2 Vifaa vya Ukusanyaji wa Data ........ 42

3.6.2.1 Maswali ya Hojaji ........................................ 42

3.6.2.2 Mwongozo wa Uchunzaji ........................................ 43

3.7 Uthabiti wa Vifaa ........................................ 44

3.8 Uaminifu wa Vifaa ........................................ 44

3.9 Majaribio ya Vifaa vya kukusanya Data ........................................ 45

3.10 Utaratibu wa Kukusanya Data ........................................ 45

3.11 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ........................................ 46

3.12 Matatizo Nyanjani ........................................ 46

3.13 Hitimisho ........................................ 47

**SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO ... 48**

4.1 Utangulizi ........................................ 48

4.2 Vigezo vya Uteuzi wa Vitabu vya Hadithi ........................................ 48

4.2.1 Vitabu vyenye Kiwango cha Wanafunzi Kilugha ........................................ 48

4.2.2 Vitabu Vinavyoeleweka kwa Urahisi ........................................ 49

4.2.3 Vitabu Vinavyoeleweka kwa Urahisi ........................................ 50

4.2.4 Vitabu Vilivyo na Vichoro na Picha ........................................ 50

4.2.5 Vitabu Vyenye Kurasa Chache. ........................................ 51

4.3 Maandalizi ya Walimu Darasani ........................................ 52

4.3.1 Umilisi wa Mwalimu ........................................ 55

4.4 Namna Walimu Wanavyotumia Vitabu vya Hadithi Kufundishia Stadi ya Kusoma ............. 56

4.4 Vipindi Vilivyotengewa Kusoma Vitabu vya Hadithi ........................................ 59

4.5 Mikakati ya Kufundishia Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi ...................... 60

4.5.1 Mikakati Andalizi kwa Matumizi ya Vitabu vya Hadithi ........................................ 60

4.5.2 Mikakati ya kufundisha kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi Darasani........................ 62

4.5.2.1 Kuongoza Wanafunzi Kukariri sauti na kusaidia wenye Matatizo ........................................ 64

4.5.2.2 Matumizi ya Vibonzo, Ramani, Michoro na Picha Zilizomo Vitabuni ............................ 65

4.5.2.3 Makadirio ya Walimu kwa Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Mikakati ............................ 67
4.5.3 Mazingira ya Kusoma ................................................................................................ 68
4.5. 3.1 Mazingira yaNdani na Nje ya Shule za Msingi ............................................................ 68
4.5.3.2 Uwepo wa Maktaba Shuleni. ...................................................................................... 69
4.5.3.3 Utoshelevu wa Vitabu vya Hadithi .............................................................................. 70
4.6 Majukumu ya Mwanafunzi ............................................................................................ 71
4.6.1 Kuwepo kwa Wanafunzi Wasio na Uwezo wa Kusoma. ................................................ 72
4. 6. 2 Jinsi ya Kusoma ........................................................................................................ 73
4. 6 .2.1 Kusoma kwa Kufululiza ............................................................................................ 73
4.6.2.2 Kusoma Pasi na Kumumunya Kidomo, Kufuatiliza Kidole au Kusogeza Kichwa Anapotamka Kila Sauti ................................................................................................ 74
4.7 Hitimisho ..................................................................................................................... 75
**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ............................ 76**
5.1 Muhtasari wa Tasnifu .................................................................................................... 76
5.2 Muhtasari wa Matokeo .................................................................................................. 76
5.2.1 Vigezo vya Uteuzi wa Vitabu ...................................................................................... 76
5.2.2 Maandalizi ya Walimu ................................................................................................ 77
5.2.3 Mikakati ya Kufundisha Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi .................... 77
5.2.4 Majukumu ya Wanafunzi ............................................................................................. 81
5.3 Hitimisho ..................................................................................................................... 82
5.4 Mapendekezo ............................................................................................................... 83
5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ........................................................................................ 84
**MAREJELEO ................................................................................................................ 86**
**VIAMBATISHO .............................................................................................................. 96**
KIAMBATISHO 1: Hojaji ya Mwalimu ............................................................................... 96
KIAMBATISHO 1.1 Hojaji iliyojazwa na mtafitiwa ............................................................ 101

KIAMBATISHO 1.2 Hojaji iliyojazwa na mtafitiwa ............................................................ 106

KIAMBATISHO 1.3: Hojaji iliyojazwa na mtafitiwa ............................................................ 111

KIAMBATISHO 2: Mwongozo wa Uchunzaji ........................................................................ 115

KIAMBATISHO 2.1 Mwongozo wa uchunzaji uliojazwa na mtafitiwa. ................................ 119

KIAMBATISHO 3: Shule za Msingi za Manispaa ya Kakamega ............................................ 122

KIAMBATISHO 4: Shule ya Msingi ya Sgs muhula wa 1 2016 ............................................ 123

KIAMBATISHO 5: Shule ya Msingi ya Bkn Darasa la tatu muhula wa 3 2016 ..................... 124

KIAMBATISHO 6: Shule ya Msingi ya Sgs Muhula wa 3 2016 ............................................ 125

KIAMBATISHO 7: Matumizi ya vitabu vya hadithi darasani. ................................................ 126

KIAMBATISHO 8: Ramani ya Eneo la Utafiti ........................................................................ 127

KIAMBATISHO 9: Kaunti Ndogo ya Kakamega ya Kati ....................................................... 128

KIAMBATISHO 10: Barua ya Idhinisho la Pendekezo la Utafiti ............................................ 129

KIAMBATISHO 11: Kibali cha utafiti na Wizara ya Elimu .................................................... 130

KIAMBATISHO 12: Kibali cha Utafiti cha NACOSTI .......................................................... 131

KIAMBATISHO 13: Kibali cha Utafiti cha Nacosti ................................................................ 132

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali 3.1** Sampuli teule ........ 41

**Jedwali 4.1** Vitabu vyenye Kiwango cha Wanafunzi Kilugha ........ 49

**Jedwali 4.2** Vitabu Vinavyoeleweka kwa Urahisi ........ 50

**Jedwali 4.3** Vitabu Vilivyo na Michoro na Picha. ........ 51

**Jedwali 4.4** Vitabu Vyenye Kurasa Chache. ........ 52

**Jedwali 4.5** Maandalizi ya Mwalimu: Data ya Hojaji ........ 53

**Jedwali 4.6** Stadi za Lugha. ........ 55

**Jedwali 4.7** Matumizi ya Vitabu vya Hadithi. ........ 57

**Jedwali 4.8** Mikakati ya Kufundishia kwa Matumizi ya Vitabu vya Hadithi Darasani ........ 63

**Jedwali 4.9** Kuongoza Wanafunzi Kukariri na Kusaidia Wenye Matatizo ........ 64

**Jedwali 4.10** Jinsi ya Kusoma Vitabu vya Hadithi. ........ 67

**Jedwali 4.11** Uwepo wa Maktaba Shuleni ........ 69

**Jedwali 4.12** Wanafunzi Wasiokuwa na Uwezo wa Kusoma. ........ 72

**Jedwali 4.13** Uwepo wa Wanafunzi Wenye Uwezo wa Kusoma Wakifululiza ........ 73

**Jedwali 4.14** Uwepo wa Wanafunzi Wenye Udhaifu wa Kusoma. ........ 75

## VIELELEZO

**Kielelezo 4.1**: Maandalizi ya Mwalimu: Data ya Uchunzaji ........ 54

**Kielelezo 4.2**: Mikakati ya Kufundishia Stadi ya Kusoma ........ 58

**Kielelezo 4.3:** Vipindi Vilivyotengewa Kusoma Vitabu vya Hadithi ........ 59

**Kielelezo 4.4:** Mikakati Andalizi kwa Matumizi ya Vitabu vya Hadithi ........ 62

**Kielelezo 4.4:** Picha Vibonzo, Ramani, Michoro na Picha. Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti ....... 66

**Kielelezo 4.5:** Utoshelevu wa Vitabu vya Hadithi ........ 70

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **K.I.E:** | Kenya Institute of Education. |
| **MMUST:** | Masinde Muliro University of Science and Technology. |
| **M.Phil:** | Master of Philosophy. |
| **TUKI:** | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. |
| **UM:** | Shule za Umma. |
| **KB:** | Shule za Kibinafsi |
| **8-4-4:** | Mfumo wa Elimu wa miaka nane katika shule za msingi, kwa shule za upili miaka minne na miaka minne katika chuo kikuu. |
| **K.I.C.D:** | Kenya Institute of Curriculum Development. |
| **UNESCO:** | United Nations Education Scientific and Cultural Organization.<br>Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Elimu Utamaduni Sayansi na |
| **NACOSTI:** | National Commission for Science, Technology and Innovation. |
| **NESSP:** | National Educational Sector Support Programme. |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Stadi za lugha ni maarifa au ujuzi unaotumiwa na watu katika kuwasiliana kwa kutumia lugha. Kuna stadi nne kuu za lugha ambazo ni kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Kila stadi ina nafasi yake maalum katika mchakato wa mawasiliano (Wanjala na Kavoi, 2013). Kusoma ni uwezo wa kutambua alama za sauti zilizowasilishwa kimaandishi au ni uwezo wa kutambua ishara zinazoandikwa kimantiki ili kutoa maana au ufahamu wa jambo fulani. Stadi ya kusoma hukuzwa baada ya stadi za kusikiliza na kuongea. Anayesoma anatarajiwa kutambua maneno katika tungo na muundo wa tungo ili kufahamu ujumbe unaowasilishwa na tungo au kifungu cha maneno husika na kutambua matumizi ya viakifishi.

Kusoma ni stadi mojawapo ya stadi nne ambazo ni muhimu kwa mwanafunzi kwa vile humwezesha kuelewa yale anayosoma kwa miaka yake ya mwanzo wa kusoma. Iwe ni kusoma kwa sauti au kimya, kusoma vitabu vya hadithi hukuza lugha ya mwanafunzi, msamiati wake na ujuzi wa kujieleza katika lugha hiyo. Kulingana na Silabasi (KIE 2002) ya shule za msingi mwanafunzi anahitajika kusoma kwa ufasaha afikapo darasa la tatu. Wanjala na Kavoi (2013) wanaeleza ya kwamba kusoma ni stadi ya msingi katika mawasiliano hususan kwa kutumia maandishi. Stadi hii hujenga msingi imara wa masomo ya wanafunzi (Teale 2003).

Mwanafunzi anapokosa kujua kusoma katika kiwango hiki huwa na changamoto ya kutoelewa anayosoma na hivyo hawezi kuwasiliana, kujibu maswali darasani na hata katika mitihani yake. Kulingana na utafiti uliofanywa na Shirika la Uwezo Kenya (2010), 43% ya wanafunzi wa madarasa ya nne na tano ya shule za msingi nchini kote hawakuweza kusoma sentensi za darasa la pili. Nusu ya hawa wanafunzi wakiwa wa madarasa ya nne na tano. Idadi kubwa ya wanafunzi wasioweza kusoma ilitoka katika eneo la Kakamega ya kati ikiwa 61%, Hamisi 59%, Bungoma 42%. Wanafunzi 39% ya madarasa ya juu ndio waliweza kusoma. Hii

inaonyesha ya kwamba 61% ya wanafunzi katika eneo la Kakamega ya kati ambapo manispaa ya Kakamega ipo hawakuweza kusoma kwa ufasaha. Uchunguzi wa mwalimu kuhusu matokeo ya wanafunzi wa darasa la nne katika shule za manispaa ya Kakamega unaonyesha kuwa kuna wanafunzi ambao hawawezi kusoma maneno na sentensi za Kiswahili. Ithibati za kitakwimu katika baadhi ya shule zinashadidia madai haya (tazama viambatisho 4, 5,6)

Kukosa kujua kusoma huathiri namna mwanafunzi anavyoandika lugha ya Kiswahili. Somo la Kiswahili hukuza, huimarisha na kuendeleza Kiswahili kama lugha ya taifa na hutahiniwa katika darasa la nane na kidato cha nne kama somo la lazima (Republic of Kenya, Tume ya Mackay 1981) na hivyo mwanafunzi asipojua kusoma na kuandika hatafaulu katika somo la Kiswahili. Kwa mujibu wa Dewey (1966), stadi ya kusoma ni uti wa mgongo wa ufundishaji na ni maarufu sana katika utekelezaji wa masomo ya kielimu. Stadi ya kusoma imefundishwa kwa kutumia mikakati tofauti kwa miaka mingi. Kwa mujibu wa KIE, (2002) wanafunzi wa Shule za Msingi wanahitaji kusoma vitabu vya hadithi ili kuimarisha Stadi ya Kusoma. Mwanafunzi anayesoma vitabu vya hadithi kwa upana huweza kujenga msamiati wake, uakifishaji na miundo ya sentensi. Vilevile wanafunzi hupata msingi bora wa kuandika insha ambazo hutahiniwa katika darasa la nane na kidato cha nne. Hivyo basi, mtafiti alichochewa sana na takwimu hizi na akaamua kutafitia ili kuelewa kama kweli walimu wanazingatia mikakati iliyopendekezwa kwenye Silabasi ya kufundisha stadi ya kusoma katika Shule za Msingi.

Musau na Chacha (2001) wanaeleza umuhimu wa kusoma kwa njia tofauti. Wanaeleza ya kwamba kusoma kwa ziada humfurahisha na kumburudisha mwanafunzi. Ikumbukwe kwamba mwanafunzi hupelekwa shuleni ili kupata ujuzi wa kusoma. Anasoma ili aelewe mambo anayofundishwa katika masomo, hana uchaguzi katika jambo hili. Lengo la nne katika Malengo Endelevu (Sustainable Development Goals) linasisitiza kuwepo kwa elimu bora katika nchi ya

Kenya. Vilevile mojawapo ya malengo ya elimu ni kumkuza mwanafunzi hadi afikie kilele chake (KIE, 2002). Hili linawezekana ikiwa mwanafunzi atapewa nafasi ya kusoma, kuelewa matini, kusoma na kujibu maswali na kusoma kwa kujifurahisha. NESSP (2013-2018) imeshughulikia hali ya kujua kusoma nchini kwa kutoa madhumuni ya kuimarisha elimu na malengo ya kuchangia ufanisi wa Maono ya Kenya ya 2030.

Kulingana na Njogu na Nganji (2011) kategoria tofauti za Stadi ya Kusoma zimeainishwa kama ifuatavyo: Kusoma kwa sauti, Kusoma kwa ufahamu, Kusoma kwa ziada au mapana na kusoma kwa kujifurahisha. Kusoma kwa sauti hulenga matamshi bora na kwa kasi bila kusitasita. Mwalimu ni sharti ateue maneno, sentensi, vifungu, taarifa au vitabu kisha awagize kusoma akisikiliza jinsi wanapotamka. Baadaye awaongoze wanafunzi kutambua matamshi mabaya, yasiyo sahihi na awashirikishe kurekebisha kwa kuiga matamshi bora akiongozwa na nadharia ya utabia inayosisitiza uigaji.

Kusoma kwa ufahamu kunahusisha usomaji kimya au kwa sauti ambapo mwalimu huwashirikisha wanafunzi kusoma kisha wajibu maswali kwa kutegemea ngazi sita za maarifa kulingana na Bloom. Kusoma kwa ufahamu ni usomaji ambao hupima kiwango cha wanafunzi cha uelewa wa lugha. Katika kategoria hii mwanafunzi hupewa makala fulani kuyasoma na kuonyesha ufahamu wake kwa kujibu maswali. Kategoria nyingine ni kusoma kwa kina kunakoweza kukadiriwa kupitia kwa maswali ya ufupisho. Mwalimu ana jukumu la kuwachagulia wanafunzi sehemu katika kitabu kiteule halafu awaulize kusoma kisha waeleze ujumbe unaojitokeza kwa ufupi.

Kusoma kwa mapana ni kategoria nyingine ya stadi ya Kusoma ambayo huhusisha usomaji wa maktabani. Mwalimu humwuliza mwanafunzi kueleza ujumbe unaojitokeza katika makala, jarida, gazeti au kitabu alichokisoma. Pia mwalimu awaelezee wanafunzi kusoma maelezo ya matumizi ya kamusi. Baadaye mwalimu awaulize maswali ya kutafuta maneno katika kamusi na namna ya kutumia vitomeo mbalimbali.

Kwa hivyo utafiti huu ulijikita katika kategoria ya kusoma kwa mapana. Kusoma kwa mapana ni aina ya kusoma ambayo humwezesha mwanafunzi kupanua elimu yake kuhusu stadi ya kusoma na pia uelewa wake wa tamaduni, watu na mahali. Chall na Stahl (1988) wanaeleza ya kwamba ufundishaji wa stadi ya kusoma huzingatia matamshi bora na maana, na mwalimu anafaa kueleza lengo la kusoma habari husika, kisha ahusishe habari hizo na tajriba za awali za mwanafunzi. Aidha mwalimu aeleze maana za maneno mapya yaliyotumiwa kisha awaelekeze wanafunzi namna ya kusoma kwa kuzingatia uakifishaji. Kwa hivyo, walimu wana jukumu la kuchagua mikakati na nyenzo faafu za kufundishia stadi ya kusoma. Maoni ya watafiti hawa yanathibitisha kuwepo na pengo la matumizi ya vitabu vya hadithi kwa kuimarisha stadi ya kusoma.

Hill (1999) naye anawashauri walimu kuwapa wanafunzi fursa ya kuchagua habari au vitabu wanavyotaka kusoma kisha baadaye majadiliano yaandaliwe kuhusu walichokisoma na changamoto walizokumbana nazo. Kwake, mojawapo ya lengo la kufundisha kusoma ni kumsaidia mwanafunzi kuchuja habari na kupata mambo muhimu yanayoafikiana na mahitaji yake.

Ilikuwa katika misingi hii ndipo mtafiti alichochewa kuchunguza mikakati inayotumiwa na walimu katika kufundisha stadi ya kusoma katika darasa la nne. Utafiti ulichunguza vigezo vinavyotumiwa kwa kuteua vitabu vya hadithi vinavyosomwa na majukumu yafanywayo na wanafunzi ili kuimarisha stadi ya kusoma.

## 1.2 Suala la Utafiti

Stadi ya kusoma ni mojawapo ya stadi nne ya masomo yaliyomo katika silabasi ya shule za Msingi (K.I.E. 2002). Stadi nyingine zikiwa kusikiliza, kuongea na kuandika. Stadi ya kusoma ni muhimu katika kukuza, kuimarisha na kuendeleza Kiswahili kama somo na lugha ya kitaifa. Uwezo Kenya (2010) ilibainisha kuwa kuna baadhi ya wanafunzi wanaofika darasa la tatu wakiwa hawana uwezo wa kusoma kwa ufasaha. Hata hivyo hakuna aliyefanya utafiti juu ya

stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika shule za msingi katika Manispaa ya Kakamega, kaunti ndogo ya Kakamega ya Kati. Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza namna vitabu vya hadithi vinavyotumiwa kufundishia stadi ya kusoma katika darasa la nne, Manispaa ya Kakamega ya Kaunti ya Kakamega. Vilevile utafiti huu ulichunguza maandalizi ya mwalimu na matumizi ya vitabu vya hadithi kama nyenzo za kufundishia stadi ya kusoma ili kukuza na kuimarisha usomaji wa mwanafunzi wa darasa la nne Manispaa ya Kakamega. Utafiti huu ulilenga kubainisha jinsi mkakati huu ulivyotumiwa katika ufundisha stadi ya Kusoma katika darasa la nne, Manispaa ya Kakamega ya kaunti ya Kakamega.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mikakati inayotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika darasa la nne. Ili kutimiza lengo hili mtafiti aliongozwa na malengo mahsusi yafuatayo:

1. Kujadili vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi vinavyotumiwa na walimu wanapofundisha stadi ya kusoma.
2. Kuchunguza maandalizi ya walimu ya ratiba ya kazi, andalio la somo darasani na matumizi ya vitabu vya hadithi.
3. Kutathmini mikakati ambayo walimu hutumia kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.
4. Kupambanua majukumu ya mwanafunzi katika ukuzaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

1. Je, ni vigezo vipi vinavyotumiwa na walimu katika kuteua vitabu vya hadithi vya kufundishia stadi ya kusoma?
2. Je, walimu wa Kiswahili huandaa ratiba ya kazi, andalio la somo darasani na Matumizi yavitabu vya hadithi?

3. Walimu hutumia mikakati ipi katika kufundisha stadi ya kusoma?
4. Mwanafunzi huchangia kwa njia gani ukuzaji wa stadi ya kusoma kupitia usomaji wa vitabu vya hadithi?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na manufaa ya kuimarisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Kutokana na utafiti huu mikakati bora ya kufundishia stadi ya kusoma ambayo inaweza kutumiwa na walimu ilibainishwa. Utafiti huu unatarajiwa kuwa na manufaa kwa makundi mbalimbali. Matarajio ya mtafiti ni kwamba utafiti huu utaweza kuwasaidia wanafunzi kuimarisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

Pia utafiti ungewafaa walimu hasa wanapofundisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi kwa kuchuja mikakati ya ufundishaji wao darasani. Hii itawaelekeza walimu na washikadau kutoa mwelekeo ulio bora wa matumizi ya vitabu vya hadithi ili kuwapa wanafunzi ari ya kusoma vitabu vya hadithi kwa wingi. Hali hii itawawezesha wanafunzi kusoma vitabu kama vile riwaya, tamthilia na hadithi fupi katika ujifunzaji wa fasihi wafikiapo shule za upili. Kwa hivyo kutokana na uchunguzi wa mikakati ya kufundishia inayotumiwa na walimu wa shule za msingi, utafiti huu uliazimia kutoa kanuni za usomaji wa vitabu vya hadithi ukiwa msingi wa fasihi.

Vilevile utafiti huu ni muhimu kwa vile unanuiwa kuwasaidia waandishi kuandika na kuchapisha zaidi kuhusu umuhimu wa vitabu vya hadithi ili kuimarisha stadi ya kusoma. Aidha utafiti huu unatarajia kuwasaidia walimu kujisaili na kubadili mtazamo wao hasi kuhusu usomaji wa vitabu vya hadithi ili waone umuhimu wake wa kufaulisha ufundishaji wa stadi ya kusoma.

## 1.6 Tahadhania za Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika misingi ya machukulio yafuatayo:

1. Inachukuliwa kuwa kuna vitabu vya hadithi shuleni.
2. Inachukuliwa kuwa silabasi ya masomo ya shule za msingi imebainisha mikakati ya kufundishia stadi ya usomaji kwa kutumia vitabu vya hadithi.
3. Walimu wote hutayarishwa katika vyuo vya ualimu kutumia mikakati mbalimbali ya ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.
4. Inachukuliwa pia kuwa watafitiwa watatoa majibu sahihi.

## 1.7 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utabia iliyoasisiwa na Skinner (1957). Nadharia hii imeendelezwa kwa mitazamo tofauti na wataalamu mbalimbali. Wa hivi karibuni kutumia nadharia hii ni Davis School District Curriculum (2016) iliyochunguza jinsi wanafunzi wanavyojifunza. Laurete Education (2015) iliangalia nafasi ya urudiaji, ukariri na uimarikaji katika ukuzaji chanya na hasi darasani. Skinner aliona kuwa ujengaji wa tabia nzuri ni kupitia uigaji, urudiaji na utuzaji wa matendo mazuri. Hawa walitafiti zaidi na kuimarisha nadharia ya Skinner na kuongezea kuwa ingawa ujifunzaji wa lugha ni mwigo, vilevile ni uimarikaji wa tabia. Kuwa tabia huimarishwa kwa matumizi ya vitia motisha chanya. Vichocheo hasi vya motisha hupunguza uwezekano wa tabia fulani kurejelewa na vitia motisha chanya ambavyo huzidisha uwezekano wa tabia hiyo kurejelewa tena na tena. Utafiti huu umefanywa kwa kujikita katika mipaka ya kanuni za umotishaji na ujenzi wa mielekeo. Nadharia hii huchukulia ujifunzaji wa lugha kama mchakato wa uigaji na mazoezi. Kwa mkabala huu, wanaojifunza lugha huzingatia wanachosikia na kukuza mazoea fulani katika lugha wanayojifunza. Nadharia hii inasisitiza juu ya upataji na mabadiliko ya uwezo wa tabia yanayotokana na michakato ya ujifunzaji na mazoea yataaluma fulani katika mazingira

mahususi. Kwa mujibu wa kimble (1961) mabadiliko haya hutokea kutokana na mazoezi yanayoimarishwa.

Skinner (1957), Rodgers (1976), na Davis School District Curriculum and Instruction (2016) walichangia utabia kwa kuendeleza nadharia ya kutia motisha ambayo inahusu ubadilishaji wa tabia kutokana na matumizi ya kitia motisha ambacho hutolewa baada ya tabia inayotakikana. Kulingana na wataalamu hawa, uwezo na tabia ya kiumbe hudumishwa kwa msingi wa kutosheleza mahitaji ya aina fulani kwa sababu ya kuwa na kitu kinachodhihirisha au matokeo ridhishi yanayotarajiwa kutokana na tabia hiyo. Nadharia hii inasisitiza utuzaji ili kuboresha utendaji kazi. Kwake Skinner, matarajio ya kupata matokeo chanya katika somo la stadi ya kusoma humtia mwanafunzi hamasa ya kufaulu. Walimu wakichukulia kuwa hawatapata yatakayowaridhisha baada ya somo, hawafanyi bidii hivyo hukosa kulifikia lengo lao la somo la Kiswahili. Kwa undani zaidi, wavithamini na wateue mikakati mwafaka zitakazo waathiri wanafunzi wao kichanya. Mwalimu aliyebobea katika tajriba ya ufundishaji hutumia mikakati na vifaa mbalimbali kuwaelekeza wanafunzi wake somoni ili wajifunze vilivyo (Orodho,1996).

Nadharia ya utabia, ina mihimili ifuatayo:

i. Kukariri na kurudiarudia matamshi ya vipande vya mazungumzo (tamthilia ndogo), miundo ya sentensi na drili za aina aina.

ii. Tabia nzuri katika kujifunza lugha ya pili hujengeka vizuri ikiwa mwanafunzi ataelekezwa vizuri kutofanya makosa.

iii. Vipengele vya lugha vifundishwe kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza kwanza kabla ya kusoma na kuandika.

iv. Ufundishaji wa sarufi na vipengele vingine vya lugha usifanywe kwa kuchambua vipengele vya lugha. Mwanzoni wanafunzi wakariri na kurudia na kuiga vipengele hivyo na kuvizoea. Wakifanya hivyo, watang'amua wao wenyewe kwa njia ya kukisia kanuni zinazotawala lugha. Kwa mfano, wakirudia na kukariri msamiati watauelewa bila kuelezwa maana na kutumia kamusi.

v. Ufundishaji wa sarufi ya lugha ya pili uendeshwe kwa kukariri tamthilia zilizo na miundo ya kisarufi inayofundishwa.

vi. Jukumu la mwanafuzi ni kufuata maagizo, ilhali lile la mwalimu ni muhimu sana kwani ndiye kiongozi wa kila jambo darasani. Hususan mwalimu anatuza matamshi yaliyo sahihi, miundo ya sentensi pamoja na vipande vya tamthilia vinavyorudiwa na kukaririwa ili tabia ya lugha ijengeke.

vii. Kujifunza lugha ni sawa na kujenga ujuzi wa vipashio vya lugha, kama vile fonimu, mofimu na vifungu vya maneno. Kwa sababu hiyo, matamshi yafundishiwe mwanzo na sarufi au miundo ya kisarufi baadaye (Musau na Chacha, 2001)

**Mihimili mitano iliyotumika katika utafiti huu kwa kurejelea malengo ni kama ifuatavyo:**

i. Vipengele vya lugha vifundishwe kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza kwanza kabla ya kusoma na kuandika. Mwalimu wa Kiswahili anaweza kuwasomea wanafunzi maneno, sentensi na vifungu kutoka kwa vitabu vya hadithi vilivyoteuliwa kwa misingi iliyopendekezwa na Wizara ya Elimu na wataalamu wa elimu. Wanafunzi watapata fursa ya kumsikiliza mwalimu na kuiga matamshi yake. Hivyo mwalimu anafaa kujaribu kuwa na ufasaha kimatamshi ili asiwapotoshe wanafunzi. Hatua ya kuzungumza kwa kuiga matamshi ya mwalimu itarahisisha ujifunzaji wa stadi ya kusoma. Nadharia inasisitiza kukariri na kurudiarudia

matamshi ya vipande vya mazungumzo (tamthilia ndogo na hadithi), miundo ya sentensi na drili za aina aina. Madhumuni ya kukariri na kurudia yalikuwa ni kujaribu kujenga tabia ya lugha iliyo sahihi, tabia au lugha isiyo na makosa na athari za lugha mama. Katika nadharia hii, makosa yalionekana kama kikwazo cha kujenga tabia nzuri. Kutokana na usomaji wa vitabu vya hadithi, mwalimu atapata nafasi ya kuongoza wanafunzi katika kutamka sauti, maneno, sentensi na vifungu fulani katika vitabu vya hadithi huku akirekebisha makosa ya matamshi ya wanafunzi wake na kujenga ufasaha utakaojitokeza katika mazungumzo na kujibu maswali ya Kiswahili katika maandishi. Kulingana na mhimili huu, tabia inayoigwa huhitaji kufanyiwa mazoezi ili kuimarishwa na kudumishwa. Nadharia ya utabia ina azma ya kuhimiza walimu wa Kiswahili kuteua na kutumia nyenzo zinazohitilafiana katika kufundisha. Matumizi ya nyenzo za ufundishaji katika somo la Kiswahili ni shughuli ambayo imependekezwa na wanasaikolojia wengi wa elimu. Nyenzo huwawezesha walimu kudhibiti hali, mihemko na uelewa wa wanafunzi wao (Nsubugha, 2000). Hali hii husababisha mielekeo chanya kuhusu somo la Kiswahili ambapo mwanafunzi huendeleza stadi hii kwa kuifanyia mazoezi zaidi ya kibinafsi na ndivyo nadharia ya utabia inahimiza katika matumizi yake. Kuwa nyenzo hunata nadhari ya mwanafunzi na humwezesha kuwa na kumbukumbu ya yale aliyoshughulikia katika somo la Kiswahili kwa muda mrefu.

ii. Tabia nzuri katika kujifunza lugha ya pili hujengeka vizuri ikiwa mwanafunzi huelekezwa vizuri kutofanya au kuepukana na makosa. Kutokea kwa makosa ni jambo la hatari kwa sababu makosa haya huenda yakawa tabia. Kwa mujibu wa nadharia hii, makosa yanapaswa kutotuzwa yaani kukatizwa au kuadhibiwa ili yasitokee tena. Schultz na Schultz (1987) nao wanakubaliana na maoni ya Skinner kwa kusema kuwa, ili tabia fulani idumu, yafaa kuigwa,

kurudiwarudiwa pamoja na kutuzwa la sivyo hufifia na baadaye hupotea kabisa. Musau na Chacha (2001) wanakubaliana na kauli hii kwa kusisitiza kuwa tabia isiyorudiwarudiwa kwa njia ya mazoezi hufifia na hata mwishowe hupotea kabisa. Wanafunzi hujifunza mchakato wa kujifunza darasani kupitia utabia. Nadharia ya utabia pia yasisitiza matumizi ya miitiko inayotoka kwenye mazingira ambayo huzidisha uwezekano wa tabia fulani kurejelewa tena na tena. Hivyo basi, mazoezi na utuzaji ni muhimu katika somo la stadi ya kusoma ili kuboresha utendaji wao. Kwa hivyo, wanafunzi wanahitajika kusoma vitabu vya hadithi kila mara yaani wawe na mazoea ili kuimarisha stadi ya kusoma.

iii. Ufundishaji wa sarufi na vipengele vingine vya lugha usifanywe kwa kuchambua vipengele vya lugha. Mwanzoni wanafunzi wakariri kwa kurudia na kuiga vipengele hivyo na kuvizoea kutoka kwa vitabu vya hadithi.Wakifanya hivyo, watang'amua wao wenyewe kwa njia ya kukisia kanuni zinazotawala lugha. Kwa mfano, wakirudia na kukariri msamiati unaopatikana katika sentensi na vifungu katika vitabu hivyo, watauelewa bila kuelezwa maana na kutumia kamusi.

iv. Kujifunza lugha ni sawa na kujenga ujuzi wa vipashio vya lugha, kama vile fonimu, mofimu na vifungu vya maneno. Kwa sababu hiyo, matamshi yafundishwe mwanzo na sarufi au miundo ya kisarufi baadaye. Ufundishaji wa sarufi ya lugha ya pili uendeshwe kwa kukariri vifungu vya hadithi zilizo na miundo ya kisarufi inayofundishwa.Walimu wa lugha ya Kiswahili wanaweza kuazima kigezo kikuu cha utabia cha uigaji hasa wanapoazimia kurekebisha matumizi mabaya ya sarufi ndani na nje ya darasa. Ukariri wa sauti zinazokanganya na miundo ya tungo za Kiswahili ni mchango dhahiri wa ujuzi wa wanautabia. Kwa mfano baadhi ya sauti zinazoleta utata zinapotamkwa ni kama[s] na [sh] na [t] na [d] miongoni mwa

mwanafunzi wa darasa la nne (Mirikau, 2008). Ukariri wa sauti hizi miongoni mwa wanafunzi hawa wa Kiswahili hurekebisha matamshi yao mabovu.

v. Jukumu la mwanafuzi ni kufuata maagizo, ilhali lile la mwalimu ni muhimu sana kwani ndiye kiongozi wa kila jambo darasani. Hususan mwalimu anatuza matamshi yaliyo sahihi, miundo ya sentensi pamoja na vipande vya hadithi vinavyorudiwa na kukaririwa ili tabia ya lugha ijengeke. Kutokana na usomaji wa vitabu vya hadithi mara kwa mara kwa kuelekezwa na mwalimu, nadharia ya utabia inalenga kueleza namna tabia inavyojengeka. Hull na wenzake, (1943) wanaamini kuwa tabia hutokana na mtagusano wa mara kwa mara wa vitu mbalimbali kama vile nyenzo na mazingira. Mwalimu anapotumia vitabu vya hadithi katika somo la kusoma na kuwa mtindo, basi uzoefu huo huleta mvuto kwa wanafunzi. Mazingira ya wanafunzi katika ufundishaji wa somo la stadi ya kusoma huwa muhimu kwa darasa, jamii, nyenzo na hata walimu. Nadharia ya utabia inalenga walimu wa Kiswahili kuandaa mandhari ya ufundishaji pamoja na nyenzo wakishirikiana na wanafunzi wao ili kusababisha ukuruba mwema kati yao na hatimaye utendaji bora kwa wote (Dewey, 1966, Rodgers, 1976). Kwa hivyo wanafunzi wanahitaji kutumia vitabu vya hadithi kama nyenzo maalum katika ukuzaji wa stadi ya kusoma.

Nadharia ya utabia pia ilitumika na Iyaya (2010) katika tasnifu yake ya "Mambo yanayoathiri ufundishaji wa ushairi katika shule za sekondari. Iyaya anaeleza kwamba, mwalimu anapaswa kuwahusisha wanafunzi kukariri na kurudiarudia msamiati. Kwa hivyo nadharia ya utabia ilimwezesha mtafiti kuchunguza ukuzaji na uimarishaji wa tabia ya wanafunzi kutokana na mazoezi maridhawa ya kusoma vitabu vya hadithi wanapokuwa shuleni na nyumbani.

Mihimili hii imeafiki utafiti huu kwa njia mbalimbali. Shuleni wanafunzi wengi huchukulia somo la Kiswahili kuwa ni gumu kueleweka. Tabia ya mwalimu na mwanafunzi huhusishwa na

hali ya mazingira ya ufundishaji kwa mkabala wa matokeo duni kulingana na nadharia hii. Nadharia ya utabia ulinufaisha utafiti huu kwa utumiaji wa vitabu vya hadithi katika kujenga tabia ya mazoea ya kusoma Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi. Kusoma vitabu vya hadithi kila wakati ni mazoezi ya kuimarisha na kudumisha stadi ya kusoma. Nadharia hii ina azma ya kuhimiza walimu wa Kiswahili kuwapa wanafunzi vitabu mbalimbali vya hadithi ili kukuza lugha ya Kiswahili. Nadharia hii pia ilitumika katika kufafanua mitazamo ya walimu na wanafunzi kuhusu usomaji wa vitabu vya hadithi.

## 1.8 Upeo na Mipaka ya Utafiti

### 1.8.1 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Manispaa ya Kakamega ya Kaunti Ndogo ya Kakamega ya Kati. Eneo hili linajumlisha wadi za Sichirayi upande wa kaskazini, Mahiakalo upande wa magharibi na Shieywe upande wa mashariki. Eneo hili lina shule za msingi 39, ishirini na tano za umma na kumi na nne za kibinafsi ambazo zilitumiwa ili kuwakilisha zingine zote nchini. Baadhi ya shule hizi ni kama vile shule ya msingi ya Mhk, Bkn, Alm, Nbg, Fsb, Abt na Sht miongoni mwa zingine (tazama kiambatisho 5). Shule 12 zilichunguzwa, hii ikiwa ni asilimia thelathini ya shule thelathini na tisa ambazo zilikuwa idadi lengwa. Shule hizi ziliteuliwa na hali kwamba zingeweza kufikiwa kwa haraka na kupunguza gharama na wakati. Vilevile shule hizi ziliteuliwa kufuatia matokeo ya mtihani (tazama viambatisho 4,5 na 6) na utafiti wa hapo awali wa Uwezo Kenya ambao ulionyesha kuwa 61% ya wanafunzi wa darasa la 4 na 5 wa eneo hili hawakuweza kusoma kwa ufasaha. Mtafiti alichunguza mikakati ya kufundishia Stadi ya Kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Mtafiti alitumia mbinu za hojaji na uchunzaji katika ukusanyaji wa data.

Uchunguzi ulijikita katika darasa la nne. Njia za uchanganuzi wa data zilizotumiwa zilikuwa ni mara idadi na asilimia. Sampuli iliteuliwa kiutabakishaji, kimakusudi na kinasibu. Katika Shule zilizokuwa na zaidi ya mkondo mmoja, mkondo mmoja uliteuliwa kupitia uteuzi wa kinasibu.

Walimu 12 waliofundisha Kiswahili katika darasa la nne kutoka shule 12 teuliwa ndio waliofanyiwa uchunzaji darasani na walimu 65 waliofundisha Kiswahili katika mikondo yote ndio waliojaza hojaji.

Darasa la nne liliteuliwa kimakusudi kutokana na hali kwamba ndilo darasa ambalo usomaji wa hadithi ndefu na visa virefu hushamiri (Njogu na Nganje, 2011). Katika darasa la kwanza hadi la tatu wanafunzi huwa wangali kupiga hatua katika usomaji wa hadithi ndefu. Ilikuwa ni kwa misingi hii ndipo darasa la nne liliteuliwa.

### 1.8.2 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti Ndogo ya Kakamega ya Kati na haukuhusisha Kaunti Ndogo zingine. Huenda Kaunti Ndogo zingine zingekuwa na matokeo tofauti. Utafiti ulihusisha tu wadi za Mahiakalo, Sichirayi na Shirere, haukuhusisha wadi nyingine. Mikakati ya kufundishia Stadi ya Kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi ni vigumu kutekelezwa katika madarasa ya chini. Kwa hivyo, uchunguzi huu ulihusisha darasa la nne pekee siyo madarasa mengine kwa sababu mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa kusoma visa virefu na hadithi ndefu afikapo katika darasa hili. Utafiti huu pia ulichunguza Stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi na siyo Stadi nyingine kwa kutumia mikakati mingine.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii kwa jumla imeshughulikia mambo ya kiutangulizi ambayo ndiyo msingi wa utafiti mzima. Mambo haya ni pamoja na usuli wa utafiti unaohusiana na mikakati inayotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Suala la utafiti ambalo linahusu matatizo ya wanafunzi ya kusoma, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, nadharia ya utafiti na upeo na mipaka ya utafiti.

## 1.10 Maelezo ya Istilahi

**Njia**: Ni utaratibu wa kuwasilisha mada kwa wanafunzi katika somo fulani wenye sifa bainifu kama vile vikundi na maswali.

**Ufundishaji**: Ni hali ya kuandaa mazingira, mambo njia, na nyenzo kwa namna ambayo itaathiri tabia za wanafunzi.

**Mbinu**: Katika utafiti huu mbinu limetumiwa kurejelea taratibu za ufundishaji yaani mikakati inayohusisha ruwaza, utendaji na uwasilishaji wa stadi ya kusoma.

**Mikakati**: Ni mpangilio mahsusi na utaratibu wa kutekeleza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa kusoma vitabu vya hadithi.

**Silabasi**: Kiongozi cha somo la Kiswahili ambacho kilitumiwana walimu katika kuandaa ratiba ya kazi ya mwaka mzima kwa darasa la nne katika shule mbalimbali.

**Mtaala**: Mipangilio ya masomo yanayoandaliwa na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala inayotumiwa kuwaelekeza walimu kuhusu kinachostahili kufundishwa katika viwango mbalimbali vya elimu katika taaluma ya Kiswahili.

**Mchakato**: Mfululizo wa shughuli walizofanya walimu katika kufundisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

**Stadi**: Ni ujuzi uliotumika ili kumwezesha mwanafunzi kusoma vitabu vya hadithi kama njia ya kupima ujifunzaji wa stadi ya kusoma.

**Ratiba ya kazi**: Kazi ambayo ilistahili kushughulikiwa katika darasa husika kwa wakati maalum ulioteuliwa kama vile mwaka, muhula, wiki au kipindi cha kufundisha.

**Vitabu vya ziada**: Ni vitabu vilivyoteuliwa na mwalimu vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu kwa kufunza na kujifunza Kiswahili katika Shule.

**Madarasa ya chini**: Darasa la kwanza hadi la tatu katika Shule za Msingi.

**Madarasa ya Juu**: Darasa la nne hadi la nane katika Shule za Msingi.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mikakati ya kufundishia kwa kutumia vitabu vya hadithi katika kuimarisha stadi ya kusoma. Uhakiki wa maandishi umefanywa kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: Stadi ya Kusoma, vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi, nafasi ya vitabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi ya Kusoma, jinsi ya kufunza Stadi ya Kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi, nafasi ya maandalizi ya mwalimu katika kufundisha Stadi ya Kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi, mikakati ya kufundishia Stadi ya Kusoma na majukumu ya mwanafunzi katika kukuza Stadi ya Kusoma.

## 2.2 Stadi ya kusoma

Katika lugha ya Kiswahili, stadi ya kusoma inahusu ujuzi wa mwanafunzi wa kusoma maandishi kwa mtiririko bila kusitasita, kwa sauti inayosikika na matamshi sahihi ya Kiswahili (Miricho na wenzake, 2008). Ufundishaji wa stadi hii unahusu vilevile, kumwezesha mwanafunzi kusoma huku akizingatia alama za uakifishaji, kuelewa akisomacho, kueleweka na wanaomsikiliza, kujenga ukakamavu wa kusoma mbele ya wenzake na kujipatia ujumbe uliyomo kitabuni. Kilicho muhimu pia, ni kumfanya mwanafunzi awe na ari ya kusoma na kumshawishi aweze kutumia muda wake wa mapumziko akijisomea. Ili kutimiza malengo haya, mwalimu anafaa kuwa mjuzi na mmilisi wa mbinu na mikakati faafu itakayomfanya mwanafunzi kujenga stadi hii ambayo itamwezesha kusoma na kupanua elimu yake. Mikakati ya kufundishia stadiya kusoma hutarajiwa kuwasaidia wanafunzi katika ukuzaji wa uwezo wa kusoma na kusoma bila kuelekezwa huenda kusimfaidi mwanafunzi kwa kiwango cha kuridhisha (Halliday,1973).

Utafiti wa Wambui (2011) kuhusu Ufundishaji wa Kusoma kwa sauti katika madarasa ya chini katika Shule za Msingi Tarafa ya Gatanga ulibainisha kuwa kuna uhaba wa nyenzo za kufundishia Stadi ya Kusoma. Hivyo basi Stadi ya Kusoma hufunzwa katika Shule za Msingi ili

kumwezesha mwanafunzi katika mawasiliana ya kila siku na kitaaluma. Lugha ya Kiswahili hutumiwa kama lugha ya kitaifa katika nchi ya Kenya na hufundishwa shuleni na kutahiniwa.

**2.3 Vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi**

Mwalimu ana jukumu la kuwateulia wanafunzi wake vitabu kwa kuzingatia sifa maalum (Musau na Chacha, 2001; Miricho, 2008; Mirikau, 2008; Njogu na Nganje, 2011). Sifa hizi ni kama zifuatazo: Vitabu vinavyoteuliwa viwe vinavyoweza kuwafurahisha na kuwaburudisha wanafunzi, kitabu kizuri kiwe cha kiwango cha wastani cha matumizi ya msamiati unaolingana na uwezo wa wanafunzi kilugha, maneno mengi yasiwe mageni kwani hili huweza kuwachosha wanafunzi. Aidha kusiwe na miundo tata ya kisarufi.

Utafiti wa Ruthiri (2012) umeshughulikia ufaafu wa vitabu vya kusoma kwa madarasa ya tano na sita katika shule za msingi nchini Kenya na Tanzania. Alieleza ya kuwa, vitabu ambavyo huteuliwa kusomwa na wanafunzi wa madarasa hayo havifuati vigezo muhimu vilivyoidhinishwa. Alisema ya kwamba lugha iliyotumiwa katika baadhi ya vitabu vilikuwa na makosa ya kisarufi kama vile kuwa na sentensi ndefu sana. Hili huonyesha kutozingatia sifa zinazofaa katika uteuzi wa vitabu vya hadithi. Maelezo haya yalinufaisha utafiti huu kwa sababu yalishughulikia ufaafu wa vitabu vya kusoma ilhali huu ulichunguza vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi katika shule za msingi darasa la nne vilivyotumiwa kuimarisha stadi ya kusoma.

Kulingana na Wizara ya Elimu (2007), vitabu vinavyoteuliwa kwa minajili ya kutumiwa kufundishia vinafaa kutimiza vigezo mbalimbali vinavyoainishwa jinsi ifuatavyo. Kwanza, mada za kusoma zinafaa kulingana na zile zilizopendekezwa kwenye silabasi. Pili, stadi ya kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika pamoja na kukumbuka, kuchanganua na kujitathmini lazima ziwe kitabuni. Pia, yaliyomo yawe ya kweli, ya kiwango chao, yapangike kimantiki, yashirikishe masuala ibuka kikamilifu na kichanya. Halikadhalika, kitabu hicho kinastahili kuwa cha kiwango cha wanafunzi kilugha mbali na michoro na picha tofautiza kuelimisha,

kueleweka rahisi na kuwahamasisha. Kulingana na Aras (2012) uteuzi wa vitabu vya hadithi vilivyo na picha za kuvutia zinaweza kuwa kichocheo cha kuwavutia wanafunzi kusoma ili kujua kinachoendelea katika kisa husika. Utafiti huu ulichunguza vigezo vifuatavyo: vitabu vyenye kiwango cha wanafunzi kilugha, vitabu vinavyoeleweka kwa urahisi, vitabu vilivyo na michoro na picha na vitabu vyenye kurasa chache.

### 2.3.1 Uteuzi wa Vitabu vya Hadithi

Kwa mujibu wa Musau na Chacha (2001), vitabu au makala yoyote iliyoteuliwa lazima itimize sifa fulani. Miongoni mwa sifa hizi ni mathalani vitabu kuwa vyenye kufurahisha na kuvutia walengwa. Viwatie hamu na ilihamu; viwe vya viwango vyao kimsamiati, kimuundo na kimawasiliano; viwe vya tajriba zao vikirejelea mazingira wanayofahamika kiumri, kimaadili na kitamaduni na visiwe vyenye kurasa nyingi sana za kuwanyongonyeza. Baird (2004) anaeleza kuwa, ni vizuri kugawa machapisho katika maktaba ya shule za msingi kwa kuzingatia umri na ngazi za wanafunzi. Kwa mfano vitabu vya hadithi za watoto, picha za watoto na vitabu kwa ajili ya wanafunzi wanaoanza kujifunza kusoma.

Taasisi ya Elimu ya Kenya huchunguza vitabu vya Kiswahili vilivyochapishwa na kupendekeza vile bora vya kutumiwa shuleni. Kwa hivyo Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (2007) iliidhinisha vitabu vya hadithi na vinginevyo ambavyo vimeteuliwa ili vitumike katika ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wa Shule za msingi na za Upili. Hivyo basi, maktaba ya shule inatarajiwa kuwa na mkusanyiko wa vitabu vya ziada na kiada kwa masomo yote, vitabu vya hadithi na vinginevyo.

## 2.4 Nafasi ya Vitabu vya Hadithi katika Ufunzaji na Ujifunzaji wa Stadi ya Kusoma

Kusoma ni stadi muhimu ambayo mwanafunzi anatarajiwa kuelewa anachosoma hususan mikakati faafu inapotumika kufundishiwa. Kwa kufanya hivyo mwanafunzi anahitajika kuelekezwa ili kutumia muda wake wa mapumziko akijisomea vitabu vya hadithi mwenyewe ili

aweze: kupanua msamiati wake, kupata mafunzo mbalimbali na kustawisha mazoea ya kupenda na kufurahia kusoma (Taylor na wenzake, 1990).

Wataalamu mbalimbali wamedai kuhusu umuhimu wa vitabu vya hadithi. Kwa mujibu wa Tuntufye (1977), mbinu ya kusoma ambayo hutumia usomaji wa vitabu vya hadithi na inayoonekana kuwa inatumia muda mwingi wa kipindi, ndiyo faafu kutumiwa kwa mapana katika ufundishaji wa somo la kusoma katika shule za msingi. Iwapo mbinu hii ingetumika kwa ufasaha na kwa uangalifu katika kusoma vitabu vya hadithi inaweza kuwafaa wanafunzi ili kuimarisha stadi ya kusoma.

Kwa maoni ya Mulokozi (1997), vitabu vya hadithi ni hazina ya maarifa kuhusu fani mbalimbali za maisha. Mtoto anapojua stadi ya kusoma, basi atakuwa ameshika funguo za kufungulia lango la hazina. Kumnyima mtoto stadi hizo ni kumdumaza kiakili na kumnyima haki ya kujua ulimwengu na malimwengu. Maoni haya yana uhusiano na utafiti huu kwa sababu ulishughulikia matumizi ya vitabu vya hadithi kukuza Stadi ya Kusoma ambavyo vina mada tofautitofauti za masuala ibuka kama vile Ufisadi, Dawa za Kulevya na Ndwele.

Kwa mujibu wa Taylor (2002), matumizi ya vitabu vya hadithi kwa kuimarisha lugha ni mbinu ambayo imetumika tangu awali. Vitabu vya hadithi huwasaidia wanafunzi katika lugha. Matumizi yavyo hupanua mawazo na kumfanya mwanafunzi kufurahia usomaji na uandishi wa kila aina kwa vile mtoto hutumia lugha katika muktadha wa mawasiliano na wengine. Walimu wa Kiswahili ni sharti wajenge msukumo wa wanafunzi wao wa kusoma fasihi ya Kiswahili. Fasihi husaidia katika utangamano na ushirikiano wa wanafunzi kupitia usomaji wa vitabu vya hadithi zinazohusu mila, desturi na tamaduni za jamii.

Kwa mujibu wa Ipara (2006), lugha inayotumiwa katika fasihi hufafanua vipengele vya kisarufi, matumizi ya methali, semi, uakifishaji, tahajia na hata mfuatano wa maneno. Kwa hivyo usomaji wa vitabu vya hadithi huwajuza wanafunzi kanuni za lugha na kuimarisha stadi ya

kusoma. Ipara (2006) anasema kwamba lugha inayotumiwa katika vitabu vya hadithi ina uhai na ukwasi. Anaeleza kuwa matumizi ya matini ya fasihi kufundishia kusoma yatafanya wanafunzi kuvutiwa na vipindi vya kusoma ambavyo hapo awali vilionekana kama vikavu na vigumu kwa hivyo kutopendwa. Mtafiti alitumia maoni ya Ipara kubainisha kwamba, matumizi ya vitabu vya hadithi yanaweza kuwasaidia wanafunzi kupata umahiri wa kusoma.

Kwa mujibu wa Collie na Slater (2000) vitabu vya hadithi hukuza lugha kwa wanafunzi hasa wanaovisoma kwa wingi. Mwanzi (1982) naye anaeleza ya kwamba, vitabu vya hadithi hukuza na kuimarisha akili ya mtoto kisaikolojia, kijamii na vilevile kubuni fikira ya uelewa ya dunia wanamoishi. Usomaji wa vitabu vya hadithi hufanya watoto kuelewa zaidi tamaduni za watu wengine katika jamii zao na zile za jamii nyinginezo. Kwa hivyo hujenga uelewa zaidi kwa kuzingatia kuwa watu wengine wana mawazo na hisia kama zao. Watoto wanaposoma vitabu vya hadithi wanapata dira ya kuwaelekeza katika kukabiliana na maisha ya sasa. Katika matini yake, huwamo masuala mbalimbali ya kijamii ambayo wanafunzi hawa hufaa kutanabahishwa kuyahusu ili kujifunza jinsi ya kuyakabili katika maisha halisi. Masuala ya kimsingi kama vile uongo, unafiki, wizi na madhara yake ndiyo hufinyanga maadili na mwongozo wa maisha yanayoafikiana na jamii. Mathalani madhara ya wizi na uongo hujenga msingi wa kuwaelimisha kuhusu ufisadi na madhara yake katika jamii.

Usomaji wa vitabu vya hadithi huwawezesha wanafunzi kuwa na umilisi wa msamiati mwingi ambao huwasaidia kujimudu katika mazungumzo na kujieleza kikamilifu. Kuhusu hali ya fasihi nchini Kenya, Ngugi (2010) anabainisha kuwa mbinu ya usomaji wa hadithi uimarisha ukuzaji wa stadi ya kusoma. Mazoezi ya kimatamshi ya mara kwa mara kupitia usomaji wa vitabu hivi kwa uelekezi wa mwalimu hujenga uzoefu, tajriba na umilisi wa stadi ya kusoma. Kwa ufupi, utafiti unaonyesha kwamba, uzoefu wa kusoma vitabu na makala ya hadithi hujenga ari ya mwanafunzi ya kusoma kwa mapana ili kujipanulia maarifa kielimu, kisarufi, msamiati na matamshi. Inakusudiwa kuwa mwanafunzi ataendeleza kutumia muda wake wa

starehe akisoma na kukuza stadi ya kusoma. Usomaji huu hukuzwa aghalabu kupitia somo linalotumia vitabu vya hadithi (Miricho na wenzake, 2008). Maoni haya ndio uchochezi wa utafiti huu ambao uliweka wazi matumizi ya vitabu vya hadithi ili kuimarisha stadi ya kusoma.

**2.5. Jinsi ya kufunza Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Kitabu vya Hadithi**

Kutokana na umuhimu wa usomaji wa vitabu vya hadithi, Taasisi ya ukuzaji wa Mtaala Nchini (KICD) ilitoa silabasi mpya mwaka wa 2002 ambayo ilihusisha mafunzo ya fasihi na lugha ya Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi la nane. Matumizi ya vitabu hivi yalilenga kumwezesha mwanafunzi kukuza stadi ya kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Kwa hivyo silabasi ya Kiswahili inatilia mkazo wa matumizi ya vitabu vya hadithi ili kuwapa wanafunzi uwezo wa umilisi wa lugha wanayoisoma.

Hata hivyo, silabasi ya 2002 haimwelekezi mwalimu wa Kiswahili kuhusu mbinu na mikakati anayohitaji kutumia na inayofaa katika ufundishaji wa kusoma vitabu vya hadithi. Kutokana na hali hii utafiti huu unafaa kwa vile unatilia maanani ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi na masuala yote muhimu katika elimu na tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

Wataalamu mbalimbali wamebainisha mbinu za jinsi ya kutumia vitabu vya hadithi katika kukuza, kuendeleza na kuimarisha stadi ya kusoma miongoni mwa wanafunzi ili kuelewa na kufasiri yale anayosoma. Kulingana na Ikobwa (2000) mwalimu ndiye anayeteua mbinu mahususi atakazotumia kufundishia somo husika. Uteuzi na matumizi ya mbinu za kufundishia upasavyo pia huchangia umuhimu wa somo na mtaala unaotekeleza uteuzi unaofaa wa mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Kwa mujibu wa Chacha na Musau (2001), mwalimu anafaa kuwahimiza wanafunzi na kujenga ari ya kusoma kwa ziada, wakati wa kujiburudisha au mapumziko. Vipindi vya Kiswahili pekee havitoshi, na hivyo, wakati mrefu unahitajika ili kujenga uzoefu wa kusoma. Mwalimu ahamasishe,

kuwapa mawaidha, mwongozo na motisha ili kujenga ile tabia ya kusoma katika wanafunzi wake. Uzoefu wa kusoma utadumu ukiwa utafanywa kila wakati.

Kwa mujibu wa Njogu na Nganje (2011), Miricho (2008) na Mirikau (2008), somo la stadi ya kusoma kwa matumizi ya vitabu vya hadithi linaweza kufuata hatua zifuatazo: kwanza, kuwaelekeza wanafunzi na kusisitiza njia mwafaka za usomaji na utunzaji bora wa vitabu. Maelezo mafupi yanaweza kutolewa kuhusu vitabu ambavyo vitasomwa. Vifaa vinavyolenga somo la usomaji vinaweza kujadiliwa darasani au shughuli nyingine yoyote ambayo itachangia kuvutia nadhari ya wanafunzi kwenye somo.

Hatua ya pili inahusu mwalimu kuwapa wanafunzi nafasi ya kuchagua vitabu watakavyosoma kisha kuwaelekeza kusoma kimya kimya. Wakati huo, mwalimu anafaa kuwaangalia wakisoma huku akiwasaidia wanaotatizika na kurekebisha kibinafsi wenye tabia dhaifu za usomaji kama vile kusoma kwa kumumunya midomo, au kufuatiliza maandishi kwa kichwa au vidole. Kwa mujibu wa nadharia ya utabia, tabia nzuri katika kujifunza lugha ya pili hujengeka vizuri ikiwa mwanafunzi ataelekezwa vizuri ili kuepukana na makosa. Kutokea kwa makosa ni changamoto kwa sababu makosa haya huenda yakawa tabia. Kwa mujibu wa nadharia hii, makosa yanapaswa kutotuzwa yaani kukatizwa au kuadhibiwa ili yasitokee tena.

Mwalimu anafaa kuweka rekodi ya vitabu vinavyosomwa na kila mwanafunzi ili kujaribu kupima ni kitabu gani kinachowavutia wanafunzi wengi na ni kipi hawapendi. Miricho na wenzake (2008) wanasema kuwa mwalimu anafaa kujaribu kutafuta sababu za kutopenda kwao kwani inawezekana kitabu kimetumia msamiati ulio mgumu kwa mwanafunzi au pengine maudhui hayawahusu wanafunzi moja kwa moja. Ikiwa kitabu hicho ni muhimu, mwalimu awaelekeze kuutambua umuhimu huo na hivyo kutilia kitabu hicho maanani.

Nne, baada ya kusoma, wanafunzi wanafaa kupewa nafasi kuwaeleza wenzao hadithi waliyosoma ili ikaguse hisia zao (Njogu na Nganje, 2011; Miricho, 2008; Mirikau, 2008).

Jambo hili litawapa wanafunzi wengine darasani fununu ya vitabu vya kuvutia ambavyo wangetaka kusoma katika kipindi kijacho. Wataalamu hawa wanasema kuwa wanafunzi wanaposimulia walichokisoma, mwalimu anapata nafasi ya kuwatathmini kupitia uangalizi na kukadiria ufanisi wa somo. Pia mwalimu hupata nafasi ya kuwarekebisha makosa ya kimatamshi, sarufi na mantiki. Wanafunzi hupata nafasi ya kuuliza maswali na kujadiliana na mwalimu na wanafunzi wenzao juu ya yale ambayo yamesomwa au yanayozinduliwa na usomaji huo. Hatua muhimu ni kuwafuatilia na kuwahimiza wanafunzi kuendelea kusoma vitabu hivyo baadaye wakati wa mapumziko au wakiwa nyumbani. Mwalimu anaweza kuwahimiza kuendelea kusoma vitabu na makala mengine tofauti na hayo. Katika utafiti huu, uchunzaji darasani ulionyesha kuwa walimu hawasimamii wanafunzi wakati wa usomaji wa vitabu vya hadithi, wao huwaacha wanafunzi kujisomea wenyewe bila kufuatilia na kuweka rekodi za namna wanavyosoma wakiwa pekee yao. Vilevile huwasomea wanafunzi hadithi huku wakiwasikiliza na hawatengi muda wa kuwapa nafasi ya kusimulia hadithi. Hali hii huwanyima wanafunzi fursa ya kufanya mazoezi ya matamshi.

## 2.6 Maandalizi ya Mwalimu katika Kufundisha Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi

Maandalizi ya mwalimu chuoni na nyanjani ni muhimu sana katika kufanikisha mpango wowote wa elimu. Kuhusu maandalizi chuoni, Egesa (2006) akimnukuu Hopson (1981), anasema kuwa ili shule zikuze stadi bora, zinahitaji walimu ambao wana stadi za hali ya juu. Anaeleza ya kwamba kuna uwezekano wa mwalimu fulani huenda akawa na umilisi wa hali ya juu katika somo analofundisha lakini akakosa uwezo wa kuwasilisha elimu hiyo kwa mwanafunzi kwa sababu ya ukosefu wa mbinu mwafaka za kutekeleza jambo hilo na kuunda mazingira mwafaka ya kujifunza.

Wakati mwalimu anapokuwa na umilisi mdogo kuna uwezekano kwamba mwalimu huyo hakuandaliwa vyema katika masomo yake ya kitaaluma. Kwa mfano, mwalimu anapofunza stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi anapaswa kutumia mikakati mwafaka ili mwanafunzi aweze kutekeleza stadi ya kusoma. Hopson anasikitika kuwa wakati fulani mafunzo ya ualimu hulenga kuzalisha wasomi badala ya walimu, hali ambayo mara nyingi hutayarisha mwalimu ambaye ana upungufu wa stadi zitakazomwezesha kuwa mwalimu bora darasani. Kuna haja ya walimu kuandaliwa vyema katika vyuo vya ualimu na vyuo vikuu ili wawe tayari kukabiliana na changamoto zozote nyanjani.

Shiundu na Mohammed (1996) wanaeleza ya kwamba mageuzi yoyote yanayonuiwa kufanywa katika elimu kuhusu mtazamo, yaliyomo na mbinu za kufundisha yanaweza kutekelezwa tu iwapo mchakato wa mpango wa mafunzo yanayofanywa kabla na baada ya kuhitimu utawaandaa barabara walimu. Isitoshe wanaeleza ya kwamba maandalizi bora ya vifaa na mtaala yakifanywa, walimu nao ni sharti wapewe mafunzo kikamilifu kuhusu mtazamo huo. Kwa hivyo walimu wanahitaji kuandaliwa kozi fupi fupi katika warsha na makongamano kuhusu ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi ili waweze kujimudu kikamilifu.

Sitima (1988) anasisitiza ya kwamba maandalizi ya walimu wanaohudumu ni jambo la busara. Kwa mujibu wa Shiundu na Omulando (1992), kozi za kupiga msasa walimu wanaohudumu husaidia walimu hao kufahamu mabadiliko yanayotokea mara kwa mara katika mtalaa na masomo wanayofundisha. Kupitia kozi hizi mwalimu hupata uwezo wa kukabiliana na mahitaji mapya katikaufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi pamoja na mitazamo mipya na mbinu zinazonuia kuendeleza na kutekeleza mafunzo hayo.

Maandalizi ya mwalimu kabla ya kufundisha darasani ni muhimu sana kwa sababu ndio msingi wa kuwawezesha wanafunzi kuelewa somo akiwa darasani. Maandalizi ya mwalimu ni muhimu hasa inapokumbukwa kwamba anakabiliana na kazi ya ufundishaji yenye changamoto nyingi. Kwa hivyo ni muhimu ualimu kujiandaa vilivyo kabla ya kuingia darasani. Katika

taauluma ya walimu maandalizi kabla ya somo yamekuwa kaida isiyoweza kuepukika kwani ufundishaji haufanywi kiholela. Mwalimu anatakiwa kutayarisha mpangilio wa somo kutokana na maazimio ambayo huwa imetayarishwa kutoka kwa silabasi (Musau na Chacha 2001). Sotto (1994) anasema kuwa, uangalifu na matayarisho kabambe yanahitajika katika kufunza stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi vilivyo. Karani (1996) anasema ya kwamba mwalimu anafaa kufanya matayarisho ya mapema ili kuwasaidia wanafunzi kusoma bila tatizo lolote. Kwa mujibu wa Collie na Slater (1987) maandalizi haya huchangia katika uwasilishaji ambao huwapa wanafunzi mshawasha wa kurudiakusoma vitabu vya hadithi tena na tena. Vile vile maandalizi ya mapema ya somo huhakikisha kuwepo kwa mpangilio mzuri kuanzia mwanzo hadi mwisho wa somo.

Ratiba ya kazi ya Kiswahili ni kifaa muhimu sana kwa mwalimu wa Kiswahili kwa vile humsaidia kupanga kazi yake ya muhula au mwaka mzima. Vilevile humwezesha mwalimu kujua jambo gani atakalolifunza katika kipindi husika na siku. Hivyo basi, ratiba humwezesha mwalimu kukamilisha silabasi ya Kiswahili katika muda ufaao (Njogu na Nganje 2011). Kutokana na ratiba ya somo mwalimu huandaa mambo atakayojishughulisha nayo na yale yatakayoshughulikiwa na wanafunzi darasani katika andalio la somo. Mwalimu huongozwa na ratiba ili kujua somo atakalofunza, nyenzo na jinsi atakavyotathmini somo hilo na malengo ya somo husika. Kwa hivyo utafiti huu ulilenga kutathmini maandalizi ya mwalimu katika ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika Manispaa ya kakamega.

Quist (2000) anaeleza kuwa, maazimio ya kazi humpa mwalimu mwongozo ambao utamwonyesha mada ambazo zimeshughulikiwa katika muhula na zile ambazo zimesalia. Bennaars na wenzake (1994) wanasema ni sharti mwalimu ajue malengo ya elimu na silabasi ili atayarishe maazimio ya kazi na mpangilio wa somo. Kulingana na Igaga (1993) mpangilio wa somo humsaidia mwalimu kuwasilisha somo kimantiki bila kuchanganya mambo. Vilevile,

mwalimu hawezi kusahau dhana fulani, atakumbuka aina za nyenzo za kufundishia na atakuwa na ukadiriaji bora wa muda anapofundisha hatua kwa hatua.

Tajriba ya mwalimu pia humwezesha mwalimu katika ujifunzaji na ufundishaji wake kwa sababu ya kuwa na umilisi katika stadi husika. Katz (1989) anasisitiza kwamba umilisi wa mwalimu ni kipengele muhimu cha kuamua ubora na kuleta matokeo yanayotarajiwa ya mpango wowote. Umilisi huu unatokana na ufahamu wa mbinu za kufundishia pamoja na mada mbalimbali za kufundisha stadi ya kusoma.

**2.7 Mikakati ya kufundishia Stadi ya Kusoma**

Mikakati ni mipangilio mahsusi na utaratibu wa tajriba za ufundishaji. Mwalimu hutafuta njia mwafaka ambazo hufuata ili kupanga, kutekeleza na kupata matokeo yanayohitajika kutoka kwa mwanafunzi wake. Haya ni mambo yote yanayotekelezwa na mwalimu na mwanafunzi kabla ya kuingia darasani na hufanywa hatua kwa hatua ili kufaulisha shabaha zilizobuniwa na mwalimu (Wanjala na Kavoi 2013).

Mikakati ya kufundishia ni njia na mbinu za kufundishia zinazotumika katika shughuli za kielimu kwa madhumuni ya kusaidia katika kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Mbuthia (1996) anaeleza ya kwamba mikakati ya kufundishia ni vigeu muhimu katika ufundishaji wenye kuleta matokeo mazuri. Mikakati hii inaweza kuainishwa katika makundi mawili makuu yaani, inayowashirikisha wanafunzi katika somo na ile inayompa mwalimu uwezo wa kutekeleza somo (Harvey na Bizar, 1998).

Kwa mujibu wa Simiyu (2001), mwalimu anafaa kuteua mikakati ya kufundishia kwa uzingativu ili kulifanikisha somo. Uteuzi wake huzingatia mada, aina ya wanafunzi na uwezo wao wa kuelewa somo husika. Mwalimu aliye na uwezo wa kitajriba ana nafasi kubwa ya kutumia stadi mbalimbali katika kuliwasilisha somo la kusoma linalohusu usomaji wa vitabu vya hadithi.

Mikakati ambayo imekuwa ikitumika tangu awali ni ile ambayo haimhusishi mwanafunzi katika usomaji unaozingatia tajriba yake (Mirikau, 2008). Mwalimu huchukua nafasi ya kuwa mwelekezi bila kujali maendeleo ya mwanafunzi katika kukuza stadi hii. Mara nyingi wamekuwa wakitumia maandishi ubaoni na vitabu vya kiada ambavyo aghalabu huwachosha wanafunzi. Hii inatokana na kutobadilisha vichocheo vya hisia. Uhusishaji wa picha na michoro ubaoni na kwenye chati pia ni mikakati iliyozoeleka ambayo haileti uchangamfu darasani. Wanafunzi wanahitaji kupewa makala na taarifa ambazo huweza kusisimua milango yote ya hisia. Makala na taarifa hizi kwa mujibu wa Miricho na wenzake (2008), hupatikana kwenye magazeti, majarida na vitabu vya hadithi.

Katika ufundishaji wa stadi ya kusoma, mwalimu anafaa kuwasomea kisehemu huku wakisikiliza na kufuatiliza ili baadaye waige usomaji huo (Ellis, 2006). Ellis anasema kuwa usomaji wa aina hii hufaidi ikiwa kila mtoto anaweza kuketi mahali anapoweza kusoma makala yanayosomwa (kwa kufuatiliza). Kwa hivyo, darasa lapaswa kuwa na matini za kusoma za kutosha au ziwe zimeandikwa ubaoni au kwenye mabango.

Wanafunzi wanaweza kuhusishwa kusoma wote pamoja kwa sauti, kisha wakasoma mistari, madawati, wawili wawili huku mwalimu akisikiliza na mwishowe mmoja mmoja. Kwa mujibu wa Watson na wenzake (2012), mazoezi haya mengi humzoeza mwanafunzi asiye na ukakamavu wa kutamka neno au sentensi kuzoea kutamka. Wanazidi kusema kuwa, mwalimu anaweza kuwaweka wanafunzi katika makundi akawahusisha kusoma huku wengine wakisikiliza na kuwakosoa. Mtindo huu husaidia kuwahusisha wanafunzi wote kwenye somo na hujenga moyo wa ushirikiano. Vilevile husaidia ujifunzaji ambapo mwanafunzi huona afadhali kukosolewa na wachache kundini kuliko kukosolewa na mwalimu mbele ya darasa zima. Huu pia ni usomaji ambao baadaye wanafunzi wanaweza kuendeleza hata bila usimamizi wa mwalimu.

Kulingana na maoni ya wataalamu hawa, ufundishaji wa stadi ya kusoma hufanyika vyema iwapo unahusisha usomaji wa makala kutoka vyanzo mbalimbali kama vile magazeti na

majarida, vikato vya magazeti na majarida na hata vitabu vya hadithi bila kutegemea tu vya kiada. Ngugi (2016) anabainisha tabia ya usomaji wa vitabu vya hadithi na magazeti miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi. Anaeleza kuwa, katika gazeti la '*Daily Nation', 'Sunday Nation' na 'Taifa Leo'* kuna sehemu inayojulikana kama "Children's corner". Sehemu hii imetengewa hadithi ambazo zimechapishwa katika kitabu na kila siku mtoto anapewa nafasi ya kuisoma hadithi hiyo. Lengo ni kujenga ilhamu ya mtoto na kumtaka asome hadithi hiyo siku inayofuata. Mbinu hii ni muhimu kwa wale wanafunzi ambao hawawezi kusoma kitabu wakakimaliza. Wanapohitimisha sehemu ya hadithi wanajiona kuwa wamekamilisha kazi kubwa. Wanafunzi kama hawa watakuwa wanaanza kujenga mazoea ya kusoma maishani mwao. Maoni haya yana mchango mkubwa katika utafiti uliofanywa ambao ulichunguza mikakati za kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

### 2.7.1 Mazingira ya Kusoma ya Nje ya Shule

Ili kukuza mtoto aliyeelimika na mmilisi wa stadi zote za Lugha kuna haja ya kubuni mazingira bora ya kumwezesha upataji wa elimu na stadi hizi. Misingi asili ya mazingira ya elimu ni kama vile nyenzo za masomo na shughuli mbalimbali, mazingira ya nje na mazingira ya jumuia na utamaduni. Uhusiano wa mambo haya yote hutoa mazingira mwafaka ya elimu yanayosisimua mwanafunzi (UNESCO, 2011).

### 2.7.2. Mazingira ya Shule za Msingi

Mazingira ya nje ni kichocheo cha kujua kusoma na kuandika. Huwa na athari kwa maendeleo na kutenda kazi kwa wanafunzi. Mazingira yanayovutia na yaliyopangwa vizuri huwatia wanafunzi moyo wa kutagusana miongoni mwao wenyewe na auhuwawezesha kufanya kazi yao kibinafsi au katika vikundi vidogo. Aidha kuzidisha uwezo wao wa kujua kusoma na kuandika na hukuza tabia na mienendo mizuri ya kusoma. Kulingana na UNESCO (2011), kuwepo kwa nyenzo kama vile vifaa halisi kwa mfano vitabu vya hadithi na chati za kufundishia

kusoma na kuandika na jinsi zilivyopangwa mahali na kuvutia na kuzidisha upataji wa ujuzi wa kusoma kwa wanafunzi.

Maktaba ya Shule ni aina nyingine ya nyenzo ambayo ina mazingira mazuri yanayomwezesha mwanafunzi kusoma vitabu vya hadithi kibinafsi kwa sababu ya utulivu wa kutosha. Kwa mujibu wa Omar (2013) huduma nzuri za maktaba zinategemeana na mazingira, vifaa vilivyomo na mtoaji wa huduma ya maktaba. Anaeleza kuwa mwalimu anahitajika kumkuza na kumwelekeza mwanafunzi kwa matumizi mazuri ya maktaba.

Kutokana na maelezo haya matumizi ya nyenzo yalimwezesha mwanafunzi kuyadhibiti mazingira yake katika masomo yake. Mwanafunzi anapoambiwa jambo bila kushirikisha nyenzo huweza kusahau, anapofunzwa hukumbuka na anaposhirikishwa huelewa (Musau na Chacha 2001). Kauli hii ndiyo ilikuwa chanzo cha utafiti huu uliokusudia kuchunguza mazingira ambamo wanafunzi hujifunzia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

Mazingira yanayoafiki elimu yanapaswa kuwa ya kusisimua. Mazingira haya ni kama vile shuleni, nyumbani, darasani, kazini na jumuia ambayo ni muhimu kwa upokezi wa elimu, maendeleo na matumizi ya milele (UWEZO, 2011). Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza ikiwa wanafunzi hupata mazingira yanayowawezesha kusoma vitabu vya hadithi wakiwa mahali mbalimbali kama vile shuleni na nyumbani.

### 2.8 Majukumu ya Mwanafunzi katika Kukuza Stadi ya Kusoma

Bishop (1995) anatambua mielekeo ya walimu na wanafunzi kuwa ya muhimu katika uamuzi wa muundo au mtaala. Mwanafunzi huweza tu kujifunza ikiwa yuko tayari kusoma yaani bila kushurutishwa na anapolazimishwa au kukatazwa, ataudhika (Hargenhann na Oslon 1997). Mwalimu anapoandaa somo la kusoma yafaa atilie maanani uwezo wa mwanafunzi wake, mikakati na nyenzo za kufunzia.

Hali za ukuaji na utambuzi wa wanafunzi katika uwezo wao huchangia katika viwango vya kujihusisha kwao masomoni kadri wanavyokua, huwa hawathubutu kutenda vitendo wasivyoelewa kuwa havileti ufanisi. Kulingana na Lumsden (1994), watoto wachanga huwa na matumaini makubwa ya ufanisi hata wanapoambulia patupu mara kwa mara, ikilinganishwa na wale wenye umri mkubwa. Wanafunzi wenye umri mkubwa, wanaposhindwa kusoma baada ya kutia bidii nyingi, huwaza kuhusu uwezo wao, ikilinganishwa na wanaposhindwa hata baada ya wao kutia bidii finyu. Kusoma kwa mapana humwezesha mwanafunzi kupanua elimu yake kuhusu taaluma mbalimbali na pia uelewa wake wa tamaduni, watu na mahali mbalimbali. Kusoma vitabu na taarifa mbalimabali hukuza lugha ya mwanafunzi na kumwezesha kujieleza katika lugha hiyo (Musau na Chacha 2001).

Usomaji wa vitabu vya hadithi huhitaji muda mrefu. Kwa hivyo walimu wanapasa kuwapa wanafunzi vitabu vya hadithi ili wakavisome wakati wao wenyewe. Kipindi cha kusoma kwa ziada kitumiwe na watengewe muda wa kukamilisha kusoma vitabu walivyo navyo. Mwalimu atunge maswali ya kijumla ambayo atatumia kuhakikisha kuwa wanafunzi kweli wamesoma vitabu walivyopewa. Wanafunzi pia wanahitaji kuongozwa na walimu ili wanaposoma vitabu vya hadithi nyumbani wasaidiwe na wazazi na watu wa jamii zao. Flavia (2011) alichunguza utamaduni wa kusoma vitabu vya hadithi miongoni mwa wanafunzi na wazazi wao nchini Kenya na Tanzania. Utafiti wake ulionyesha kuwa, wanafunzi na wazazi wao hawakuwa wamemakinika katika usomaji wa vitabu vya hadithi. Hali hii ndio ulikuwa mshawasha wa utafiti huu ili kutathmini uwepo wa wakati wa kuwawezesha wanafunzi kusoma na ikiwa wao hupata usaidizi wa watu mbalimbali.

## 2.9 Tafiti za hivi karibuni

Stadi ya kusoma imekuwa ikifundishwa kwa matumizi ya nyenzo zisizo za kifasihi kama vile chati, kadi za maneno, mbinu ambazo hazichochei ilhamu ya mwanafunzi. Kwa mujibu wa

Ahmadi na Aziz (2009), wanafunzi wengi hawaimudu lugha kwa sababu ya mikakati inayotumiwa katika ufundishaji.

Wasike (2007) alichunguza mikakati ya ufundishaji wa fasihi simulizi katika shule za upili wilayani Bungoma na anadai ya kwamba utafiti wake haukushughulikia vipengele vyote muhimu kuhusu ufundisahaji wa fasihi simulizi. Alipendekeza kuwa utafiti kuhusu mikakati ya kufundishia fasihi simulizi katika shule za msingi hufanywe ili kuweka misingi madhubuti katika ufundishaji wa Kiswahili kama somo. Kwa hivyo, utafiti huu ulishughulikia mikakati inayotumiwa na walimu katika kufundisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika shule za msingi ili kuziba mwanya huo. Lakini utafiti huu haukufanywa kwenye kaunti ya Bungoma.

Mukundi (2009) alifanya utafiti ulioshughulikia mikakati ya ufundishaji katika shule za upili wilayani Uasin Gishu kwa kuchunguza jinsi uteuzi wa njia za kufundishia ulivyoathiri ufundishaji wa insha. Utafiti huo ulibainisha kuwa tatizo lilikuwa uteuzi wa njia za kufundishia insha. Matokeo hayo ya Mukundi yalikuwa chanzo cha utafiti huu ili kuchunguza walimu wa Kiswahili wanavyoteua vitabu na njia za kufundishia stadi ya kusoma. Natwart (2009) alifanya utafiti kuhusu uchunguzi wa mbinu za kufundishia hadithi fupi katika shule za sekondari wilayani Kakamega ilhali utafiti huu ulishughulikia uchunguzi wa mikakati inayotumiwa na walimu katika usomaji wa vitabu vya hadithi kama mbinu ya kufundishia stadi ya kusoma katika shule za msingi. Matokeo ya Natwart yalitambua kuwa, walimu hawatumii mbinu faafu katika kufundisha hadithi fupi. Uhusiano uliopo kati ya utafiti wa Natwart na huu ni kwamba alichunguza mikakati ya kufundishia hadithi. Ilhali utafiti huu umetofautiana na utafiti huo kwa vile ulishughulikia shule za sekondari na utafiti huu umeshughulikia shule za msingi za Manispaa ya Kakamega. Isitoshe, aliangalia mikakati ya ufundishaji wa hadithi fupi ilhali utafiti huu umechunguza mikakati ya ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

Ngugi (2009), ametafiti kuhusu hali ya fasihi ya watoto nchini Kenya. Ameshughulikia fasihi ya watoto hao katika usomaji kwa kuzingatia sababu zilizowafanya wanafunzi wasipende kusoma fasihi. Kazi yake imetofautiana na utafiti uliofanywa kwa sababu huu umeshughulikia uchunguzi wa mikakati inayotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika darasa la nne, maandalizi ya mwalimu, uteuzi wa vitabu vya hadithi na majukumu ya mwanafunzi katika kukuza stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

Iyaya (2010) alichunguza mambo yanayoathiri ufundishaji wa ushairi katika shule za upili tarafa ya Dagoreti. Utafiti huu unaafikiana na wa Iyaya ulipobainisha kuwa tabia na mienendo ya wanafunzi iliathiri uelewaji wao katika usomaji wa ushairi. Uchochezi ulitokana na hali hii ili kuchunguza majukumu ya mwanafunzi katika kukuza stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi ingawa utafiti wake ulijikita katika usomaji wa ushairi. Utafiti wa Iyaya uliongozwa na nadharia ya utabia iliyoasisiwa na Skinner (1957). Nadharia hii imetumiwa katika utafiti huu kwa sababu ulilenga kuchunguza tabia ya mwanafunzi ili kuimarisha usomaji wa vitabu vya hadithi.

Romanors (2015) alishughulikia mikakati ya kufundishia vitendawili vya Kiswahili katika darasa la tatu katika kaunti ndogo ya Nambale. Matokeo ya utafiti uliofanywa ulibainisha ya kwamba walimu hupendelea kutumia njia ya mhadhara kwa vile huwawezesha kukamilisha silabasi ili wawe na muda wa kutosha wa kudurusu. Njia mwafaka zinazofanikisha vyema ufundishaji wa vitendawili vya Kiswahili zinazomshirikisha mwanafunzi kama vile maigizo, kazi mradi, maonyesho, drama na vikundi zimepuuzwa.

Utafiti huo unahusiana na huu kwa vile umeshughulikia mikakati ya kufundishia inayolenga maandalizi ya walimu, njia za kufundishia na nyenzo za kufundishia. Utafiti huo ulishughulikia mikakati ya kufundishia vitendawili ilihali huu umechunguza mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi, katika darasa la nne na eneo la kaunti ndogo ya Kakamega.

Wanyonyi (2015) alichunguza mikakati ya kusikiliza kama njia ya ufunzaji wa Kiswahili katika shule ya upili katika Kaunti Ndogo za Nandi kaskazini. Matokeo ya utafiti wa Wanyonyi yalitambua ya kwamba walimu walifahamu umuhimu wa mikakati ya stadi ya kusikiliza katika ufundishaji na ujifunzaji lakini hawaitumii kimakusudi darasani. Uhusiano uliopo kati ya utafiti huu na utafiti wa Wanyonyi ni uchunguzi wa mikakati inayotumiwa kufundishia stadi. Hata hivyo, unatofautiana na utafiti huu kwa vile ulishughulikia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika Shule za Msingi za Kaunti Ndogo ya Kakamega ya Kati, nao ulijikita katika stadi ya kusikiliza katika Shule za Upili Kaunti Ndogo ya Nandi Kaskazini. Kwa ujumla, tafiti tulizozipitia hazikulenga uchunguzi wa mikakati inayotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika Shule za Msingi. Kwa misingi hii, imebainika kuwa tafiti hizo zilizingatia ufundishaji wa stadi za kusikiliza, kuongea na kuandika. Utafiti huu umenuia kutathmini mikakati ambayo walimu hutumia ili kuimarisha stadi hii na kuwasaidia kuchuja mikakati ya ufundishaji wao darasani. Hii ni kwa sababu fasihi ni chombo muhimu sana cha kuboresha usomaji kwa kuwa huathiri sarufi, insha na ufahamu ambavyo hutahiniwa katika mtihani wa KCPE.

Baadhi ya tafiti za awali zimeshughulikia uchunguzi wa mikakati ya ufundishaji wa fasihi simulizi katika shule za upili ambapo utafiti huo haukuhusisha vipengele vyote muhimu vya fasihi simulizi. Vilevile zilishughulikia mikakati ya ufundishaji katika shule za upili kwa kuchunguza jinsi uteuzi wa njia za kufundishia ulivyoathiri ufundishaji wa insha. Aidha utafiti ulifanywa wa kuchunguza mbinu za kufundishia hadithi fupi katika shule za sekondari ilhali kipengele cha mikakati ya ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika shule za msingi za Manispaa ya Kakamega hakikushughulikiwa. Kutokana na uhakiki wa maandishi, hakuna yale ambayo yamelenga ufundishaji wa Stadi ya Kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kusoma wa wanafunzi wa Shule za Msingi.

## 2.10 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia uhakiki wa maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti. Mambo haya ni kama vile vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi, maandalizi ya walimu darasani, matumizi ya vitabu vya hadithi, mikakati ya ufundishaji wa stadi ya kusoma, majukumu ya mwanafunzi katika ukuzaji wa stadi ya kusoma. Huu ni uhakiki wa maandishi yanayohusu suala la utafiti.

# SURA YA TATU

# MUUNDO NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mbinu za utafiti, eneo la utafiti, njia za utafiti, uteuzi wa sampuli, mbinu za uteuzi wa sampuli, idadi lengwa na sampuli teule. Vilevile ulishughulikia, vifaa vya kukusanya data, uthabitiwa vifaa, uaminifu wa vifaa, majaribio ya vifaa vya kukusanya data, utaratibu wa kukusanya data, njia za uchanganuzi wa data na matatizo nyanjani.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo wa usoroveya ambao ulitumiwa ili kupata data ya kuainisha mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Gay (1981) anafafanua utafiti wa aina hii kama mchakato wa kukusanya data ili kujibu maswali ya utafiti yanayolenga kuakisi hali ya sasa ya watafitiwa. Katika mchango wao, Cohen na Manion (1980) wanaeleza kwamba lengo la utafiti wa kimaelezo wa usoroveya ni kukusanya data katika wakati maalum na kuitumia kueleza jinsi hali ya mambo yalivyo kwa wakati huo.

Mtafiti alichagua muundo huu kwa vile alitaka kueleza vile hali ya ufundishaji wa stadi ya kusoma ilivyokuwa wakati wa utafiti katika Shule za Msingi za Manispaa ya Kakamega. Matumizi ya uchunguzi wa kimaelezo yalikuwa mwafaka katika utafiti huu. Kama asemavyo Kerlinger (1978), mbinu hii inapotumika hutoa maelezo mengi ya kutegemewa. Msingi na ufahamu wa utafiti wa muundo huu ulimpa msukumo wa kutumia. Utafiti huu ulifanywa kwa lengo la kukusanya habari, maoni, misimamo, na mapendekezo kutoka kwa walimu wa Kiswahili kuhusu mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa matumizi ya vitabu vya hadithi. Ni matumaini ya mtafiti kuwa utafiti huu utatia ari kwa watafiti wengine kuutalii uwanja wa stadi ya kusoma ili kuufanyia uchunguzi zaidi utakaotatua baadhi ya matatizo yanayohusiana na stadi hii na hasa mikakati ya kuifundishia.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika shule za msingi za Manispaa ya Kakamega ya Kaunti Ndogo ya Kakamega ya Kati, Kaunti ya Kakamega. Manispaa ya Kakamega inajumlisha wadi ya Sichirayi upande wa Kaskazini, Mahiakalo upande wa magharibi na Shieywe upande wa mashariki.Kulingana na mipaka ya kielimu, Manispaa ya Kakamega hupatikana katika Kaunti ndogo ya Kati ya Kakamega ya Kaunti ya Kakamega. Eneo hili lina shule 39 za msingi, shule 25 ni za umma na 14 ni za kibinafsi. Orodha ya shule hizi ilipatikana katika Ofisi ya Elimu ya kaunti ndogo ya Kakamega ya Kati (tazama Kiambatisho 3).

Mtafiti alichagua sehemu hii kwa sababu amefundisha baadhi ya shule hizi na aligundua kuwa kumekuwa na baadhi ya wanafunzi ambao hawawezi kusoma kwa ufasaha hata wafikapo darasa la nne. Tuckman (1978) anasema kuwa, uzoefu wa eneo la utafiti humpa mtafiti kibali miongoni mwa wakazi wa eneo husika. Singleton (1993) naye anatilia mkazo maoni haya anaposisitiza kuwa, eneo linalofaa kwa utafiti ni lile la kufikiwa kwa urahisi na lililokubali mtagusano baina ya mtafiti na watafitiwa. Vile vile anaeleza kuwa eneo asilokaribishwa mtafiti ni dhahiri kuwa hawezi kufanikiwa katika utafiti wake. Mtafiti akiwa mwalimu katika eneo hili la utafiti alipendelea kaunti ndogo ya Kakamega ya kati kutokana na hali kwambaalielewa vyema eneo la utafiti. Vilevile eneo hili lilichaguliwa kwa sababu utafiti wa Shirika la Uwezo Kenya (2010) ulithibitisha kuwa baadhi ya wanafunzi wa eneo hili walikuwa na tatizo la kusoma hata wale ambao wamefika madarasa ya juu (tazama 1.1).

Idadi ya wahojiwa 216 ambamo sampuli iliteuliwa ilikuwa kubwa na yenye sifa tofauti tofauti. Hivyo basi ilichukuliwa kuwa sampuli katika eneo zima ingewezesha vigeu vyote vilivyoainishwa kuchunguzwa katika utafiti huu. Pia eneo hili lilitumiwa kwa vile tafiti za maktaba zilidhihirisha kuwa hakuna utafiti wowote mwingine unaojulikana ambao ulikuwa umefanywa kuhusu mikakati ya ufundishaji wa stadi ya kusoma katika eneo hili. Ni kutokana na hali hiyo ndipo utafiti huu ulitaka kuchunguza mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma

kwa kutumia vitabu vya hadithi kwa kusudi la kuona jinsi stadi ya kusoma hufunzwa. Eneo la utafiti limeonyesha pale ambapo Manispaa ya Kakamega ipo katika ramani ya Kaunti Ndogo ya Kakamega ya Kati (tazama kiambatisho 9).

### 3.4 Idadi Lengwa

Manispaa ya Kakamega ina shule 39 za msingi zenye sifa zifuatazo: za umma (UM) na za kibinafsi (KB) (rejelea kiambatisho 3). Utafiti ulihusisha walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za umma na shule za kibinafsi. Darasa la nne ndilo lililolengwa kutafitiwa. Darasa la nne lilichaguliwa kwa sababu wanafunzi wake wanahitajika kuwa wameimarika katika kusoma maneno ya lugha ya Kiswahili. Vilevile wanafunzi hao wamekuwa wakifunzwa stadi ya kusoma tangu walipokuwa darasa la kwanza.

Vilevile, wanaweza kuchukuliwa kuwa wana ujuzi zaidi wakusoma vitabu vya hadithi na hivyo, wanatarajiwa kuwa wana uwezo wa kusoma vitabu vya hadithi kwa ufasaha. Utafiti huu haukuzingatia madarasa ya chini kwa sababu wengi wao hawana ujuzi wa kusoma vitabu vya hadithi. Wanafunzi wa madarasa ya juu nao walitarajiwa kuwa na ujuzi zaidi ya wale wa darasa la nne. Hivyo basi mtafiti alitazamia kugundua mapema chanzo cha kutoweza kusoma ili kuthibiti hali hiyo. Utafiti ulilenga sampuli ya walimu wanaofundisha Kiswahili darasa la nne katika shule hizo za msingi za Manispaa ya Kakamega. Walimu hao walikuwa wa muhimu katika utafiti huu kwa sababu wao hutumia mikakati tofauti tofauti katika kuendeleza mafunzo ya kuimarisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

### 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Katika utafiti huu, sampuli iliteuliwa kwa kutumia mbinu za utabakishaji, kimakusudi na kinasibu. Kwa mujibu wa Kothari (2012) uteuzi wa sampuli ndio unaotupa idadi kamili ya watafitiwa. Anaeleza ya kwamba ni vigumu sana kuchunguza idadi nzima ya watafitiwa kwa sababu ya wakati na gharama. Hivyo basi, kutokana na maoni ya Kothari ni vyema kutumia sampuli teule.

### 3.5.1 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Ili kupata sampuli wakilishi ya utafiti, mtafiti aliweka shule katika matabaka mawili tofauti: UM na KB. Sababu ya kufanya hivi ni kuwa kila aina ya shule huwa na mazingira yake bainifu na tofauti ambayo huathiri ufundishaji na ujifunzaji. Yuko na Onen (2005) wanaeleza kuwa, utabakishaji unahakikisha kuwa vikundi vidogo vya watafitiwa vilivyo na sifa sawa vinawakilishwa katika utafiti. Utabakishaji pia husaidia kuelezea tofauti za kisifa zinazopatikana kati ya matabaka haya. Matabaka yalitumiwa kwa sababu idadi ya vitabu vya hadithi na matumizi katika shule za umma na za kibinafsi ni tofauti. Pia, utabakishaji ulitumiwa ili kupata sampuli yenye uwakilishi tosha na yenye kutupatia data inayoweza kutegemewa na matokeo ya kuaminika na kuthibitika (Kilemi na Wamahiu, 1995; Kerlinger, 2004; Kothari, 2012).

Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999) ni vigumu sana kuchunguza idadi nzima ya watu inavyotakiwa kwa sababu ya wakati na gharama na hivyo watafiti huchagua na kuzingatia idadi fulani ambayo huitwa sampuli. Tuckman (1988) anasema kwamba sampuli ya asilimia 30 ya wahojiwa ni wakilishi na ya kutosha kukusanya data ya kutegemewa na isiyo na upendeleo wowote mradi imeteuliwa kwa misingi ya sifa bainifu za sampuli.

Shule ziliteuliwa kwa misingi ya matabaka mawili kama ifuatavyo: UM -8 (asilimia 30 ya shule 25) na KB -4 (asilimia 30 ya shule 14). Jumla ni shule 12 ambazo ni asilimia 30 ya shule zote za msingi 39) katika Manispaa ya Kakamega (rejelea Kiambatisho 3). Baada ya kupewa orodha ya shule zote katika Manispaa ya Kakamega, mtafiti aliziorodhesha na kuzipa herufi na kisha kuandika herufi hizo kwenye vijikaratasi, halafu akavitia hivyo vijikaratasi katika makasha mawili ili kuteua UM na KB. Makasha haya yalitikiswa na mtafiti akateua kinasibu vijikaratasi vinane na vinne mtawalia katika haya makasha mawili ili kupata shule nane za umma na nne za kibinafsi zilizohusishwa katika utafiti.

Kwa upande mwingine, mbinu ya uteuzi wa kinasibu ilitumika pia kuchagua sampuli wakilishi ya walimu 65 ambao walishiriki katika utafiti huu. Hii ni asilimia 30 ya walimu 216 wa Kiswahili katika manispaa ya Kakamega. Haingewezekana kuhusisha walimu wote 216 kwa sababu ya ukubwa wa idadi. Mtafiti alitumia walimu wote wa shule teuliwa 12 wanaofundisha darasa la nne. Uteuzi huu ulifanywa kimakusudi ili mtafiti aweze kupata mtazamo wa kila mwalimu aliyefundisha hii stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

### 3.5.2 Sampuli Teule

Sampuli ya kutumiwa katika utafiti huu iliwahusisha walimu kumi na wawili wanaofunza Kiswahili katika darasa la nne. Walimu wanane walitoka katika shule za msingi za umma na wanne katika shule za kibinafsi ambao walitazamwa darasani wakifundisha ambayo ilikuwa asilimia thelathini (30%) ya shule za msingi katika kila kategoria ya shule hizo zipatikanazo katika Manispaa ya Kakamega. Walimu 65 kupitia kwa sampuli teuliwa na wanaofundisha darasa la nne walipewa hojaji wajaze.

Mtafiti aliwatumia walimu wanaofundisha somo la Kiswahili kutoka katika Shule 12 za Msingi za umma na kibinafsi katika eneo hili (Rekodi katika Afisi ya Elimu, Kaunti Ndogo Kakamega ya Kati, 2016). Orodha ya majina ya shule zilizotumika ilipatikana katika kiambatisho 3. Ripoti ambazo walimu wakuu huwasilisha katika Afisi ya Elimu kila mwisho wa mwezi zilionyesha kwamba katika hizo shule 39, kulikuwa na walimu 216 wa Kiswahili waliohitimu.

**Jedwali 3.1 Sampuli teule**

| Sampuli | Idadi ya jumla | idadi teule | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Shule | 39 | 12 | 30% |
| Walimu wa Kiswahili | 65 | 216 | 30% |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alitumia mbinu zifuatazo kukusanya data: Hojaji na uchunzaji.

#### 3.6.1 Njia za Ukusanyaji wa Data

Ili kuweza kuchunguza mikakati inayotumiwa katika kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi, utafiti huu ulizingatia utafiti wa maktabani na nyanjani. Utafiti wa maktabani ulifanywa kwa kuchunguza maandishi mbalimbali kuhusu stadi ya kusoma na mikakati ya kuifundishia shuleni. Uchunguzi huu ulimpa mtafiti msingi bora wa kueleza na kupendekeza njia mwafaka ya kutumia vitabu vya hadithi katika ufundishaji wa stadi ya kusoma. Uchunguzi wa maandishi ulisaidia kueleza maoni na mitazamo ya wataalamu mbalimbali kuhusu mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma katika Kiswahili.

Utafiti huu ulifanywa nyanjani katika shule 12 za msingi katika Manispaa ya mji wa Kakamega. Mbinu ya hojaji na uchunzaji zilitumiwa kukusanya data kuhusu mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Maswali ya hojaji kilikuwa kifaa muhimu kwa ukusanyaji wa habari ambayo haiwezi kupatikana kwa kutazama tu au kwa mahojiano. Kutumia hojaji husaidia kupata hisia za watu, mielekeo yao na tajriba ya mtu binafsi (Gall, Borg na Gall, 1996).

Mbinu ya uchunzaji pia ilitumiwa kukusanya data katika utafiti huu. Gathumbi (1995) anasema kuwa, uchunzaji ni mbinu mojawapo mwafaka zaidi kutumia kuchunguza uhusiano kati ya mwalimu na wanafunzi katika ufunzaji na ujifunzaji. Tafiti zingine zimedhihirisha kuwa utazamaji ni muhimu sana kwani ndiyo njia ya pekee isiyo na ubaguzi katika kupima utendaji kazi wa mwalimu na tabia ya wanafunzi darasani (Brumfit na Johnson 1985). Uchunguzi wa mikakati inayotumiwa kufundisha stadi ya kusoma katika Kiswahili ulifanywa kwa kukusanya data kutoka kwa walimu kupitia kwa vifaa viwili: maswali ya hojaji na mwongozo wa uchunzaji.

### 3.6.2 Vifaa vya Ukusanyaji wa Data

Ili matokeo ya utafiti wowote yapatikane na yawe na uthabiti, mtafiti hana budi kushirikisha vifaa mbalimbali (Peil, 2002). Peil anaeleza kwamba matumizi ya vifaa zaidi ya kimoja huweza kuziba pengo lililoachwa na kingine hasa ikiwa kimetumiwa kuibua data sawa. Matumizi ya vifaa vya kukusanya data anuwai huimarisha uaminifu na uthabiti wa data. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia vifaa vifuatavyo: maswali ya hojaji na mwongozo wa uchunzaji. Vifaa hivi vimejadiliwa hapa chini kimoja baada ya kingine. Vifaa hivi viliandaliwa kulingana na madhumuni ya utafiti ambayo yalinuia kuchunguza mikakati inayotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika Shule za Msingi, Kaunti Ndogo ya Kakamega ya Kati.

#### 3.6.2.1 Maswali ya Hojaji

Mtafiti alitumia hojaji kati ya vifaa vingine kukusanya data. Hojaji ilijitokeza kuwa ya muhimu katika utafiti huu kwa sababu ilikuwa mwafaka sana na mbinu nyepesi isiyo na gharama kubwa kutafuta data kutoka kwa watafitiwa wengi na kwa muda mfupi (Kothari, 2012). Hojaji iliyotumiwa ilikuwa na maswali funge na wazi kama inavyopendekezwa na Wamitila (2004). Sehemu funge ilikuwa na maswali na majibu ambapo mhojiwa alihitajika kuteua majibu kisha kulikuwa na maswali wazi ambayo yalihitaji maoni, maelezo na mitazamo ya wasailiwa. Mtafiti alikubaliana na mawazo haya na aliyazingatia katika maandalizi ya hojaji. Katika utafiti huu,

hojaji iliyosambazwa kwa walimu ilikuwa imegawika katika sehemu ya A na B. Sehemu ya A ilihusisha habari za kimsingi kumhusu mwalimu. Sehemu ya B ilihusu vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi, mikakati inayotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi na changamoto zinazowakumba wanafunzi wakati wa kusoma vitabu vya hadithi. Mbali na hojaji mtafiti alitumia uchunzaji darasani kukusanya data za kimsingi kuhusu mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. (tazama kiambatisho 2. 1)

#### 3.6.2.2 Mwongozo wa Uchunzaji

Matumizi ya maswali ya uchunzaji yaliwezesha kunukuliwa kwa matukio yoyote darasani yaliyohusiana na mada ya utafiti. Kwa kutumia njia hii, maelezo yalipatikana kutokana na uchunguzi wa mtafiti mwenyewe pasipo kumwuliza mtafitiwa maswali yoyote (Kothari, 2012).

Uchunzaji uliweza kuibua mambo ya ndani ambayo njia zingine haziwezi kuelezea. Nkapa (1997) anaeleza kuwa uchunzaji una faida katika mazingira ambapo watu hawapendi kujieleza kwa kuongea. Stubbs (1976) anadhihirisha kuwa uchunzaji hutoa uchanganuzi wa hali halisi darasani kwa kuzingatia maelezo na rekodi zilizopo. Msingi huu ndio uliozingatiwa katika kuchagua mbinu ya uchunzaji. Uchunzaji ulifanyika darasani na hapo mtafiti aliweza kutazama na kukadiria matumizi ya vitabu vya hadithi kama wenzo katika ufundishaji wa stadi ya kusoma darasani. Mtafiti alihakikisha kuwepo kwa vitabu vya hadithi vya Kiswahili ambavyo alitumia kuthibitisha matumizi yavyo.

Mbinu ya hojaji ilitumika na kisha uchunzaji ulifanyika darasani ili kupata picha halisi kuhusu mikakati iliyotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika Shule za Msingi. Mtafiti aliingia darasani na kukaa nyuma ya darasa, mtafitiwa akifundisha ambapo aliandika matukio yote yaliyoambatana na mwongozo wa uchunzaji alioutayarisha (tazama kiambatisho 2.1).

### 3.7 Uthabiti wa Vifaa

Best na Khan (1993) wanasema kuwa, uthabiti ni kiwango cha kupima ukamilifu wa kitu kinachotarajiwa kupimwa. Kerlinger (1976) naye anasema kuwa, uthabiti ni usahihi wa vifaa vya kupima upana wa mbinu za kukusanya data. Kutokana na maelezo hayo, maswali ya hojaji na mwongozo wa uchunzaji ambavyo ni vifaa vya utafiti huu vilihitaji kupima ukweli. Ili kupima usahihi wa data iliyokusanywa kwa kutumia vifaa hivi, mtafiti alivifanyia majaribio katika shule mbili. Majibu katika majaribio ya vifaa vya utafiti yalionyesha kuwa, kulikuwa na sehemu ambazo hazikueleweka kutokana na hojaji zilizotayarishwa.

Field (2005) anaeleza kuwa uchanganuzi wa kigezo ni kifaa cha uchunguzi kilichotumiwa kwa kusaidia mtafiti kutoa uamuzi ikiwa vigeu vinavyochunguzwa vinafafanua vigeu tegemezi. Uchanganuzi wa majibu katika majaribio ya nyenzo ulimsaidia mtafiti kurekebisha baadhi ya maswali kwa madhumuni ya kuboresha maswali na kuyafanya yawe na mantiki katika utafiti huu. Hivyo basi mtafiti alishirikiana na wasimamizi wake ili kuimarisha nyenzo na kuandika upya kwa kusudi la kufanya maswali ya hojaji na mwongozo wa uchunzaji yalingane na malengo ya utafiti. Katika muktadha wa utafiti huu, uthabiti ulirejelea matokeo ambayo yalieleza athari ya kutosoma na kutotumia vitabu vya hadithi kwa kuimarisha stadi ya kusoma katika shule za Manispaa ya Kakamega.

### 3.8 Uaminifu wa Vifaa

Uaminifu ni tathmini ya nyenzo za utafiti (Enon 2005) ili kupima majibu yaliyotolewa kwa wakati tofauti. Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003) kando na vifaa kuwa thabiti ni sharti vizingatie uaminifu ili viwe faafu katika utafiti. Pia Heaton (1988) anasema ya kwamba, mbali na vifaa kuwa thabiti ni lazima vizingatie uamilifu wao. Vifaa huwa na uaminifu iwapo matokeo sawa kwa kipindi kingine tofauti yatatolewa. Mtafiti aliwapa walimu wawili kutoka shule tofauti hojaji sawa mara mbili kwa siku tofauti. Mtafiti amekubaliana na maoni ya Mugenda na

Mugenda kwani utafiti wake ulikuwa na lengo la kuchunguza mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

### 3.9 Majaribio ya Vifaa vya kukusanya Data

Mark na Peter (2001) waneleza ya kwamba majaribio ya awali ya nyenzo humwezesha mtafiti kugundua udhaifu na ubora wa nyenzo zake. Kwa mujibu wa Best na Khan (2003) majaribio huwa toshelevu iwapo yalichunguza kwa makini kile kilicholengwa kupimwa. Matatizo huweza yakawa ya utunzi mbaya wa maswali usio mwafaka na kadhalika. Matatizo haya ni sharti yarekebishwe kabla ya utafiti kamili kuanza.

Vifaa vya utafiti vilifanyiwa majaribio kwa walimu wawili wanaofundisha Kiswahili katika darasa la nne; mmoja wa shule ya msingi ya umma na mwingine wa shule ya kibinafsi ya katika Manispaa ya Bungoma ya Kaunti Ndogo ya Bungoma ya Kati. Kusudi la kufanya jaribio hilo ni kupima au kutahini ili kujua ikiwa vifaa hivyo vilifaa kutumiwa kwa utafiti huo kwa nia ya kuviboresha ili kuzidisha urazinishaji na uhalalishaji wa vifaa hivyo. Shule hizi zilihusishwa kupitia uteuzi wa kimaksudi. Majaribio yenyewe yalichukua muda wa siku mbili kila shule ikitengewa siku moja. Walimu wawili katika kila shule walipewa hojaji kujaza na wanafunzi 55 kutoka shule ya msingi ya umma na 25 kutoka shule ya kibinafsi walitazamwa wakisoma vitabu vya hadithi wakati wa funzo la kusoma. Watafitiwa walijaza hojaji ilhali uchunzaji ulifanywa darasani wakati wa kipindi cha kusoma vitabu vya hadithi. Miongoni mwa madhumuni ya majaribio haya yalikuwa ni kugundua udhaifu kwenye vifaa hivi. Ugunduzi wa udhaifu ulitumiwa kuboresha maagizo yaliyotolewa, muundo wa maswali, kushughulikia ugiligili wowote kwenye muundo wa maswali yaliyoandaliwa na kukadiria ikiwa nyenzo zingefaa katika kufaulisha uchanganuzi wa data baadaye.

### 3.10 Utaratibu wa Kukusanya Data

Mtafiti alipewa idhini ya kufanya utafiti kutoka NACOSTI na kibali cha Wizara ya Elimu ya Kaunti ya Kakamega na Kamishona wa Kaunti ya Kakamega. Mtafiti aliomba walimu

wakuu wa shule husika walioarifiwa kuhusu utafiti uliofanyika katika shule zao ambao walimpa kibali cha kufanya utafiti katika shule zilizoteuliwa. Walimu wakuu walitoa idhini. Walimu waliofundisha darasa la nne waliarifiwa na walimu wakuu kuhusu utafiti huu.

### 3.11 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data iliyokusanywa kupitia kwa hojaji na uchunzaji ilichanganuliwa kimaelezo na kitakwimu. Msingi wa kuainisha miitiko ulikuwa kuweka pamoja vipengele mbalimbali ambavyo vilishughulikia lengo moja la utafiti. Uchanganuzi huu ilifanywa ili kukusanya data inayopambanua mikakati inayotumiwa katika ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Kutokana na hojaji kila swali lilichujwa tofauti tofauti ili kuainisha miitiko kulingana na malengo manne. Hojaji zote zilichanganuliwa kwa kutumia uradidi wa utokeaji na miitiko maalum iliyokokotozwa na kuelezwa kitakwimu. Matokeo yaliwasilishwa kimaelezo na kwa viwango vya asilimia. Tathmini elezi zinafaa katika usoroveya kutokana na hali kuwa, vifaa hivi hushughulikia mikakati inayotumiwa kufundishia somo husika.

Uchunzaji wa ufundishaji darasani ulifanyika na data iliwasilishwa ili kulinganisha data iliyopatikana kutokana na hojaji. Sampuli ya utafiti iligawanywa katika makundi mawili ya aina za shule yaani za umma na za kibinafsi. Kutokana na utafiti huu, mbinu na vifaa vya kukusanya data vilichunguzwa na matokeo kuhusu mikakati iliyotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi kuwasilishwa kupitia asilimia, chati, grafu na majedwali.

### 3.12 Matatizo Nyanjani

Utafiti huu ulikumbwa na matatizo kadhaa. Mtafiti alihairisha siku alizotengea kufanya utafiti katika shule tatu zilizosalia kwa sababu ya hali ya anga ambayo ilitatiza usafiri. Baadhi ya sehemu za mji wa Kakamega zilikuwa na barabara mbovu ambapo usafiri ulitatizika

hasa kwa kutumia pikipiki wakati wa mvua. Ilibidi awasiliane na watafitiwa hao ili kupanga siku nyingine.

Tatizo lingine lililojitokeza ni kwamba baadhi ya walimu hawakuwa radhi kushiriki katika utafiti. Ilichukua muda kuwashawishi kwamba matokeo ya utafiti yasingeathiri kwa vyovyote vile kazi zao. Mtafiti pia alipata changamoto ya kukosa muda wa kutosha wa kutagusana na walimu kwa vile walikuwa na shughuli nyingine walizostahili kutekeleza. Ilibidi apange vikao vya ziada ili kulishughulikia suala hili. Aidha mtafiti hakusanya hojaji kwa muda aliopanga kwa vile hazikuwa zimejazwa na baadhi ya walimu. Ilibidi kuwasihi walimu wajaze hojaji hizo kwa muda uliofaa.

### 3.13 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyaji wa data, uthabiti wa vifaa, uamilifu wa vifaa, majaribio ya vifaa vya kukusanya data, utaratibu wa kukusanya data, uchanganuziwa data na matatizo nyanjani. Vifaa vya utafiti vilikuwa hojaji na uchunzaji. Sura inayofuatia inalenga uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo yaliyokusanywa kutoka nyanjani kwa kutumia hojaji na mwongozo wa uchunzaji. Data ilichanguliwa kwa mtindo wa maelezo kwa kutumia majedwali, asilimia na chati kwa madhumuni ya kuifanya ieleweke kwa urahisi. Inatoa ripoti kuhusu mikakati ya kufundishia Stadi ya Kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Mtafiti alichunguza vigezo vya uteuzi wa vitabu vya hadithi vinavyotumiwa na walimu wanapofundisha stadi ya kusoma, Maandalizi ya walimu ya ratiba ya kazi, andalio la somo na matumizi ya vitabu vya hadithi wanavyofundishia stadi ya kusoma, mikakati ambayo walimu hutumia kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi, jukumu la mwanafunzi katika ukuzaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

## 4.2 Vigezo vya Uteuzi wa Vitabu vya Hadithi

Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE) ambayo ilibadilishwa na kuwa (KICD) huchunguza vitabu vya Kiswahili vilivyochapishwa na kupendekeza vile bora vilivyo katika "Orange Book" kutumiwa shuleni. Kulingana na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala nchini Kenya, (KICD) orodha ya vitabu vimeidhinishwa na ni wajibu wa kila shule kuchagua vitabu vya hadithi katika kila darasa. Utafiti ulinuia kubainisha vigezo vilivyotumiwa na walimu katika kuteua vitabu vya hadithi.

### 4.2.1 Vitabu vyenye Kiwango cha Wanafunzi Kilugha

Kigezo cha vitabu vyenye kiwango cha wanafunzi ni muhimu wakati wa uteuzi wa vitabu vya hadithi. Sababu ni kwamba, mwanafunzi anatarajiwa kuelewa kile anachokisoma ili awe na uwezo wa kutumia muda wake kujisomea vitabu vya hadithi. Kwa mujibu wa Njogu na Njange (2011) mwanafunzi anapoelewa akisomacho huwezeshwa kujisomea yeye

mwenyewe ambao ni mkakati bora wa kupanua msamiati wake, kupata mafunzo mbalimbali na kustawisha mazoea ya kupenda na kufurahia kusoma. Musau na Chacha (2001) nao wanasisitiza uteuzi wa vitabu vya hadithi unaorejelea kiwango cha wanafunzi kilugha.

**Jedwali 4.1 Vitabu vyenye Kiwango cha Wanafunzi Kilugha**

| **Mwitiko** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndio<br>La | 12<br>14 | 46<br>54 |
| Jumla | 26 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Jedwali 4.1 linaonyesha kigezo cha kuteua vitabu vyenye kiwango cha wanafunzi kilugha. Miongoni mwa watafitiwa 26 waliotumia vitabu vya hadithi kufundishia stadi ya kusoma, 12 (46%) walizingatia vitabu vyenye kiwango cha wanafunzi kilugha. Kigezo hiki hakikutumiwa na watafitiwa 14 (54%).

### 4.2.2 Vitabu Vinavyoeleweka kwa Urahisi

Kigezo hiki ni cha muhimu mno ambacho kinahitaji kuzingatiwa wakati wa uteuzi wa vitabu vya hadithi. Kwa mujibu wa Ruthiri (2012) vitabu vilivyoteuliwa kusomwa na wanafunzi vilikuwa na makosa ya kisarufi na sentensi ndefu zilizowakanganya. Vitabu vya hadithi vinavyoteuliwa viwe na msamiati mwepesi na sentensi fupi za kueleweka kwa urahisi kwa kuzingatia kiwango cha uelewa cha wanafunzi.

**Jedwali 4.2 Vitabu Vinavyoeleweka kwa Urahisi**

| **Mwitiko** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndio<br>La | 18<br>8 | 69<br>31 |
| Jumla | 26 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

### 4.2.3 Vitabu Vinavyoeleweka kwa Urahisi

Kigezo cha uteuzi wa vitabu vinavyoeleweka kwa urahisi kilizingatiwa na walimu 18 (69%) na walimu 8 (31%) hawakuzingatia kigezo hiki cha uteuzi wa vitabu vya hadithi. Utafiti huu umeonyesha kuwa uteuzi wa vitabu vya hadithi usipofanywa vizuri, ni mojawapo ya hali zinazosababisha ugumu katika usomaji miongoni mwa wanafunzi.

### 4.2.4 Vitabu Vilivyo na Vichoro na Picha

Kwa mujibu wa Aras (2012) anasema kuwa, picha zinaweza kuwa kichocheo cha kuwatanguliza wanafunzi wachanga kwa fasihi. Anasisitiza kuwa matumizi ya picha huwasaidia wanafunzi kupata mbinu bunifu kwa kuwa motisha na kuwafanya wawe makini kwa lile jambo wanalolisoma. Aliendelea kusema ya kwamba picha huchangia kwa ule muktadha ambao lugha imetumika na pia kuleta ulimwengu mzima darasani.

Musau na Chacha (2001) wanaeleza kuwa, picha, michoro na vibonzo hutumika ili kuchochea hisia za mwanafunzi na mwalimu anapouliza maswali kuhusiana nazo, huwapa moyo kujadiliana kwa mapana kile wanachoona na fasiri zake.

Hivyo basi huweza kumfanya mwanafunzi kuwa mdadisi, kumfikirisha, kujielekeza na hata kuiandika mada fulani. Pia picha humhamasisha mwanafunzi akataka kujifunza misamiati na miundo mipya kupitia kuchochea uwezo wa kubuni.

**Jedwali 4.3 Vitabu Vilivyo na Michoro na Picha.**

| **Mwitiko** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndio<br>La | 6<br>20 | 23<br>77 |
| Jumla | 26 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Kigezo cha kuteua vitabu vilivyo na michoro na picha za kuelimisha, kueleweka na kufurahisha wanafunzi kilizingatiwa na walimu 6 (23%). Kigezo hiki hakikuzingatiwa na walimu 20 (77%).

### 4.2.5 Vitabu Vyenye Kurasa Chache.

Kigezo kingine kilichozingatiwa na watafitiwa ni kile cha kuteua vitabu vyenye kurasa chache ambavyo husomwa katika kipindi kimoja. Vitabu hivi vinahitaji kuwa na urefu unaofaa kwa darasa linaloshughulikiwa. Kulingana na Musau na Chacha (2001) wanafunzi wanapoteuliwa vitabu ambavyo vina urefu wa kiwango chao, wao hupata hisia za furaha na mafanikio wanaposoma na kukikamilisha.

**Jedwali 4.4 Vitabu Vyenye Kurasa Chache.**

| Mwitiko | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Ndio | 10 | 38 |
| La | 16 | 62 |
| Jumla | 26 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Walimu 10 (38%) walitumia kigezo hiki kwa kuteua vitabu vya hadithi nao walimu

16 (62%) hawakuzingatia kigezo hiki cha uteuzi wa vitabu vya hadithi. Kigezo cha vitabu vyenye kurasa chache ambavyo husomwa katika kipindi kimoja hakikuzingatiwa na walimu wengi (62%). Hali hii inaonyesha ya kwamba asilimia kubwa ya walimu hawakuchagua vitabu vyenye kurasa chache ambavyo vinaweza kusomwa katika kipindi kimoja. Kutokana na matokeo haya kigezo ambacho kilitumiwa na walimu wengi walipoteua vitabu ni kile cha kuteua vitabu vinavyoeleweka kwa urahisi (tazama majedwali 4.1, 4.2, 4.3 na 4.4).

Kwa hivyo inaonyesha kuwa vigezo vya uteuzi bora wa vitabu vya hadithi vinaweza kutumiwa kama kichocheo cha kujenga utamaduni wa usomaji miongoni mwa wanafunzi. Jambo la muhimu ni washikadau kuweka mikakati ya namna ya kuwaelekeza wanafunzi wa viwango mbalimbali kujua namna ya kuendeleza ubunifu wao.

**4.3 Maandalizi ya Walimu Darasani**

Kulingana na Nabwire (2002) na Khan (1999) mbinu ya uchunzaji ilitumika kama mbinu ya mjalizo kwa zingine kama vile hojaji na usaili ili kuthibitisha habari husika. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu ni uchunguzi usioshirikisha mtafitiwa. Kothari (2012) anasema kuwa kwa kutumia uchunzaji, mtafiti hutafuta data kwa kushuhudia data yeye mwenyewe na wakati mwingi bila kushirikisha watafitiwa.

Kwa hivyo utafiti huu ulitumia hojaji na mwongozo wa maswali ya uchunzaji ili kupata data ya kimsingi na sahihi moja kwa moja kwa kuchunguza shughuli za walimu na wanafunzi wakati wa michakato ya ufundishaji wa somo la usomaji kwa kutumia vitabu vya hadithi darasani. Kutokana na utafiti huu, walimu 65 walipewa hojaji kujaza na kumi na wawili kuchunzwa wakiendeleza somo la kusoma.

KIE (2002) imeorodhesha malengo ambayo mwalimu huhitaji kutimiza anapofundisha darasani. Ili kushughulikia malengo haya, mwalimu huandaa ratiba yakazi na mpangilio wa somo husika ili awe na uwezo wa kutimiza lengo husika. Stakabadhi hizi ndizo zinazomwelekeza mwalimu kutayarisha vifaa vinavyohitajika. Katika kufundisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi mwalimu ni sharti awe na vitabu vya kutosha wanafunzi ili kufanikisha somo hili. Kwa hivyo, jedwali lifuatalo limeonyesha jinsi walimu walivyojiandaa kwa minajili ya kufundisha somo hili.

**Jedwali 4.5 Maandalizi ya Mwalimu: Data ya Hojaji**

| | **Ndio** | **La** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Ratiba | 35(53.8%) | 30(46.2%) | 100% |
| Andalio La Somo | 30(46.2%) | 35(53.8%) | 100% |

Kutokana na hojaji, baadhi ya walimu waliandaa somo la kusoma vitabu vya hadithi kabla ya kufundisha. Walimu 35 (53.8%) walikuwa wametayarisha ratiba ya somo, ilhali walimu 30 (46.2%) hawakuandaa somo la kusoma kupitia usomaji wa vitabu vya hadithi. Walimu 30 (46.2%) waliandaa mpangilio wa somo na 35 (53.8%) hawakuandaa mpangilio wa somo. Kwa mujibu wa Sitima (1988) maandalizi ya mwalimu ni muhimu sana kwa sababu humwezesha kufunza kwa kutimiza lengo husika bila tatizo lolote. Hali hii huenda imechangia

kwa wanafunzi wengi kukosa ari ya kusoma kwa vile baadhi ya walimu hawakuwa na maandalizi kabambe ya somo (tazama jedwali 4.5).




**Kielelezo 4.1: Maandalizi ya Mwalimu: Data ya Uchunzaji**

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Licha ya walimu kudai kuwa maandalizi ya somo yalikuwa muhimu, uchunzaji darasani ulibainisha kuwa walimu 15 (23.1%) walitayarisha ratiba ya masomo, walimu 5 (7.7%) waliandaa andalio la somo pekee yake, walimu 25 (38.5%) walikuwa wameandaa ratiba ya somo na andalio la somo na walimu 20 (30.8%) hawakuandaa ratiba ya somo wala andalio la somo. Matokeo yalionyesha ya kwamba kuna baadhi ya walimu ambao hawakujitayarisha ipasavyo kwa minajili ya kufundisha kipindi cha kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi kama ilivyopendekezwa na taasisi ya ukuzaji wa mitaala (KICD) (tazama kielelezo 4.1).

### 4.3.1 Umilisi wa Mwalimu

Katika utafiti huu, uchunguzi ulifanywa ili kujua iwapo walimu wa Kiswahili walielewa mada zinazohusiana na stadi ya kusoma. Kuna stadi nne muhimu sana kwa kukuza lugha ya Kiswahili. Stadi hizi ni: kusikiliza, kuongea au kuzungumza, kusoma na kuandika. Stadi hizi zinapaswa kufunzwa moja baada ya nyingine mtawalia ili mwanafunzi aweze kuimudu lugha ya Kiswahili. Stadi ya kusikiliza ndiyo stadi ya kwanza anayohitajika mwalimu kumfunza mwanafunzi. Stadi ya kuzungumza hufuata kisha stadi za kusoma na kuandika.

**Jedwali 4.6 Stadi za Lugha.**

| Stadi za Lugha | Rahisi sana kufunza | Rahisi kufunza | Ngumu kufunza | Ngumu sana kufunza |
|---|---|---|---|---|
| Kusikiliza | 15(23%) | 25(39%) | 15(23%) | 10(15%) |
| Kuzungumza | 15(23%) | 30(46%) | 15(23%) | 5(8%) |
| Kusoma | 20(31%) | 20(31%) | 17(26%) | 8(12%) |
| Kuandika | 20(31%) | 10(15%) | 25(39%) | 10(15%) |

Kulingana na matokeo walimu 40(62%) walieleza kuwa stadi ya kusikiliza inayohitaji mwanafunzi kusikiliza kisha atamke maneno ipasavyo waliielewa na walisema ni rahisi sana kufunza. Walimu 45(69%) walielewa na kujua kuifunza stadi ya kuzungumza na kutamka. Walimu 40(62%) walielewa stadi ya kusoma na walimu 30(46%) walielewa kufunza stadi ya kuandika na kusema ni rahisi kuifunza. Asilimia zilizotajwa zilibainisha uelewa wa stadi hizo ambazo walimu hawa walisema zilikuwa rahisi sana kufunza na hivyo hawakushuhudia tatizo lolote.

Kwa upande mwingine, asilimia zifuatazo za walimu zilidhihirisha ugumu wa kufunza stadi za Kiswahili. Walimu 25(38%) walichukulia stadi ya kusikiliza kuwa ngumu kufunza. Walimu 20(31%) walichukulia stadi ya kuzungumza kuwa ngumu. Walimu 25(39%) walipata ugumu kufundisha stadi ya kusoma na kwa walimu 35(54%), stadi ya kuandikailiwawia ngumu kuifunza. Hali hii ilichukuliwa kuchangia kutofunza ipasavyo stadi hizi za Kiswahili. Mwalimu anapokosa umilisi wa kutosha katika mada fulani, wanafunzi hawawezi kufunzwa vizuri (tazama jedwali 4.6).

Walimu 10(15.4%) walisema ni rahisi kufunza stadi ya kusikiliza. Walimu 30(46.2%) nao walieleza ya kwamba walielewa stadi ya kuzungumza. Walimu 20(30.8%) walielewa stadi ya kusoma na walimu 10(15.4%) walielewa stadi ya kuandika. Walimu hawa walisema stadi hizi zilikuwa rahisi kufunza na hivyo hawakushuhudia tatizo lolote. Walimu 20(30.8%) walisema ya kwamba stadi ya kusikiliza ilikuwa rahisi kiasi. Walimu 15(23.1%) walielewa stadi ya kuzungumza kiasi. Walimu 20(30.8%) walichukulia stadi ya kusoma kuwa rahisi kiasi na walimu 25(38.5%) walichukulia stadi ya kuandika kuwa rahisi kiasi.

## 4.4 Namna Walimu Wanavyotumia Vitabu vya Hadithi Kufundishia Stadi ya Kusoma

Kusoma vitabu vya hadithi na taarifa mbalimbali hukuza lugha ya mwanafunzi, msamiati wake na ujuzi wa kujieleza katika lugha hiyo. Kusoma kwa ziada humpa mwanafunzi nafasi ya kufahamu mifumo, miundo na matumizi tofauti ya lugha.

Mwalimu anajukumu la kuwateulia wanafunzi wake vitabu kwa kuzingatia sifa maalum. Sifa hizi ni kama zifuatazo: Vitabu vinavyoteuliwa viwe vinavyoweza kuwafurahisha na kuwaburudisha wanafunzi, kitabu kizuri kiwe cha kiwango cha wastani cha matumizi ya msamiati unaolingana na uwezo wa wanafunzi kilugha, maneno mengi yasiwe mageni kwani hili huweza kuwachosha wanafunzi. Aidha kisiwe na miundo tata ya kisarufi. Kulingana na Njogu na Nganje (2011) vitabu vya hadithi vichaguliwe kwa kuzingatia viwango vya wanafunzi.

Wanaeleza kuwa kuanzia darasa la nne hadithi zinazosomwa ni ndefu ambapo wanafunzi huhitaji misaada mbalimbali ili wajiendeleze.

**Jedwali 4.7 Matumizi ya Vitabu vya Hadithi.**

| **Mwitiko** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndio | 26 | 40 |
| La | 39 | 60 |
| Jumla | 65 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Matokeo yamefichua ya kwamba walimu 39 (60%) hawatumii vitabu vya hadithi kwa kuimarisha stadi ya kusoma. Walimu 26 (40%) huwapa wanafunzi vitabu vya hadithi ili wawe na uwezo wa kusoma (tazama jedwali 4.7).

Kwa hivyo ilionekana kuwa, matumizi ya mkakati wa kusoma vitabu vya hadithi hautumiwi kwa kiwango kinachoridhisha. Kwa mujibu wa Flavia (2011) utamaduni wa kusoma vitabu vya hadithi miongoni mwa wanafunzi na wazazi wao haujamakinika nchini Kenya. Hii umetokana na umaskini, njia potovu za ufundishaji wa fasihi na ukosefu wa vitabu hivyo maktabani.




**Kielelezo 4.2 Mikakati ya Kufundishia Stadi ya Kusoma**

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Kulingana na Batambuzi (2007) watu hawawezi kujenga utamaduni wa kusoma pale ambapo hakuna cha kusomwa.Walimu walipoulizwa sababu zilizofanya wasitumie vitabu hivyo walitoa sababu zifuatazo: Walimu thelathini na watano (35) ambayo ni asilimia tisini (90%) ya walimu thelathini na tisa (39) ambao hawatumii vitabu vya hadithi walisema hawana muda wa kutosha wa kujiandaa kwa sababu ya kazi nyingi. Walimu 35 ambayo ni asilimia sabini (70%) walitoa sababu ya uchache ya vitabu. Walimu 23 (60%) walisema ukosefu wa mazingira bora ya usomaji kama vile maktaba, madawati ya kutosha na msongamano wa wanafunzi ulizuia kutumia mbinu hii. Walimu wasiotumia vitabu vya hadithi kufundishia kusoma walipoulizwa mikakati waliyotumia, asilimia 56% ya walimu 39 walisema kuwa wao hutegemea vitabu vya kiada na makala yaliyomo kufunza stadi hii. Walimu 10 (26%) walisema walitumia mkakati wa

wanafunzi kutazama picha na kutamka huku walimu 7 (18%) wakitumia mbinu ya kadi za maneno (tazama Kielelezo 4.2)

### 4.4 Vipindi Vilivyotengewa Kusoma Vitabu vya Hadithi

Mazoezi ya kusoma vitabu vya hadithi ni muhimu ili kuweza kuimarisha stadi ya kusoma. Abbas (2013) alibainisha ya kwamba ni jambo la basara mwalimu kuandaa kipindi maalum kwa ajili ya kutembelea maktaba angalau mara moja kwa wiki.




**Kielelezo 4.3: Vipindi Vilivyotengewa Kusoma Vitabu vya Hadithi**

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Kutokana na matokeo, kielelezo 4.3 kinaonyesha kwamba walimu 10 (39%) kati ya walimu 26 waliokiri kutumia vitabu vya hadithi kufundisha stadi ya kusoma waliripoti kuwa wanafunzi walipewa vitabu vya hadithi kuvisoma mara moja tu kwa wiki. Walimu 4 (15%) ya walimu waliripoti kuwa wanafunzi hutengewa vipindi viwili kusoma vitabu vya hadithi, kipindi kimoja cha somo la uchoraji au mazoezi ya viungo. Walimu 12(46%) ya walimu

walisema kuwa, wanafunzi hupewa nafasi ya kusoma vitabu vya hadithi muda wa ziada kama vile baada ya chamcha, jioni kabla ya masomo ya kirasmi au wakati wanapokuwa nyumbani.

Hivyo basi tunachukulia kuwa walimu wengi hawakutilia maanani usomaji wa vitabu vya hadithi, kwani imeonyesha kuwa walimu wengi hawakushughulikia kutenga muda mwingine wa kujenga mwelekezo ufaao katika hali ya usomaji wa vitabu vya hadithi. Imebainika wazi kuwa wanafunzi waliachwa pekee yao kujisomea pasipo mwongozo wa mwalimu. Hali ambayo hutingwa na ushindani kutoka kwa masomo mengine ikizingatiwa kuwa wanafunzi hao walipewa kazi za ziada au mazoezi ya kufanya wakati huo wa ziada. Kwa mujibu wa Abbas (2013) mwalimu anapaswa kuandamana na wanafunzi wake hadi maktabani na kushirikiana na mkutubi ambaye anahitaji kuwa mstari wa mbele katika kuwafunza matumizi ya maktaba hatua baada ya hatua.

## 4.5 Mikakati ya Kufundishia Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi

### 4.5.1 Mikakati Andalizi kwa Matumizi ya Vitabu vya Hadithi

Utafiti huu ulichunguza mikakati ambayo walimu hutumia kuwaandaa wanafunzi kwa matumizi ya vitabu vya hadithi kufundishia stadi ya kusoma. Mikakati ambayo ilichunguzwa ilikuwa ni: kuhamasisha wanafunzi kusoma kwa ziada, kuwachagulia vitabu faafu vya viwango vyao vya kuwafurahisha na kuwaburudisha, kuwahimiza wasome kwa kasi wakifululiza, kuwapa vitabu vya kujisomea nyumbani na kuorodhesha vilivyosomwa na kila mwanafunzi na kuwafanya wanafunzi kuandika insha kurejelea hadithi walizosoma, kuhakikisha vitabu vya hadithi vinakuza msamiati, istilahi na miundo ya sentensi. Miongoni mwa walimu 15 waliokiri kutumia vitabu hivi katika ufundishaji wa stadi ya kusoma, takwimu za matokeo zilionyesha kuwa walimu 22 (85%) wanafunzi kusoma kwa ziada. Walimu 3 (15%) hawakuhamasisha wanafunzi kusoma kwa ziada. Walimu 10 (38%) waliwachagulia wanafunzi vitabu faafu vya hadithi vya viwango vyao vya kuwafurahisha na kuwaburudisha. Walimu 16 (62%) hawakuwachagulia vitabu vya hadithi vya kusoma ili viwafurahishe na kuwaburudisha. Walimu 12 (46%)

waliwahimiza wanafunzi kusoma kwa kasi wakifululiza. Walimu 14 (54%) hawakuwahimiza wanafunzi kusoma kwa kasi wakifululiza. Walimu 4 (19%) waliwapa wanafunzi vitabu vya kujisomea nyumbani na kuorodhesha vilivyosomwa na kila mwanafunzi. Walimu 21(81%) hawakuwapa wanafunzi vitabu vya kujisomea nyumbani wala hawakuorodhesha vilivyosomwa na kila mwanafunzi. Walimu 4 (15%) tu ndio waliohakikisha wamechagua vitabu vinavyorejelea mazingira na tajriba zao kama vile umri, maadili na tamaduni za wanafunzi. Walimu 17 (65%) hawakuhakikisha vitabu vya hadithi vinavyokuza msamiati, istilahi na miundo ya sentensi ndivyo vinavyosomwa na wanfunzi. Walimu 9 (35%) ndio waliozingatia kigezo hicho.

Kutokana na matokeo haya mkakati unaotumiwa sana ili kumsaidia wanafunzi kusoma kwa ufasaha ni kuhamasisha wanafunzi kusoma vitabu vya hadithi wakati wa ziada. Idadi kubwa ya walimu walitumia mbinu hii ili kuimarisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi (tazama Kielelezo 4.4)




**Kielelezo 4.4 Mikakati Andalizi kwa Matumizi ya Vitabu vya Hadithi**

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

### 4.5.2 Mikakati ya kufundisha kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi Darasani

Utafiti ulibainisha kuwa walimu 26 (40%) tu ndio waliotumia vitabu vya hadithi kufundishia stadi ya kusoma (tazama jedwali 4.7). Ilikuwa nia ya mtafiti kubainisha mikakati wanayopendelewa nawalimu, kufundishia stadi ya kusoma wanapotumia vitabu vya hadithi. Miongoni mwa hawa, utafiti ulifichua kuwa kuna mikakati ambayo hutumika na walimu ili kufaulisha usomaji wa vitabu vya hadithi. Walimu 19(73%) walieleza ya kwamba wao hupendelea kuwaweka wanafunzi katika vikundi ili wagawiwe vitabu vya hadithi na kusoma kimoyomoyo. Walimu 7 (27%) hawatumii mkakati huu. Walimu 14(54%) tu ndio huwahusisha wanafunzi katika usomaji kwakuchagua mwanafunzi mmoja kutoka kwenye makundi kusoma wengine wakimsikiliza. Walimu 12 (46%) hawatumii mkakati huu wa kuchagua mwanafunzi mmoja kusoma wengine wakimsikiliza. Mkakati unaompa kipaumbele wanafunzi ndio unaopendelewa sana. Walimu 25 (96%) walisema wao hupendelea kusoma wanafunzi wakisikiliza huku mwalimu 1 (4%) akisema hautumii mkakati huu.

Hali hii husaidia kuboresha matamshi bora ikiwa mwalimu anayesoma hajaathirika na lugha mama. Kutokana na matokeo haya walimu husoma vitabu vya hadithi ili wanafunzi waige matamshi bora na kuwanyima nafasi ya kufanya mazoezi ya kutamka wao wenyewe. Kuandika insha inayorejelea hadithi waliyoisoma wanafunzi hukuza uwezo wao wa kukumbuka stadi ya kusoma kwani huwa ni njia moja ya kukariri matamshi kimoyomoyo wakikumbuka walivyoyatamka maneno katika hadithi darasani (Mirikau, 2013).

**Jedwali 4.8 Mikakati ya kufundishiakwa matumizi ya vitabu vya hadithi darasani**

| Mikakati | Unatumika | Hautumiki |
|---|---|---|
| Wanawekwa katika vikundi kusoma kimoyomoyo | 19 (73%) | 7 (27%) |
| Wanawekwa katika vikundi na mmoja kusoma kwa zamu wengine wakimsikiliza | 14(54%) | 12 (46%) |
| Mwalimu anasoma wanafunzi wakimsikiliza | 25 (96%) | 1 (4%) |
| Kuwafanya wanafunzi kuandika insha kurejelea hadithi walizosoma | 6 (27%) | 19 (73%) |

**Chanzo: ukokotozi wa mtafiti**

Hata hivyo, mbinu hii haikutumiwa sana na walimu. Walitoa sababu ya idadi kubwa ya wanafunzi ambayo huwatinga kusahihisha vitabu na kuwarekebisha wanafunzi. Walimu 6 (27%) tu ndio waliowapa wanafunzi insha kwa kurejelea hadithi walizosoma. Walimu 19 (73%) hawakuwapa wanafunzi insha kwa kurejelea hadithi walizosoma (tazama jedwali 4.8).

#### 4.5.2.1 Kuongoza Wanafunzi Kukariri sauti na kusaidia wenye Matatizo

Mbinu ya kukariri huimarisha ujuzi wa kusoma. Karukenya (2010) anasema matamshi ya wanafunzi yanaweza kuimarishwa kupitia ukariri wa tanzu mbalimbali za fasihi kama vile vitanza ndimi, nyimbo na hata hadithi. Anazidi kusema kuwa walimu wanafaa kuwaongoza wanafunzi kutamka maneno yenye sauti tatanishi kwao. Anafaa kuwatia shime wale walio na udhaifu kimatamshi na kuwapongeza wanaomudu matamshi.

Njia hii itajenga mwelekeo chanya wa wanafunzi kuhusu shughuli ya usomaji na hivyo kukuza utamaduni wa kusoma miongoni mwao kama vile ilivyosisitizwa na nadharia ya Utabia kulingana na Laurete Education (2015). Pia, wanafunzi wote wanafaa kuwa na fursa sawa ya kusoma ili kukuza uwezo wao bila mapendeleo.

**Jedwali 4.9 Kuongoza wanafunzi kukariri na kusaidia wenye matatizo**

| **Kauli** | **Mwitiko** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Kuongoza wanafunzi kukariri | Ndio | 11 | 42 |
| | La | 15 | 58 |
| | Jumla | 26 | 100.0 |
| Kusadia wenye matatizo | Ndio | 10 | 39 |
| | La | 16 | 61 |
| | Jumla | 26 | 100.0 |

**Chanzo: ukokotozi wa mtafiti**

Kutokana na matokeo, walimu 11 (42%) walisema kuwa waliwasaidia wanafunzi kusoma maneno yenye sauti zilizowatatiza kwa kukariri sehemu za vitabu vya hadithi. Waliongoza wanafunzi kwa kuyatamka maneno na sauti hizo ipasavyo nao wanafunzi walirudia kusoma.

Hata hivyo, wengi 15 (58%), hawakuhusisha mkakati huu katika uimarishaji wa stadi ya kusoma. Kuhusu kutambua wenye matatizo kimatamshi ili kuwasaidia, walimu 16 (61%) walieleza ya kwamba hawakujishughulisha kutambua na kusaidia wanafunzi waliokuwa na matatizo ya kusoma bali waliwachagua wengine waliojua kusoma kwa ufasaha wakasoma. Walisema sababu za kufanya hivi ni kuwa madarasa yana idadi kubwa ya wanafunzi na hivyo kumsaidia mwanafunzi mmoja mmoja ni muhali kutokana na kazi nyingi walizonazo shuleni. Hii inadhihirisha wazi kuwa ingawa vitabu vya hadithi vinatumika, mikakati bora ya kuimarisha stadi hii haikuzingatiwa.

#### 4.5.2.2 Matumizi ya Vibonzo, Ramani, Michoro na Picha Zilizomo Vitabuni

Picha, vibonzo, michoro na majedwali ni vifaa muhimu sana vya kufundishia somo la kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi. Vifaa vya kufundishia kama vile picha na michoro huwa kichocheo cha kuwasisimua watoto wachanga kwa fasihi (Aras 2012). Kwa hivyo, mwalimu anatarajiwa kutumia vielelezo hivi kuchochea ari ya wanafunzi na kuwafanya watake kusoma ili kujua kile kinachoendelea katika hadithi husika.




**Kielelezo 4.4 Picha Vibonzo, Ramani, Michoro na Picha**

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Kutokana na utafiti huu walimu 4 (20%) kwa walimu 26 waliokiri kutumia vitabu vya hadithi walitumia vielelezo hivi katika kufundishia usomaji wa vitabu vya hadithi. Vielelezo vilitumika kwa kuwaonyesha wanafunzi kisha kuwauliza maswali yaliyohusiana na picha hiyo. Mwalimu aliwapa wanafunzi moyo wa kujadiliana kwa mapana kile walichoona na kutoa fasiri zao. Walimu 21 (80%) walisema hawakutumia vibonzo, ramani, michoro na picha zilizomo vitabuni katika ufundishaji wao.

#### 4.5.2.3 Makadirio ya Walimu kwa Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Mikakati

Mintarafu ya haya matokeo, mtafiti alitafuta maoni ya walimu kuhusu mielekeo ya wanafunzi kuhusiana na namna ya usomaji wa vitabu vya hadithi darasani.

**Jedwali 4.10 Jinsi ya Kusoma Vitabu vya Hadithi.**

| Kauli | Wanapenda sana | Wanapenda kiasi | Hawapendi |
|---|---|---|---|
| Kusikiliza na kusimulia | 21(81%) | 4(15) | 1(4%) |
| Kusoma hadithi kwa sauti | 24(92%) | 1(4%) | 1(4%) |
| Kusoma kimoyomoyo | 0(0%) | 9(35%) | 17(65%) |
| Kuandika insha kuhusiana na hadithi waliyosoma | 10(39%) | 5(19%) | 11(42%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Aina mbalimbali zilizohusisha usomaji zilibainishwa na matokeo yalionyesha kuwa Wanafunzi wengi wanaopenda kusoma kwa sauti. Walimu 24 (92%) walieleza kuwa wanafunzi wao wanapenda sana kusoma hadithi kwa sauti na hakuna hata mmoja aliyeeleza ya kwamba wanafunzi wake hupenda kusoma kimoyomoyo. Walimu 21 (81%) walisema kuwa wanafunzi wao wanapenda kusikiliza na kusimulia hadithi. Walimu 10 (39%) walieleza kuwa wanafunzi wao walipenda sana kuandika insha kuhusu hadithi walizosoma (tazama jedwali 4.10).

Matokeo haya yanaonyesha jinsi walimu huwanyima wanafunzi fursa ya kujifunza stadi ya kusoma kwa kuwahusisha katika michakato ya usomaji. Kupendelea mkakati wa kuwasomea hadithi kuliko wao wenyewe kusoma ni kuwanyima fursa ya kushiriki katika ujifunzaji kwa sababu ya uhaba wa vitabu vya hadithi na muda mfupi uliotengewa kipindi cha Kiswahili.

### 4.5.3 Mazingira ya Kusoma

Ili kukuza mtoto aliyeelimika na mmilisi wa stadi zote kuna haja ya kubuni mazingira bora ya kumwezesha upataji wa elimu na stadi hizi. Misingi asili ya mazingira ya elimu ni kama vile nyenzo za masomo na shughuli mbalimbali, mazingira ya nje na mazingira ya jumuia na utamaduni. Uhusiano wa mambo haya yote hutoa mazingira mwafaka ya elimu yanayosisimua mwanafunzi (UNESCO, 2011).

Mazingira yanayoafiki elimu yanapaswa kuwa ya kusisimua. Mazingira haya ni kama vile shuleni, nyumbani, darasani, kazini na jumuia ambayo ni muhimu kwa upokezi wa elimu, maendeleo na matumizi ya milele (Easton, 2006). Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza ikiwa wanafunzi hupata mazingira yanayowawezesha kusoma vitabu vya hadithi wakiwa mahali mbalimbali kama vile shuleni na nyumbani.

#### 4.5. 3.1 Mazingira yaNdani na Nje ya Shule za Msingi

Mazingira ya nje ni kichokoo cha kujua kusoma na kuandika. Huwa na athari kwa maendeleo na kutenda kazi kwa wanafunzi. Mazingira yanayovutia na yaliyopangwa vizuri huwatia wanafunzi moyo wa kutagusana miongoni mwao wenyewe na au huwawezesha kufanya kazi yao kibinafsi au katika vikundi vidogo. Aidha kuzidisha uwezo wao wa kujua kusoma na kuandika na hukuza tabia na mienendo mizuri ya kusoma. Kuwepo kwa nyenzo kama vile vifaa halisi na chati za kufundishia kusoma na kuandika na jinsi zilivyopangwa mahali kunavutia na kuzidisha upataji wa ujuzi wa kusoma na kuandika kwa wanafunzi (UNESCO 2011). Kutokana na maelezo haya matumizi ya nyenzo yalimwezesha mwanafunzi kuyadhibiti mazingira

yake katika masomo yake. Mwanafunzi anapoambiwa jambo bila kushirikisha nyenzo huweza kusahau, anapofunzwa hukumbuka na anaposhirikishwa huelewa (Musau na Chacha 2001). Kauli hii ndiyo ilikuwa chanzo cha utafiti huu uliokusudia kuchunguza Kimazingira ambamo wanafunzi hujifunzia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

#### 4.5.3.2 Uwepo wa Maktaba Shuleni.

Maktaba ni mojawapo wa nyenzo muhimu sana shuleni katika kuimarisha stadi ya kusoma. Kutokana na utafiti wa Press Reader (2017) upo umuhimu wa maktaba shuleni kwa sababu humwezesha mwanafunzi kujisomea pasipo mwalimu. Utafiti huo uliwashauri wanafunzi kujiwekea utaratibu wa kusoma vitabu vya hadithi, majarida na magazeti, kwani kwa kufanya hivyo kutakuza uelewa.

**Jedwali 4.11 Uwepo wa Maktaba Shuleni**

| Mwitiko | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Ndio | 10 | 15.4 |
| La | 55 | 84.6 |
| Jumla | 65 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa, shule nyingi hazina maktaba ya shule. Walimu 55 (84.6%) walidhihirisha ya kwamba hakuna maktaba shuleni mwao. Asilimia kumi na tano nukta nne (15.4%) ikiwa walimu kumi walieleza kuwa shuleni mwao mlikuwa na maktaba (tazama Jedwali 4.11). Kutokana na matokeo ya utafiti huu idadi kubwa ya shule hazikuwa na maktaba. Hali hii ilionyesha kuwa wanafunzi wengi hawatumii maktaba wakati wa somo la kusoma ili kujichagulia au kuchaguliwa vitabu vya hadithi na kuvisoma.

Ukosefu wa maktaba ni ithibati ya ukosefu wa mazingira yanayovutia na yaliyopangwa vizuri kutia wanafunzi moyo wa kutagusana miongoni mwao wenyewe ili kukuza tabia na mienendo mizuri ya kusoma. Wanafunzi wanahitaji vitabu vya hadithi vingi katika maktaba ili kujenga ari na mazoea ya kusoma.

### 4.5.3.3 Utoshelevu wa Vitabu vya Hadithi

Vitabu vya hadithi ni hazina ya elimu ambavyo mwanafunzi hutumia katika masomo yake Mulokozi, 1997). Ufundishaji wa stadi ya kusoma kama kusoma kwa ziada hukuza matumizi ya lugha ya wanafunzi. Kutokana na matumizi fasaha ya lugha mwanafunzi hujenga ukwasi wa lugha wa kumsaidia kujieleza vizuri.




**Kielelezo 4.5: Utoshelevu wa Vitabu vya Hadithi**

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Utafiti huu ulionyesha ya kwamba vitabu vya hadithi havikutosha kwa kila mwanafunzi kutumia katika kipindi kimoja cha kusoma. Kigezo hiki kiliwahusisha walimu wote 65 wanaotumia na wasiotumia vitabu hivi kufundishia. Matokeo yanaonyesha kuwa walimu 61(93.8%) walieleza ya kwamba vitabu havitoshi katika madarasa yao (rejelea kiambatisho 7).

### 4.6 Majukumu ya Mwanafunzi

Lengo la nnela utafiti ilikuwa kupambanua majukumu ya mwanafunzi katika kuimarisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika darasa la nne la shule za msingi, katika eneo la Manispaa ya Kakamega. Kufikia lengo hili la utafiti kila mwalimu aliyetafitiwa aliulizwa kujibu maswali kuhusu majukumu ya mwanafunzi katika kuimarisha stadi ya kusoma. Majukumu ni mambo yanayojengeka kwa misingi ya tofauti za kibinafsi. Yale atakayotekeleza mwanafunzi wakati wa kusoma huweza kutokana na motisha ya kipekee pamoja na ujuzi wa awali na sababu mbalimbali zinazomhusu mwanafunzi katika hali za kipekee.

Kwa mujibu wa utafiti huu ilibainika kuwa ingawa kuna tofauti za kipekee miongoni mwa wanafunzi. Yapo majukumu ambayo ni ya kimsingi katika usomaji wa vitabu vya hadithi ili kufaulisha stadi ya kusoma. Musau na Chacha (2001) wanaeleza baadhi ya hayo majukumu kama ifuatayo: Wanafunzi kusoma vitabu vya hadithi kwa kasi wakifululiza, kusomea vitabu nyumbani kwa sababu ya muda mfupi shuleni, kuandika insha kwa kurejelea hadithi walizosoma, kusoma kwa kutomumunya midomo anapotamka kila sauti, kusoma kwa kutofuatiliza kidole au kusongeza kichwa, kusoma kimoyomoyo bila kutamka kila neno kwa sauti, kutoegemea dawati anaposoma na kuwa na utulivu anaposoma vitabu vya hadithi.

#### 4.6.1 Kuwepo kwa Wanafunzi Wasio na Uwezo wa Kusoma.

Utafiti linganishi wa uwezo wa wanafunzi kusoma matini andishi ulifanywa mintarafu ya walimu wanaotumia vitabu vya hadithi na wasiotumia vitabu hivi kufundishia stadi ya kusoma. Musau na Chacha (2001) wanaeleza kuwa, kusoma ni kati ya zile mbinu zinazotumiwa kukuza ujuzi wa lugha ya wanafunzi. Kusoma vitabu vya hadithi au taarifa mbalimbali hukuza lugha ya mwanafunzi, msamiati wake na ujuzi wa kujieleza katika lugha hiyo. Kusoma kunamwezesha mwanafunzi kupanua elimu yake kuhusu taaluma mbalimbali na pia aelewe tamaduni zake, watu na mahali mbalimbali. Kusoma pia humsaidia mwanafunzi aelewe mambo anayofundishwa katika masomo shuleni. Mwanafunzi hana uchaguzi katika lengo hili kwa sababu mojawapo ya malengo ya elimu ni kumkuza mwanafunzi hadi afikie kilele chake.

**Jedwali 4.12 Wanafunzi Wasiokuwa na Uwezo wa Kusoma.**

| **Matumizi ya vitabu** | **Mwitiko** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| **Wanaotumia vitabu vya hadithi** | Ndio | 10 | 38 |
| | La | 16 | 62 |
| | Jumla | 26 | 100.0 |
| **Wasiotumia vitabu vya hadithi** | Ndio | 21 | 54 |
| | La | 18 | 46 |
| | Jumla | 18 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Matokeo yalidhihirisha kwamba madarasa yaliyotumia vitabu hivi yalishuhudia kiwango kidogo cha wanafunzi wasio na uwezo wa kusoma (38%) ikilinganishwa na 54% ya wanafunzi ambao walimu wao hawakutumia vitabu vya hadithi. Umilisi wa juu wa kusoma miongoni mwa wanafunzi wanaofundishwa kwa kutumia vitabu vya hadithi unahalalisha madai ya mtafiti kuwa

matumizi ya vitabu vya hadithi ni mkakati mzuri wa kukuza usomaji na stadi ya kusoma miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi. Uwezo wa kusoma wa waliofunzwa kwa mkakati huu ulikuwa 62% ilhali wa wale wasiofunzwa kwa mkakati huu ulikuwa 46% (tazama Jedwali 4.12).

Kutokana na matokeo ya utafiti huu kuna baadhi ya wanafunzi ambao hawakuweza kusoma vitabu vya hadithi. Walimu 21(54%) wasiotumia vitabu vya hadithi walieleza ya kwamba kulikuwa na wanafunzi katika shule zao ambao walikuwa wamefika darasa la nne na hawakujua kusoma sentensi za Kiswahili. Walimu 18 (46%) ndio walioeleza ya kwamba hawakuwa na wanafunzi katika darasa la nne ambao hawakujua kusoma.

### 4. 6. 2 Jinsi ya Kusoma

#### 4. 6 .2.1 Kusoma kwa Kufululiza

Utafiti huu ulitaka kubainisha ikiwa wanafunzi waliotafitiwa walisoma kwa mfululizo na ufasaha vitabu walivyochaguliwa walivyokuwa navyo au makala mengine ya kusoma. Kutokana na utafiti huu baadhi ya wanafunzi walisoma wakifululiza japo kulikuwa na wengine waliositasita katika usomaji wao. Utafiti ulilenga wale wenye uwezo wa kusoma.

**Jedwali 4.13 Uwepo wa Wanafunzi Wenye Uwezo wa Kusoma Wakifululiza**

| Matumizi ya vitabu | Mwitiko | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Wanaotumia vitabu vya hadithi** | Ndio | 13 | 81 |
| | La | 3 | 19 |
| | Jumla | 16 | 100.0 |
| **Wasiotumia vitabu vya hadithi** | Ndio | 9 | 50 |
| | La | 9 | 50 |
| | Jumla | 18 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Ilidhihirika kuwa stadi hii ni ya kiwango cha juu miongoni mwa waliotumia vitabu vya hadithi (81%) ikilinganishwa na wale wasiotumia vitabu hivi (50%) (tazama jedwali 4.13). Matokeo yalibainisha kuwa ni asilimia ndogo tu (19%) ndiyo iliwakilisha wanafunzi wasio na uwezo wa kusoma wakifululiza miongoni mwa watafitiwa wanaotumia vitabu vya hadithi. Walimu 9(50%) wasiotumia vitabu hivi walisema kuwa wanafunzi wao walikuwa na uwezo wa kusoma wakifululiza na kwa ufasaha. Asilimia nyingine (50%) ya wanafunzi ilisitasita katika kusoma kwao. Walimu 60 (92.3%) walieleza kwamba wanafunzi wao walisoma kwa kusitasita. Kupitia uchunzaji, walimu walitumia mbinu za kukariri sauti zilizowatatiza wanafunzi na wengine waliwasomea wanafunzi vitate vinavyohusisha sauti lengwa ili waandike kama imla (tazama jedwali 4.9).

#### 4.6.2.2 Kusoma Pasi na Kumumunya Kidomo, Kufuatiliza Kidole au Kusogeza Kichwa Anapotamka Kila Sauti

Miongoni mwa wanafunzi wenye uwezo wa kusoma kwa kuegemea vitengo viwili vya walimu wanaotumia vitabu vya hadithi na wasiovitumia, swali liliulizwa kuhusu kuwepo kwa udhaifu wa kusoma kwa kufuatiliza kidole, kumumunya midomo au kusogeza kichwa.

**Jedwali 4.14 Uwepo wa Wanafunzi Wenye Udhaifu wa Kusoma.**

| Matumizi ya vitabu | Mwitiko | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Wanaotumia vitabu vya hadithi | Ndio | 2 | 12 |
| | La | 14 | 88 |
| | Jumla | 16 | 100.0 |
| Wasiotumia vitabu vya hadithi | Ndio | 11 | 61 |
| | La | 7 | 39 |
| | Jumla | 18 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Takwimu zilionyesha kwamba udhaifu huu umekita sana miongoni mwa wanafunzi wasiofunzwa kwa kutumia vitabu vya hadithi kwa asilimia 61% ikilinganishwa na asilimia 12 ya wanaotumia vitabu hivi (tazama jedwali 4.14).

## 4.7 Hitimisho

Sura hii iliwasilisha data kuhusu mikakati inayotumiwa kufundishia stadi ya kusoma katika Kiswahili kwa kutumia vitabu vya hadithi katika shule za msingi, za manispaa ya Kakamega. Data iliyowasilishwa ilihusu vigezo vinavyotumiwa na walimu kuteua vitabu vya hadithi, maandalizi ya walimu ya ratiba ya kazi, andalio la somo na matumizi ya vitabu vya hadithi wanavyofundishia stadi ya kusoma, mikakati ambayo walimu hutumia kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi na majukumu ya mwanafunzi katika ukuzaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano ambapo kila sura inashughulikia mambo maalum japo yana uhusiano wa moja kwa moja na kazi hii nzima ya utafiti. Utafiti umeshughulikia kila sura kwa undani na ukamilifu unaohitajika kiutafiti. Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vilevile iliangazia umuhimu wa utafiti, tahadhania za utafiti na maelezo ya nadharia yaliyoongoza utafiti. Hatimaye, vipengele vya upeo na mipaka ya utafiti na ufafanuzi wa istilahi zimehitimisha sura ya kwanza.

Katika sura ya pili, uhakiki wa maandishi yaliyolenga mada ya utafiti yalikuwa ya kimsingi. Maandishi haya yalihusishwa na suala na malengo ya utafiti. Aidha, katika sura ya tatu, njia na nyenzo za utafiti zilishughulikiwa. Yaliyojadiliwa ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli teuliwa, nyenzo na njia za kukusanya data na utaratibu wa kuchanganua data. Halikadhalika, sura ya nne ilishughulikia uwasilishaji wa data, matokeo ya utafiti na mjadala. Haya yalitekelezwa kwa kutumia majedwali, chati, vielelezo na maelezo. Hatimaye ni sura hii ya tano.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo manne na matokeo yake ni kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Vigezo vya Uteuzi wa Vitabu

Kwa mujibu wa Bwire na wenzake (2008), mbali na mwalimu kufuatilia usomaji wa kila mwanafunzi wa vitabu vya hadithi, anafaa kuhakikisha kuwa amewachagulia vitabu ambavyo vinajumuisha nyenzo zinazochochea hisia za kutazama, kugusa, kushika, kunusa na hata kuonja. Nyenzo hizi ni kama vile picha za rangi, vibonzo, ramani, majedwali nahata vikato vya magazeti. Nyenzo hizi huchochea mwitiko wa mwanafunzi na kumtia hamu ya kutaka kukisoma na hivyo kukuza hulka ya usomaji ambao hujenga stadi ya kusoma. Upungufu kwa

upande wa walimu kuhusu shughuli hizi unaonyesha wazi kuwa stadi hii haichochewi vya kutosha ili kuimarishwa mingoni mwa wanafunzi.

Katika uteuzi wa vitabu vya kusomwa walimu wengi walizingatia tu kigezo kimoja na kupuuza vingine. Walimu walizingatia tu kigezo cha wepesi wa lugha na kupuuza uchache wa kurasa, uwepo wa picha na michoro na vitabu vyenye kiwango cha wanafunzi kilugha. Vitabu visivyozingatia vigezo hivi huweza kuwachusha na kuwakinaisha wanafunzi na kuwa kikwazo kwa utimizaji wa malengo ya mwalimu katika somo (Miricho, 2008; Mirikau, 2008). Hivyo basi vigezo vyote vinafaa kuzingatiwa.

### 5.2.2 Maandalizi ya Walimu

Kulingana na Moseti (2003) maandalizi ya walimu kabla ya kuingia darasani kufundisha huathiri ufunzaji na ujifunzaji pakubwa. Maandalizi haya huimarisha uwasilishaji ambao huhakikisha kuwepo kwa mpangilio mzuri kuanzia mwanzo hadi mwisho wa somo. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa maandalizi haya ni ya kutilia shaka licha ya mapendekezo ya Moseti. Mintarafu ya maandalizi ya ratiba ya somo na andalio la somo data ya uchunzaji na hojaji inadhihirisha kuwa walimu hawajiandai ipasavyo kabla ya kuingia darasani kufundisha. Baadhi ya walimu walikosa ratiba ya kazi, andalio la somo na nyenzo za kufundishia, hapa nyenzo kuu za funzo hili zikiwa vitabu vya hadithi. Kuingia darasani bila ya maandalizi ya vyombo hivi ni dhihirisho wazi kuwa hawawezi kutendea haki somo la stadi ya kusoma.

### 5.2.3 Mikakati ya Kufundisha Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, inafichuliwa kuwa ufundishaji wa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi ni suala linalostahili kushughulikiwa kwa dhati na dharura. Jambo linalojitokeza ni kwamba kusoma kwa mapana kwa kutumia vitabu vya hadithi ili kuimarisha stadi ya kusoma halijashughulikiwa kwa uzito unaostahili. Utafiti unaonyesha kuwa walimu hawatumii vitabu vya hadithi kufundishia stadi ya kusoma na hivyo kuwanyima

wanafunzi fursa ya kukuza lugha yao, msamiati, ujuzi wa kujieleza katika lugha ya Kiswahili, ufahamu wa mifumo, miundo na matumizi tofauti ya lugha pamoja na stadi ya kusoma. Wengi wanatoa sababu za kukosa muda wa kuhusisha vitabu hivi kutokana na kazi nyingi. Sababu nyingine ni kukosa vitabu hivi na mazingira mabovu ya usomaji. Kwa hivyo walitegemea matumizi ya vitabu vya kiada, maandishi ubaoni, picha na kadi za maneno.

Mikakati isiyofaa ya kufundisha stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi imebainika. Kwa wachache waliokubali kuvitumia vitabu hivi, imebainika wazi kuwa wanafunzi huachwa pekee yao kujisomea pasipo mwongozo wa mwalimu. Aidha walimu hawafuatilii maendeleo ya mwanafunzi kwa kuchunguza iwapo amesoma kitabu au la. Walimu walisema kuwa, wanafunzi hupewa nafasi ya kusoma vitabu vya hadithi muda wa ziada kama vile baada ya chamcha, jioni kabla ya masomo ya kirasmi au wakati wanapokuwa nyumbani. Hali hii hutingwa na ushindani kutoka kwa masomo mengine ikizingatiwa kuwa wanafunzi hao hupewa kazi za ziada au mazoezi ya kufanya wakati huo wa ziada. Kwa mujibu wa Schroeder (2011), mchango wa mwalimu ni muhimu katika ufundishaji wa fasihi ya watoto. Anasisitiza kuwa walimu wanapaswa kujenga mwelekeo ufaao wa kufunza wanafunzi fasihi ndipo kutakuwa na mabadiliko katika hali ya usomaji.

Isitoshe, walimu wachache waliripoti kutenga vipindi na kuwapa wanafunzi wao vitabu vya hadithi kuvisoma darasani mara moja tu kwa wiki. Wengi hawakuthubutu hata kidogo. Hii inatilia shaka maandalizi ya wanafunzi katika ujenzi wa hulka ya usomaji. Kwa mujibu wa Musau na Chacha (2001) lengo kuu la kusoma kwa ziada ni kumfurahisha na kumburudisha mwanafunzi. Ikumbukwe kwamba mwanafunzi huenda shuleni ili kujifunza stadi za lugha ikiwemo Stadi ya kusoma (KIE, 2002). Kwa mfano kusoma kwa mapana kutamwezesha aelewe mambo anayofundishwa katika masomo mbalimbali. Mwalimu hupaswa kuhimiza na

kujenga ari ya mwanafunzi ya kusoma vitabu vya hadithi darasani, wakati wa burudani na mapumziko.

Kusoma darasani pekee hakutoshi kwani ni sehemu ndogo tu ya wakati wao. Wakati mrefu huhitajika kujenga uzoefu wa kusoma kwa makini na bila ya uchovu na kwa urahisi. Hivyo basi mwanafunzi ana kazi kubwa; Jukumu la mwalimu ni kumpa tu mawaidha, mwongozo na motisha ili kujenga ile tabia ya kusoma vitabu vya hadithi kwa wingi. Hivyo basi, inabainika kuwa walimu ni kikwazo kikubwa katika ukuzaji wa stadi ya kusoma miongoni mwa wanafunzi wao, kwa kukosa kuwapa usomaji uliosimamiwa wa vitabu vya hadithi ambavyo ni mhimili muhimu katika ujenzi wa stadi hii.

Usimamizi na ufuatiliaji wa mwalimu kuhusu usomaji wa wanafunzi wa vitabu vya hadithi ni mkakati muhimu katika kuimarisha upataji wa stadi ya kusoma (Wairimu, 2000). Utafiti ulibainisha kuwa walimu huishia katika kuwahamasisha tu wanafunzi kuhusu umuhimu wa kusoma kwa ziada katika kukuza stadi ya kusoma ilhali hawakufuatilia kuona kuwa umetekelezwa na wanafunzi. Walimu hawakujihusisha sana katika shughuli za kuwapa vitabu vya hadithi kujisomea nyumbani na kuorodhesha vilivyosomwa na kila mwanafunzi, kuwafanya wanafunzi kuandika insha kurejelea hadithi walizosoma kuwachagulia vitabu faafu vya viwango vyao vya kuwafurahisha na kuwaburudisha, na kuhakikisha vitabu vinarejelea mazingira na tajriba zao umri, maadili na tamaduni zao.

Mikakati inayowashirikisha wanafunzi katika hatua za ujifunzaji ndizo faafu kwa sababu huhusisha tajriba ya mwanafunzi na kuchochea ilhamu yake ya kujifunza zaidi (Wasike 2007). Utafiti ulibainisha kuwa wanafunzi wanastahabu sana kuhusishwa katika usomaji kwa kutamka sauti kisha kusimulia kuliko kusomewa na mwalimu. Hata hivyo, walimu hawakutendea haki mikakati inayoshirikisha na kuwapa kipaumbele wanafunzi katika upataji wa stadi ya kusoma. Wanapendelea njia inayowapa wao nafasi ya kusoma wenyewe mathalani kuwasomea

wanafunzi hadithi huku wakisiliza. Wanaposomewa huwa wamenyimwa fursa ya kufanya mazoezi ya matamshi. Walimu wanatoa sababu zilezile za kazi nyingi itokanayo na idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitaji kushughulikiwa pamoja na mazingira mabovu yasiyoruhusu usomaji kama vile msongamano wa wanafunzi darasani na madawati mabovu.

Hii inabainisha kuwa baadhi ya walimu huwanyima wanafunzi nafasi ya kushiriki katika kusoma. Ingawa mkakati wa kuwasomea wanafunzi matini wakisikiliza hukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza iwapo mwalimu atayatamka maneno bila athari ya lugha ya kwanza, hulemaza ujenzi wa stadi ya kusoma kwani mwanafunzi huwa msikilizaji tu badala ya kushiriki.

Walimu wachache sana waliwaongoza wanafunzi kusoma na kukariri sauti, maneno, sentensi na vifungu katika vitabu vya hadithi, wengi hawakujishughulisha kutambua na kusaidia wanafunzi waliokuwa na matatizo ya kusoma bali waliwachagua wengine waliojua kusoma kwa ufasaha wakasoma. Kuwapuuza wenye udhaifu wa kusoma kwa kutowahusisha katika usomaji kunawanyima fursa ya kujenga stadi ya kusoma kupitia mazoezi.

Vibonzo, ramani, michoro na picha zilizomo vitabuni hubeba ujumbe wa mkato na husaidia kunatisha yaliyomo kwenye akili za msomaji (Bwire na wenzake, 2008). Vielelezo hivi huwa nyenzo nzuri ya kuchochea ilhamu ya mwanafunzi kusoma zaidi. Kwa kuwa walimu wengi hawakushiriki katika uteuzi wa vitabu vya hadithi vya kusomwa na wanafunzi wao, umuhimu wa vielelezo hivi haujatiliwa maanani. Wengi wa walimu waliotumia vitabu vya hadithi vilevile walikiri kutokuwa makini sana kuhusu vielelezo hivi kama visaidizi vya kuchochea ari na ilhamu ya wanafunzi katika usomaji. Hali hii inadumaza makuzi ya stadi ya kusoma kwa kukosa kuvitumia kama kiteka nadhari na hamu ya wanafunzi na kufanya wapende hadithi. Umuhimu huu umepuuzwa na kusababisha wanafunzi wenye udhaifu wa kusoma kudorora zaidi.

Shirika la UNESCO (2011) linatambua umuhimu wa mazingira ya nje na ndani ya shule katika kuwawezesha wanafunzi kusoma vitabu vya hadithi na kukuza stadi ya kusoma. Lilibainisha kuwa mazingira yanafaa kuwa ya kusisimua na kuchochea hisia za mwanafunzi na kumwezesha kupata stadi hii. Utafiti umeonyesha kuwa shule nyingi hazina maktaba wala mahali maalum palipotengewa usomaji wa vitabu vya hadithi. Vilevile, walimu wengi walikiri kutowapa wanafunzi vitabu hivi kutokana na ukosefu wa mazingira bora ya kuvisomea.

Mazingira yenye upungufu wa madawati, nafasi ya kukaa kwa starehe na utulivu yanayosababishwa na msongamano wa wanafunzi darasani na ukosefu wa maktaba ndizo sababu zilizojitokeza kama vikwazo katika uwezeshaji wa wanafunzi kusomakwa ziada. Wengi walisema kuwa vitabu vya hadithi havitoshi kwa kila mwanafunzi kutumia katika kipindi kimoja cha maktaba. Hali hii imewanyima wanafunzi fursa ya kujenga mazoea na ari ya kusoma pamoja kwa mwongozo na usimamizi wa mwalimu na hivyo kutinga ukuzaji wa stadi ya kusoma miongoni mwao.

Fauka ya uhaba wa maktaba, utafiti ulionyesha kuwa vitabu vya hadithi havikutosheleza idadi kubwa ya wanafunzi. Vitabu vya hadithi ni nyenzo za kufundisha kusoma kwa ziada na mapana. Kusoma kwa ziada na mapana hukuza stadi ya kusoma na matumizi ya lugha ya wanafunzi (Miricho na Wenzake, 2008). Kutokana na kumudu stadi za kuzungumza na kusoma mwanafunzi hujenga ukwasi wa lugha wa kumsaidia kujieleza vizuri. Ukosefu wa vitabu hivi basi ni kikwazo kwa juhudi za kukuza stadi ya kusoma miongoni mwa wanafunzi.

### 5.2.4 Majukumu ya Wanafunzi

Utafiti linganishi kuhusu majukumu ya wanafunzi ulidhihirisha kuwa kuna tofauti kubwa kati ya wanafunzi waliofundishwa kwa kutumia vitabu vya hadithi ikilinganishwa na wale wasiofundishwa kwavyo. Matokeo yalionyesha kuwa wanafunzi wasiofunzwa stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu hivi walikuwa na matatizo ya kutoweza kusoma. Hata hivyo, wale

waliomudu kusoma kwenye kundi hili walikumbwa na changamoto kubwa ya kusoma kwa kudodosa, kusoma kwa kufuatiliza matini kwa kidole, kumumunya midomo au kusogeza kichwa. Kusoma kwa mtindo huu ni ithibati ya mwanafunzi mwenye matatizo katika usomaji, kuonyesha kuwa hakukuza stadi yake ya kusoma kwa kiwango cha kuridhisha (Mirikau, 2008). Hiki ni kiashiria kinachohalalisha haja ya kutumia vitabu vya hadithi katika ufunzaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma. Utafiti huu ulionyesha kwamba, miongoni mwa walimu waliotumiwa katika utafiti huu walikuwa na mielekeo hasi kuhusu ufundishaji wa stadi za lugha. Mathalani matokeo yalionyesha kuwa baadhi ya walimu hawakuelewa wala kufurahia kufundisha stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Matokeo haya ni ya kuhofisha kwani ufundishaji wa stadi ya kusoma hauwezi kufanikiwa ikiwa wadau wakuu hawawezi kuifurahia kazi yao. Mwelekeo huu si wa kutia moyo kwa sababu mwelekeo hasi wa walimu huathiri ufunzaji wao darasani. Jambo hili ni lazima lichukuliwe hatua ya dharura na washikadau wote wanaohusika na sekta ya elimu. Mwanafunzi anapokosa kufunzwa ipasavyo stadi moja, yeye huathirika katika utendaji wa stadi zote. Mwanafunzi aliye na ugumu katika kuelewa stadi ya kusikiliza na kuandika vile vile hawezi kuelewa stadi ya kusoma. Wambui (2011) alichunguza ufundishaji wa kusoma kwa sauti katika madarasa ya chini katika shule za msingi za taarafa ya Gatanga. Utafiti huo ulibainisha kuwa, watoto wanapokosa msingi mzuri katika stadi ya kusoma hawawezi kufaulu katika masomo yao. Hivyo basi, vitabu vya hadithi vikitumiwa jinsi inavyostahili vinaweza kuwapa wanafunzi msingi bora wa ujifunzaji wa Stadi ya Kusoma.

### 5.3 Hitimisho

Utafiti huu unatuelekeza kuhitimisha kwamba walimu wengi hawazingatii mikakati bora ya kufundisha somo la stadi ya kusoma. Wengi walitegemea matumizi ya vitabu vya kiada tu ambavyo huwanyima wanafunzi fursa ya kusoma kwa mapana na ziada. Hata hivyo, wale wachache ambao hawakutumia vitabu vya hadithi, hawakushirikisha mikakati iliyopendekezwa ya matumizi yake ili kumhusisha mwanafunzi na kumweka katika nafasi ya usukani katika

mchakato wa upataji wa stadi ya kusoma. Utafiti ulionyesha kwamba walimu hawakuzingatia vigezo vya uteuzi vyote wa vitabu vya hadithi. Vigezo hivi ni kama vile kuwachagulia wanafunzi vitabu vya hadithi na kuwahamasisha wavisome wakati wa ziada na hata wakiwa nyumbani. Uchanganuzi wa data zilizopatikana nyanjani kuhusiana na suala la utafiti unatuelekeza katika kuhitimisha kuwa mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi umekumbwa na matatizo ya utekelezaji katika shule za msingi. Hali hii inatokana na ukosefu wa maktaba na vitabu vya hadithi shuleni, idadi kubwa ya wanafunzi inayofanya walimu kutowashirikisha au kutotumia vitabu vya hadithi kwa kuchelea kukosa nafasi ya kushughulikia kila mwanafunzi kibinafsi. Hali hii imemnyima mwanafunzi nafasi ya usukani katika mchakato wa upataji wa Stadi ya Kusoma. Hatimaye, mielekeo na ujuzi wa walimu kuhusu jinsi ya kufundisha stadi zote za lugha inadhihirisha nafasi ya mwalimu kama chanzo kikubwa cha matatizo katika ufundishaji wa stadi hii.

**5.4 Mapendekezo**

Utafiti huu umebainisha kuwa baadhi yawalimu hawakuzingatia vigezo vilivyopendekezwa na Wizara ya Elimu na wataalamu kuhusu jinsi ya kuteua vitabu vya hadithi ambavyo vitaweka msingi mwema wa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma. Hivyo basi, inapendekezwa kwamba Wizara ya Elimu ihakikishe vitabu vya hadithi vilivyochaguliwa ndivyo vinavyotumika katika shule zote za msingi nchini ili pasiwe na utata wowote. Washikadau wa elimu nao wahakikishe vimesomwa na hata kutahiniwa ili kuboresha stadi ya kusoma. Hali hii itawapa motisha ya kusoma zaidi na hata wafikapo katika shule za upili watakuwa na uwezo wa kusoma vitabu vya fasihi bila shida yoyote kwa sababu watakuwa wamepata ari na uzoefu wa kusoma matini mengi. Isitoshe, imejiri kutokana na utafiti huu kwamba, walimu wengi hawahusishi mikakati inayowashirikisha wanafunzi katika ujifunzaji wa stadi ya kusoma. Inapendekezwa kwamba, walimu waimarishe mikakati wanayotumia. Mikakati hii iwe niile inayowashirikisha wanafunzi zaidi. Miongoni mwa mikakati hiini; kuwawekwa katika vikundi kusoma kimoyomoyo kisha mmoja mmoja kusoma kwa zamu wengine

wakimsikiliza, kusikiliza na kusimulia, kuwafanya wanafunzi kuandika insha kurejelea hadithi walizosoma, kuongoza wanafunzi kukariri, kusaidia wenye matatizo. Mikakati hii ambayo huimarisha umilisi wa stadi ya kusoma (Halliday, 1973; Brown, 2007). Katika mbinu zote mwalimu awe mwelekezi huku wanafunzi wakiwa ndio kiini cha mazungumzo.

Kutokana na hali kuwa walimu hawatumii vitabu vya hadithi mara kwa mara kufundishia stadi ya kusoma, tunapendekeza kwamba walimu wahakikishe wamefundisha wanafunzi stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi vya Kiswahili mara kwa mara. Matini na vielelezo vilivyomo kama vile vibonzo vitawawezesha wanafunzi kuimarisha stadi ya kusoma ili kusoma kwa mfululizo na matamshi bora. Baada ya kupata umilisi wa kusoma walimu wawaelekeze wanafunzi ili watumie muda wao vizuri kwa kujisomea vitabu vya hadithi wakiwa nyumbani na wakati mwingine pasipo masomo rasmi. Kupitia usomaji wa vitabu vya hadithi wanafunzi watapata ujuzi wa kuwa wabunifu. Halikadhalika, mikakati inayowapa wanafunzi ari ya kusoma kwa kuwahusisha katika ujifunzaji wakati wa matumizi ya vitabu vya hadithi inafaa kuzingatiwa.

Utafiti umeonyesha kuwa kuna mielekeo hasi kuhusu ufunzaji wa stadi zote za lugha. Mielekeo hasi hudidimiza utendaji katika jambo lolote lile (Babusa, 2010; Njuguna, 2002). Ni jambo la muhimu walimu wa Kiswahili wapewe mafunzo nyanjani yatakayowawezesha kujenga mielekeo chanya kuhusu ufunzaji wa stadi ya kusoma ambayo ni muhimu katika mawasiliano na maingiliano katika jamii. Hivyo basi, utafiti huu umechangia maarifa kwa taaluma ya ufundishaji wa Kiswahili.

### 5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Kutokana na kuwa suala hili la utafiti halijafanyiwa utafiti mwingi nchini Kenya, tafiti zaidi zifuatazo zimeshughulikiwa ili kutoa mwelekeo utakaodhihirisha: Kwanza, kwa vile utafiti huu

ulifanywa kwa wanafunzi wa darasa la nne pekee katika Manispaa ya Kakamega, ipo haja ya utafiti mwingine kufanywa katika maeneo mengine nchini na pia katika madarasa mengine.

Vilevile utafiti mwingine ufanywe kuhusu nafasi ya somo la maktaba katika uimarishaji wa Stadi ya Kusoma miongoni mwa wanafunzi wa Shule za Mingi. Kwa misingi kuwa utafiti huu umejikita katika tathmini ya matumizi ya vitabu vya hadithi katika kufundisha stadi ya kusoma, utafiti wa majaribio kuhusu ubora wa kutumia mkakati wa usomaji wa vitabu vya hadithi kufundishia vipengee vingine vya lugha kama vile uandishi wa insha, imla na vipengele vinginevyo vya Kiswahili unafaa kutekelezwa.

## MAREJELEO


Abbas M. Omar (2017) Maktaba za Skuli from https://ke.linkedin.com>dr.abbas-omar. Alexandria University Egypt. Retrieved on 26th October 2018.

Ahmed, F. & Aziz, J. (2009). *Students Perception of the Teachers Teaching of Literature Communicating and Understanding through the eyes of the Audience*. European Journal of Social Sciences, 7 (3), 17-39.

Aras G. (2012). *Teaching writing through non library formats in Departments of English and literature.* Fronters of language & Teaching, (3 rd ed.), 132 – 138.

Babusa, H. (2010). *Uchanganuzi Linganuzi wa Mielekeo na Umilisi wa Lugha ya Kiswahili wa Wanafunzi Katika Mikoa ya Pwani na Nairobi Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. ( Haijachapishwa).

Baird R. w. (2017). *Baird Annual Report* from Bairdannualreport.com. United Kingdom: Europe Ltd. Retrieved on 26th October 2018.

Bennaars, G. A., J. E. Otiende & B. R. Boisevert (1994). *Theory and Practice of Education*. Nairobi: East Africa Education Publishers Ltd.

Berliner, J. S. (1972). *Economy, Society and Welfare: A study in Social Economies*. New York: Praeger.

Best, J.W. (1992). *Research in Education*. New Delhi: Prentice Hall of India Private Ltd.

Best J.W. & J. V. Khan. (2003). *Research in Education.* New Delhi: Asoke K. Ghosh.

Best, J. W (2004). *Doing your Research* Project: *A guide for First Time Researchers*. New Delhi: Education and Social science.

Bishop, (1995). *Curriculum Development: A textbook for Students*. Hong Kong: Macmillan Education Limited.

Bloom, B.S. (1981). *All children Learning: A premier for Parents, Teachers and Other Educators*. London: McGraw Hill Company.

Brown, H. D. (2007). *Principles of Language Learning and Teaching*. 1( 5). White Plains: New York: Pearson Education.

Brumfit, C. J. & K. Johnson (1985). *The Communicative Approach to Language Teaching.* New York: Oxford University Press.

Bwire, A.M. &L.I. Vikiru. (2008). *Approaches to the Teaching of Grammar And Vocabulary in Groenewegen Bencharks for English language Education*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Cohen, L. & L. Manion. (1994). *Research Methods in Education*. London: Routledge.

Cohen, L. &Wenzake (1996). *A guide to Teaching Practice.* 1( 4). London: Routledge.

Cole, (1971). *Implementation of a Process Curriculum by the Campus Team Strategy*. New York: Eastern Regional Institution for Education.

Collie, J & S. Slater (1987). *Litereature in Language classroom*. Cambridge: Cambridge University Press.

Davis School District Curriculum and Instruction (2016), Key Boarding Practice Materials. http:// www.iste.org./standards/ standards/for students – 2016. Retrieved on 26th October 2018.

Descombe, M. (1998). Good Research Guide for Small – Scale social Research Projects. Buckingham: Open University Press.

Dewey, J. (1916). *Democracy and Education: An introduction to the Philosophy of Education*. New York: The Macmillan Company.

Egesa, D. K. (2006). *Uhakiki wa Matatizo Yanayowakumba Walimu katika Utekelezaji wa Silabasi ya Kiswahili ya Shule za Upili Wilayani Kakamega*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. (Haijachapishwa).

Ellis, R. (2006). *Current Issues in the Teaching of Grammar: An SLA perspective*. Tesol Quarter. London: Oxford University Press.

Flavia, A.T. (2011). *Children`s Literature in African Language Swahili for children in Kenya and Tanzania*. A Journal University of Calabria.

Gall, D., Borg, M. & J. Gall (1997). *Educational Research: An Introduction* 1 (6). New York: London Publishers.

Good, C. (1972). *Essentials of Education Research*. New York: Appleton – Century– crofts.

Gay, L. R. (1992). *Educational Research: Competencies for Analysi and Application.* New York: Macmillan Publishing Company.

Halliday, M.A. (1973). *Explorations in the Functions of Language*. London: Edward Arnold.

Harvey, D. & M. Bizar (1998). *Methods that Matter*. York, Maine: Sternhouse.

Hergenhahn, B. R. & M. H. Olson. (1997). *An introduction to Theories of learning.* 1(5). New Jersey: Prentice-Hall, Upper Saddle River.

Hill, J (1999). *Collocation Competence*. Massachusettes, Allyn & Bacon.

Hopson, B. (1981). *Life Skills Teaching*. London: McGraw Hill Book Co. Ltd.

Ikobwa, V. (2000). *The Extent of constituency between the Kenyan Institute of Education's policy. Guidelines in Teaching Practice in use of Instructional Methods: The case Study of History and Government Teachers in Nandi District*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. (haijachapishwa).

Ipara, O. I. (2006) *Matatizo ya kufundishia Fasihi Simulizi katika shule za Upili. Katika Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communication na CHAKITA.

Iyaya, R. (2010). *Mambo Yanayoathiri Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia. (haijachapishwa).

Karani, E. (1996). *Oral Communication in Kiswahili. A study of selected Secondary Schools in Kakamega District, Kenya*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. (haijachapishwa)

Karukenya, N. (2010). *Walioona shida katika Kiswahili wapatiwe shime*. Taifa Leo, Nairobi: Nation Media Group, toleo la 04.02.2010.

Katz, L. G. (1989). "Afterward. Young Children in cross National Perspective." In: *How Nations Serve Young Children; Profile and Child care of Education in 14 Countries.* (Olmsted, P.P. & D. P. Weikar). Michigan: High/Scope Educational Research Foundation.

Kerlinger, F. N. (1973). *Foundation of Behavioural Research*. New York: Holt Renahart & Winston.

K.I.E. (2002). *Primary School Syllabus*. 1 (1). Nairobi: Kenya Institute of Education.

K.I.E. (2006). *Kiswahili Secondary: Mwongozo wa Walimu*. Nairobi: Kenya Institute of Education

Kimble, G.A. (1961). *Hilgard and Marquis Conditioning and Learning*. 1 (2). New York: Appleton-Century-crofts.

Kombo, K &A. L. D Tromp. (2006). *Proposal and thesis writing: An Introduction.* Nairobi: Pauline Publications Africa.

Kothari, C. (2012). *Quantitative Techniques. (Toleo 3 ).* New Delhi: Vicas Publishing House Limited

Koul, P. (1992). *Research Methodology and Education Research*. New Delhi: Vicas Publishing House Limited

Macharia, S. & L. Wario (1989). *Teaching Practice in Primary Education*. Hong Kong: Macmillan publishers.

Mark, B. & C. Peter. (2001). *An introduction of quantitative Research Methods.* London: SAGE Publications.

Mbuthia, F. K. (1996). *A Comparative Study of Effevt of Two Instructional Approaches on Students Performance in Kiswahili Poetry in Selected Secondary Schools in Eldoret Municipality.* M.phil. Thesis of Moi University. (Unpublished).

Miles, B. M. (1994). *Quantitative Data Analysis*. Saga: Saga Publishers.

Miricho, M. Nganje, D., Kobia, J. & Wacira, D. (2008). *Distinction Kiswahili for Primary Teacher Education.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mirikau, S. (2008). *Msururu wa PTE: Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Moseti, O. (2002*). Swahili Research and Development Needs in Kenya. Katika Inyani S. Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Mugenda, O .M &A.G. Mugenda. (2003). *Qualitative and Quantitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mukundi, E. W. (2009). *A comparative Study of the Effects of Instructional Modes on Performance in Kiswahili Report Writing in Uasin Gishu District Secondary Schools.* Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Moi. (haijachapishwa).

Mulokozi, M. M. (1983). *Utafiti wa Fasihi Simulizi. Katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Musau, P.M. &L. Chacha. (2001). *Mbinu za Kisasa za kufundishiaKiswahili*. Nairobi: K.L.B.

Mwangi, P. K. (1998). *Uhusiano Uliopo Kati ya Mitazamo ya Lugha ya Wanafunzi waKidato cha nne na Utendaji wao: Hali ya Kiswahili Katika Taarafa ya Maseno*. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Moi.

Natwart, R. N. (2009). *Uchanganuzi wa Mbinu za Kufundishia Hadithi Fupi katika Shule za Sekondari Wilayani Kakamega Kenya*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. (Haijachapishwa).

NESSP (2013-2018). *NESSP (National Educational Sector Support Programme)* www.education.go.ke. Access date 27th October 2018.

Ngugi P.M.(2016) *Mgazeti kama Kichocheo cha kuendeleza Fasihi ya watoto: Mfano kutoka Daily Nation na Taifa Leo. Katika Kiswahili na utandawazi*. Mh.Mwita C.L. Nairobi: Twaweza communications.

Njogu, K. & Nganje, D.K. (2011). *Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njuguna, N. (2002). *Verbal Classroom Interaction Patterns of Selected Secondary School, Homescience Teachers with their students in Nairobi Province, Kenya*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Nkapa, N. (1997). *Educational Research for Modern Schools.* Enugu: Fourth Dimensional Publishing Company Limited.

Nsubugha, E.H. K. (2000). *The Teacher as a Professional.* Kampala: MK. Publishers Ltd.

Openhein, J.O. (2003). *Questionnaire Design. Interviewing and Attitude Measurement.* London: Continumn.

Ornstein, A.C. & Wenzake (2000). *Strategies for Effective Teaching*. New York: McGraw Hill.

Orodho, I. (1996). *Social Sciences Environmental Improvement in Kenya*. Addis Ababa: Bereau of Education Research.

Orodho, J.A. (2002). *Elements of Education & Social Science Research Methods*. Nairobi: Masola Publishers.

Peil, M. (1995). *Social Science Research Methods: A Handbook for Africa*. Nairobi: East Africa Education Publishers.

Picciano, A. G. (2004*) Educational Research Primer*. London: continuum

Press Reader (2017). *Umuhimu wa Maktaba*. Kutoka Pressreader https://www.pressreader.com> mtanzania.Toleo la 26/10/2018.

Quist, D. (2000). *Primary Teaching Methods.* Malaysia: Macmillan Education Limited.

Republic of Kenya. (1981). *Kenya Education Commission Report*. Nairobi: (Mackay Report) Government Press.

Rodgers, S. (1976). *Approaches and Methods in Language Teaching. A Description and Analysis.* Cabridge: Cabridge.University Press

Schroeder, S. (2011 w). *What readers have and do: Effects of students' verbal ability and Reading time components on comprehension ith and without text availability.* Journal of Educational Psychology. (4), 877-896).

Schultz & Schultz (1987). *A Neural Substrate of Predication and Reward*. Science. 275: 1593-1598.

Shiundu, J. & S. Omulando. (1992). *Curriculum Theory and Practice.* Oxford University: Nairobi, Kenya.

Simiyu, A. (2001*). System approach to teaching: A Handbook for Teachers*. Eldoret: Western Publishing Press.

Singleton, R. A. (1993). *Approaches to Social Rresearch*. New York: O. U. P.

Sitima, T. (1988). *Issues of Implementation of 8-4-4. Programme and Inspection of School. Report of Educational Administration Conference*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Skinner, B.F. (1957). *Verbal Behaviour*. New York: Appleton.

Skinner B. F. (2003). *Educational Psychology*. (Toleo 4). New York: Prentice Hall India Private Limited.

Sotto E. (1994). *When Teaching Becomes Learning*. *A Theory and Practice of Teaching.* London: Continuum.

Taylor, B.M., B.J. Frye & G.M. Maruyama. (1990). *Time Spent Reading and Reading Growth*. American Educational Research Journal, 27( 2), 351-362.

Teale, W.H.(2003). *Reading aloud to young children as a classroom instructional activity: insights from research and practice.* In A Van Kleek, S. A. Stahl E.B. Bauer. On Reading Books to Children. 2(1), 114-139). Mahwah, Nj: Lawrence Erlbaum.

Tuntufye, N. (1977). *Jinsi ya kufundisha Kiswahili*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Uwezo Kenya (2010). *Are Our Children Learning*? Nairobi, Kenya.

Uwezo Kenya (2011). *Are our children Learning. Annual Assessment* from www.org/wp-content/upload/2012/05/Uwezo2011.Access date 15th May 2018.

Wairimu, A. M. (2000*). Factors Influencing the Performance of Kiswahili in KCPE in Dagoreti Division, Nairobi Province*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Wambui, M. (2011). *Ufundishaji wa Kusoma kwa Sauti Katika Madarasa ya Chini Katika Shule za Msingi Tarafa ya Gatanga*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Wanjala F.S. & J. M. Kavoi. (2013). *Stadi za Mawasiliano na mbinu za kufundishia Kiswahili*. Nairobi: Kenya.

Wanyonyi, K. M. (2015). *Tathmini ya mikakati ya stadi ya kusikiliza kama njia ya Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule za upili katika Kaunti Ndogo ya Nandi Kaskazini.* Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. (Haijachapishwa)

Wasike, C. K. (2007). *Uchanganuzi wa Mikakati ya Kufundishia Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika Shule za Upili Wilayani Bungoma.* Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. (Haijachapishwa).

Watson, S. M. R., R. A. Gable, S. B. Gear & K. C. Hughes. (2012). *Evidence-based strategies for improving the reading comprehension of secondary students: Implications for students with learning disabilities.* Learning Disabilities Research & Practice, 27,79

Wizara ya Elimu (2006). *Kiswahili Sekondari: Mwongozo wa Walimu*. Nairobi: K. I. E.

Yuko, W. & D. Onen (2005). *A Handbook for beginning Researcher*. Nairobi: Otiona Press Publication.

Yuko, O. W. & D. Onen. (2005). *AGeneral Guide to Research Proporsal and Report*. Kisumu: Options Printers and Publishers.

## VIAMBATISHO

**KIAMBATISHO 1: Hojaji ya Mwalimu**

**Utangulizi**

Kwa mwalimu,

Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika Elimu ya Kiswahili kwenye chuo kikuu cha Masinde Muliro Sayansi na Teknolojia. Ninafanya utafiti kuhusu mada ya "Uchunguzi ya mikatiti inayotumiwa kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi", kama sehemu ya mahitaji ya shahada hii. Wewe kama mwalimu wa Kishwahili umeteuliwa kutoa maoni, mtazamo na mawaida yako ambayo itakuwa mchango mkubwa kwa huu utafiti. Kwahivyo, unaombwa kujaza hii hojajikwa uangalifu.

**Maagizo.**

Tafadhali jaza nafasi katika hojaji uliyopewa.Haina haja ya kuandika jina lako. Maelezo utakayotoa yatatumiwa tu kwa kusudi la uchunguzi huu na yatahifadhiwa sana wakati wa baada ya utafiti.

**SEHEMU YA A: Maelezo Kuhusu Mwalimu**

Tarehe__________________________________________

1. Aina ya shule: (a) Shule ya umma ☐
   (b)Shule ya kibinafsi ☐

2. Jinsia (a) Kiume ☐
   (b) Kike ☐

2. Kiwango chako cha mafunzo ya kitaaluma
   a) P1 ☐
   b) Stashahada ☐

c) Shahada B.E.D/BA ☐

4. Tajriba yako kama mwalimu ni:

a) Chini ya miaka 5 ☐

b) Zaidi ya miaka 5 ☐

**SEHEMU YA B.**

1. Kuna wanafunzi wangapi katika darasa lako? Wasichana ☐

Wavulana ☐

2. Unatumia vigezo vipi kuteua vitabu vya hadithi kwa kufundishia stadi ya kusoma.

(a)

(b)

(c)

(d)

3. Ikiwa kuna vigezo vingine vitaje?

________________________________________

________________________________________

________________________________

2 Unatumia mikakati ipi kumsaidia mwanafunzi ili aweze kusoma kwa ufasaha?

a. Kuhamasisha wanafunzi kusoma kwa zaida ☐

b. Kuwachagulia vitabu faafu kwa viwango vyao vya kuwafurahisha na kuwaburudisha ☐

c. Kuwahimiza wasome kwa kasi wakifulululiza ☐

d. Kuwapa vitabu vya kujisomea nyumbani na kuorodhesha vitabu vilivyosomwa na kilamwanafunzi ☐

e. Kuwafanya wanafunzi kuandika insha kurejelea hadithi walizosoma ☐

f. Kuhakikisha vitabu vinarejelea mazingira na tajriba zao

(umri wao,maadili na tamaduni zao) ☐

g. Kuhakikisha vinakuza msamiati,istilahi na miundo ya sentensi za wanafunzi. ☐

4 Ikiwa wapo unatumia mikakati ipi kuwasaidia ili waweze kusoma vitabu vya hadithi kwa ufasaha

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

____________________________________________________

5 (a) Wanafunzi husoma vitabu vya hadithi?

(i) Ndio ☐

(ii) La ☐

(b) Ikiwa jibu ni ndio taja vitabu ambavyo wanafunzi husoma.

(c) Vipindi vingapi vimetengewa kusoma vitabu vya hadithi kwa jumla

i) Kipindi kimoja ☐

ii) Vipindi viwili ☐

iii) Muda wa ziada ☐

6 Ni changamoto zipi zinazowakumba wanafunzi wakati wa kusoma vitabu vya hadithi?

a) Kumumunya midomo ili kutamka kila sauti. ☐

b) Kusoma kwa kufutiliza kidole au kusongeza kichwa. ☐

c) Kusoma kimoyomoyo huku akitamka kila neno kwa sauti ya chini. ☐

d) Kusoma akisitasita.kwa kutamka neno moja moja. ☐

e) Kusoma kwa kurudia au kuruka maneno bila kukusudia. ☐

7. Taja changamoto zingine mbali na zile ambazo zimewakumba wanafunzi wako?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

____________________________________________________

8.Kuna maktaba ya shule?

(a) Ndio ☐

(b) La ☐

9 .Vitabu vya hadithi vinatosha kwa kila mwanafunzi kutumia.

(a)Ndio ☐

(b)La ☐

10. Ikiwa ni vichache,eleza jinsi unafundisha kipindi hicho cha kusoma vitabu vya hadithi?

a) Hawasomi vitabu vya hadithi ☐

b) Wanawekwa katika vikundi ☐

c) Mwanafunzi mmoja anasoma wengine wakimsikiza ☐

d) Mwalimu anasoma wanafunzi wakisikiliza ☐

11. Kuna wanafunzi darasani mwako ambao hawana uwezo wa kusoma

(a) Ndio ☐

(b) La ☐

13.Mwalimu anatumia nyenzo zipi katika kufundisha somo hili? ___________________________

______________________________________________________________________________

14.Je,mazingira ya shule yanamruhusu mwanafunzi kusoma vitabu vya hadithi?.........................

15. Onyesha stadi zifuatazo kulingana na utaratibu wa kupenda kwa wanafunzi wako wakati wa kufunza.

